SUPA JACKPOT
TZS. 1,059,844,733
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4

**POLISI:** Dereva tukimkamata amelewa ni mahakamani tu




UKURASA 13

# Nipashe

Ijumaa Desemba 23, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581168

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## UJAZAJI MAJI BWAWA LA NYERERE

# Vigogo wenye ng'ombe maelfu waingia matatani

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo ya Waziri wa Nishati, January Makamba pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme (TANESCO), Maharage Chande (kushoto), kuhusu Kituo cha Kusafirishia Umeme (Switchyard) kwenye Mradi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) mkoani Pwani jana. **PICHA: IKULU**

# Bei za vyakula zazidi kupaa




UKURASA 3

# Mbaroni kwa tuhuma za uzushi dhidi ya Samia, JK

UKURASA 3

MICHEZO MAYELE AJAZWA NOTI NBC UK. 28

KATUNI UK. 6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa waraka wa Bodi ya Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Katibu Mtendaji wa (MCT), Kajubi Mukajanga, wakati wa mazungumzo na uongozi wa Baraza la Habari Tanzania yaliyofanyika Ikulu jana. **PICHA: IKULU**

# Vigogo wenye ng'ombe maelfu waingia matatani

**Na Maulid Mmbaga,** RUFIJI

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema hakuna aliye mkubwa zaidi ya sheria za nchi, akiagiza kuchukuliwa hatua dhidi ya wote wanaodaiwa kutunishia misuli wakuu wa wilaya na mikoa kwa kuingiza mifugo kwenye ardhi oevu.

Akizungumza jana wakati wa hafla ya ufungaji lango litakaloruhusu maji kuanza kujaa kwenye Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Nyerere (JNHPP), Rais Samia alisema manufaa ya bwawa hilo yataonekana endapo vyanzo vinavyopeleka maji vitatunzwa.

Alisema Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alitoa maelekezo ya kuondolewa kwa mifugo yote kwenye Bonde la Ihefu, huku akiwataka wakuu wa mikoa kusimamia kikamilifu na uwezo wa vijiji uangaliwe kabla ya kupeleka mifugo huku kukiwa na msisitizo wa kufuata sheria na kanuni ikiwamo kuzingatia haki za binadamu katika utekelezaji wake.

"Tuna uzoefu wa mapigano ya wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Kilosa, Mkuu wa Wilaya alipoulizwa 'kwanini kwako kuna wengi wanakufa kutokana na matukio haya?' alisema 'ng'ombe wengi wanaoingizwa ni wa wakubwa, nami siwezi kuwagusa'.

"Sasa ninataka kusema hakuna mkubwa mbele ya sheria, hakuna mkubwa mbele ya kulinda rasilimali hii tuliojenga kwa fedha nyingi, mradi mkubwa na wa mkakati, hakuna mkubwa atakayetuharibia mradi huu. Ninawaomba wakuu wa wilaya, mikoa, mkafanye kazi yenu, ambaye ataogopa wakubwa anyoshe mkono wakubwa wamshughulikie," aliagiza.

Rais Samia alielekeza wanaochepusha maji kwenye Bonde la Mto Rufiji, wazuiwe ili yaingie kwenye mkondo wake, huku akitaka kanuni za mgawanyo wa maji kuzingatiwa pamoja na vibali kutotolewa uwanda wa juu bali wa chini ya mradi.

"Tuna taarifa kwamba Ruaha Mkuu utachangia maji kwa asilimia 15, ninawaomba watu wa Iringa na Mbeya kuacha wanayofanya (uharibifu) ili maji yafuate mkondo wake. Morogoro na Iringa Mto Kilombero unachangia asilimia 65, Mto Luwegu asilimia 19, ninawaomba sana watu wa maeneo haya kutunza mazingira (ili) makisio ya kujaza maji yaende kama tulivyokusudia," aliagiza.

Mkuu wa Nchi alisema mradi huo umejengwa kwa gharama kubwa na kwa kujinyima vitu vingi muhimu, hivyo itakuwa alichokiita dhambi kubwa kama hawatatimiza malengo kwa sababu ya uzembe na ubinafsi wa watu wachache.

"Kulinda mazingira kwa ajili ya mradi huu sasa ni suala la kufa na kupona, waziri pamoja na wakuu wa mikoa wasimamie kikamilifu utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji kwenye mabonde yetu likiwamo la Mto Rufiji," aliagiza.

**MANUFAA YA MRADI**

Rais Samia alisema mradi huo utaleta umeme wa uhakika kwa ajili ya maendeleo endelevu, huku akiwashukuru wote walioshiriki kuanzia wazo na hata utekelezaji wa mradi huo, akisisitiza kazi hiyo ni kubwa na ya viwango vinavyotakiwa.

"Hatuwezi kuzungumzia mafanikio bila kutaja aliyeanzisha mawazo ya mradi huu na ncha yake, ni Mwalimu (Julius) Nyerere na marehemu (Dk. John) Magufuli.

"Niwapongeze Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kampuni na Serikali ya Misri, China, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na wafanyakazi walioshiriki utekelezaji unaoendelea kufanywa," alipongeza.

Rais Samia aliongeza kwamba hatua waliyofikia katika utekelezaji wa mradi huo ni kubwa, huku akionyesha kufurahishwa na maendeleo yake, akiahidi atahakikisha unakamilika kwa viwango na kwa wakati ulivyopangwa.

Alisema Watanzania wana kila sababu ya kujivunia mradi huo ambao ni miongoni mwa miradi mikubwa barani Afrika, akifafanua kuwa bwawa hilo litaweka akiba kubwa ya maji na kuzalisha umeme hata pale mvua itakapokuwa imepungua.

Pia alisema bwawa hilo litasaidia kudhibiti mafuriko ya mara kwa mara ya Mto Rufiji na kuwezesha kilimo cha uhakika cha umwagiliaji.

Rais pia alisema mradi huo utafungua na kuimarisha fursa nyingi za utalii kwenye eneo la kusini mwa Tanzania hususani Hifadhi ya Nyerere na kutoa ajira za uhakika, akiwakumbusha kuwa wakijipanga vizuri sekta nyingi zitanufaika.

"Nitoe maelekezo kwa sekta ya kilimo, mradi huu unakwenda kufungua fursa ya kilimo cha umwagiliaji, ninatambua kuna eneo la ekari 400,000 kwenye uwanda wa chini linaloweza kutumika kwa kilimo, ninaelekeza Wizara ya Kilimo pamoja na Ardhi na TAMISEMI, mkayapime maeneo na kuyaweka kwenye maeneo makubwa na kufanya mnada wa wazi kwa wawekezaji wa uhakika.

"Bwawa hili pia litatoa fursa ya uvuvi, Wizara ya Uvuvi na Mifugo ije na mpango mahususi kwa ufugaji wa kisasa wa samaki ili tukuze uchumi," alielekeza Rais Samia.

**MAJI YAENDE DAR**

Kiongozi huyo pia alisema maji yanayopita kwenye mradi huo ni mengi na yanaweza kusaidia upatikanaji wa maji safi kwenye Mkoa wa Dar es Salaam.

Kwa kutambua hilo, Rais Samia aliwaelekeza Waziri wa Maji pamoja na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuangalia namna ya kutumia maji ya Mto Rufiji, utoe fursa ya kuanza ujenzi wa kituo cha kupokelea maji, yasafishwe na yatumike Dar es Salaam.

"Suala hili ni muhimu sana kwa sababu hatuwezi tena kutegemea Mto Ruvu kutosheleza Jiji la Dar es Salaam, hivyo maji ya Mto Rufiji yatumike kwenye maeneo hayo," aliagiza Rais Samia.

Katika hafla hiyo, Waziri wa Nishati, January Makamba aliwashukuru wadau wote wakiwamo viongozi, TANAPA, Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), vyombo vya ulinzi na usalama, Wakala wa Barabara (TANRODS), TANESCO ma wafanyakazi zaidi ya 12,000 kwa kujitoa na kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa viwango vinavyoonekana.

"Mradi huu ni wa fedha nyingi na pale kunapochelewa malipo kwa mujibu wa mkataba kuna adhabu. Tumejitahidi kuweka kipaumbele cha kulipa fedha za mradi huu, na hii ni ishara ya dhamira njema ya kutaka mradi huu ufanikiwe.

"Maneno yote yanayoendelea kuwa mradi huu unahujumiwa ni ya uongo na unaendelea kama inavyotarajiwa. Kusimamia mkataba mkubwa kama huu si kazi rahisi, tumepishana mara nyingi lakini tulitenganisha usimamizi wa mkataba na mambo mengine, hiyo ilisaidia mradi kuendelea kama inavyotarajiwa.

"Na ili kuongeza kasi na umahiri, tuliamua kazi ifanyike usiku na mchana, na tumekuwa na ushirikiano na viongozi wenzangu na Serikali ya Misri katika kuhakikisha tunakamilisha utekelezaji wa mradi huu," alisema.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alisema Bwawa wa Nyerere lina ukubwa wa kilomita za mraba 915, mita za ujazo bilioni 32.3, mitambo tisa ambayo kila mmoja utakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati za umeme 235.

Pia alibainisha kuwa bwawa hilo ambalo limejengwa eneo unakopita Mto Rufiji na ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, liko katikati ya mikoa ya Pwani na Morogoro na lina vyanzo vitatu vya kuingiza maji ambavyo ni Mto Kilombero, Luwegu na Ruaha.

"Mradi huu umejengwa kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira. Kabla haujaanza kulifanyika utafiti na kuhimiza masuala yote ya mazingira yanayopaswa kufuatwa na yote yamezingatiwa katika utekelezaji wa mradi huu na mengine yote yakiwamo yanayohusu Kihansi," alisema Chande.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Misri, Sameh Shoukry, alipongeza Serikali ya Tanzania kwa uthubutu wa utekelezaji wa bwawa hilo, akieleza kuwa litakuwa na manufaa makubwa kwa wananzania, ikiwamo kutatua tatizo la upungufu wa umeme.

"Maono yetu ni kuhakikisha mradi huu unakamilishwa kwa viwango vya kimataifa, utaalamu huu ambao Misri imeuleta ni heshima ya kipekee ambayo imeamua kuileta kwa Watanzania, pia ushirikiano wa utekelezaji wa mradi utasaidia kuongeza uwekezaji Tanzania," alisema Shoukry.

Mkuu wa Mkoa wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliahidi mkoa huo utahakikisha ulinzi wa vyanzo vya maji ili kulinda uhai wa bwawa hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatuma Mwasa, alisema watashirikiana na wananchi kuhakikisha vyanyo vya maji ikiwamo mito inayoingiza maji kwenye mradi huo inalindwa ili iendelee kujaza maji bwawani.

Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, alisema utekelezaji wa mradi huo ni moja ya ahadi na utekelezaji wa Ilani ya CCM, huku akiahidi kuwa chama hicho kitaendelea kuhakikisha kinafuatilia utekelezaji wa mradi huo ili ukamilike kwa asilimia 100.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, alisema wataendelea kuunga mkono jitihada zinazofanyika katika kukamilisha utekelezaji wa miradi mikubwa na ya maendeleo inayofanyika nchini.

Alisema mradi huo utasaidia katika shughuli mbalimbali katika mikoa ya Morogoro na Pwani, zikiwamo za kilimo na ufugaji ambazo zitachochea kukua kwa uchumi wa wananchi.

HABARI KITAIFA

## Mbaroni tuhuma kusambaza taarifa za uongo kuhusu Rais

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam kwa kushirikiana na timu maalum ya kuzuia na kupambana na makosa ya mtandao, limewakamata watu 11 kwa tuhuma za makosa ya kimtandao.

Watu hao wamekamatwa kwa tuhuma za kusambaza taarifa za uongo na uzushi zinazomhusu Rais Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine wakuu wa serikali.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Polisi Kanda hiyo, Muliro Jumanne, watuhumiwa hao wamekamatwa kutokana na ufuatiliaji unaoendelea kufanywa na timu maalum.

Akiwataja waliokamatwa kuwa ni Alex Magoti (26) mkazi wa Tabora Mjini na wenzake wanane kwa tuhuma za kumiliki runinga za mtandaoni na akaunti za mitandao ya kijamii ambazo zimekuwa zikitumika kusambaza taarifa hizo.

"Watuhuhumiwa hao wamekuwa wakiweka taarifa za uzushi, uongo na upotoshaji kwenye runinga za mtandaoni zinazotambulika kwa majina ya BSUN Online TV, GATTU Online TV, TAMUTAMU Online TV, KILIMANJARO Online TV na nyinginezo," alisema.

"Mfano wa taarifa hizo ni kama "Rais Samia akosoa vikali utawala wa Rais JPM, aanika ukatili aliofanya (haukubaliki hata kidogo), imevuja video ya Mbowe apewa shavu, deni la taifa laibua mazito, Mwigulu kutumbuliwa, ghafla mke wa Magufuli afa, itakutoa machozi ukweli wote kifo cha Magufuli," alibainisha taarifa hiyo.

Jeshi hilo pia limemkamata Joseph Mzava (19) mkazi wa Kinondoni Dar es Salaam, mwanafunzi wa mwaka wa kwanza Chuo cha Elimu ya Biachara (CBE) kwa tuhuma za kujinasabisha kuwa yeye ni Rais Mstaafu Jakaya Kikwete na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kupitia mtandao kwa kutumia laini za simu zenye usajili usio na majina yake.

Mtuhumiwa mwingine ni Li Naiyong (48) raia wa China, ambaye anatuhumiwa kujihusisha na shughuli za kuingilia mfumo wa mawasiliano kinyume cha taratibu za nchi na kuisababishia serikali hasara ya Sh. 221,163,600.

"Mtuhumiwa huyo amekuwa akitumia vifaa visivyo rasmi kuwaunganisha watu kwa simu kufanya mawasiliano nje ya nchi kinyume cha Sheria za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)," alisema.

Muliro alisema watuhumiwa hao walikutwa wakiwa na vifaa mbalimbali ambavyo wanavitumia kufanya uhalifu huo ikiwamo simu za mkononi 23.

Kamanda Muliro alitaja baadhi ya vilivyokamatwa kuwa ni laini za simu 437 za kampuni mbalimbali za huduma za simu zenye usajili wa watu tofauti na kompyuta mpakato sita.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, akizungumza katika kikao cha wizara na kampuni zinazofanya kazi ya urasimishaji Dar es Salaam jana. Wa pili kushoto ni Kamishna wa Ardhi Msaidizi, Shukran Kyando. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Sababu kupaa bei ya chakula

**Na Jenifer Gilla**

WAFANYABIASHARA wa nafaka kwa bei ya jumla jijini Dar es Salaam, wamesema sababu za kupaa kwa bei ya vyakula imetokana na upungufu wa uzalishaji shambani kwa kukosekana kwa mvua za kutosha.

Kwa mujibu wa taarifa za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), za Januari hadi Novemba, mwaka huu zimeonyesha baadhi ya nafaka na bidhaa za mazao zilipanda bei na kuchangia mfumuko huku nyingine zikishuka.

Nafaka zilizopanda bei ni mchele na maharagwe huku unga wa mahindi, ngano, mafuata ya kupikia, samaki wabichi, dagaa, soya na choroko zikipanda na kushuka kwa tofauti ya kila mwezi.

Vyakula vilivyoshuka bei na kubaki kwenye bei ya awali kwa kipindi chote ni mboga za majani, viazi vitamu, mihogo, ndizi za kupika na karanga.

Wafanyabiashara hao wamedai uamuzi wa serikali kuruhusu watu wa nje ya nchi kununua bidhaa hizo moja kwa moja shambani kumechangia kupanda kwa bei nchini kwa sababu wananunua kwa bei ya juu na wakulima kuwataka wazawa kununua bei hiyo.

Mfanyabiashara wa maharagwe katika soko la Tandika, Shekhe Mbwana, alisema kutaonyesha kwa mvua kwa misimu mitatu kumeathiri shughuli za kilimo hivyo kupunguza upatikanaji wa nafaka nchini hali inayochangia kupanda kwa bei.

Alisema baadhi ya mikoa iliyokuwa vinara wa kuuza maharagwe ikiwamo Arusha, Sumbawanga na Morogoro kwa sasa haina bidhaa hiyo kutokana na ukame na sasa wanategemea mikoa ya Bukoba na Makambako.

"Kwa sasa bei ya jumla ya maharagwe tunauza kuanzia Sh. 2,800 kwa maharagwe ya kombati na hii imeshuka tulikuwa tunauza Sh. 3,300, na bei ya juu ni Sh. 3,500 haya ni maharagwe ya njano ambayo upatikanaji wake umekuwa wa shida ndio maana bei ipo juu," alifafanua.

Naye mfanyabiashara wa mchele katika soko la Buguruni, Salma Rashid alisema bei ya mchele shambani kutokana na ugumu wa kupatikana nafaka hiyo hali inayosababisha kupanda kwa bei hizo huku watu wa hali ya chini wakiteseka zaidi.

Aidha, alisema ukiacha uhaba wa mvua sababu nyingine ya kupanda kwa bei ya chakula ni kitendo cha wafanyabiashara kutoka nje ya nchi kwenda kununua bidhaa hiyo kwa bei ya juu shambani na kusababisha wakulima kutaka wazawa wanunue kwa bei hiyo.

"Mimi sina tatizo na serikali kufungua mipaka, lakini wasiwaruhusu wageni kwenda shambani kuchukua mazao kama wanavyofanya Watanzania kwa sababu wale wananunua bei ya juu wanalipa kwa dola, sasa wakulima wakiona hivyo wanataka na sisi tulipe bei hiyo hiyo, kwa hivyo na sisi inabidi tupandishe bei," alisema.

Mfanyabiashara wa duka la nafaka la rejareja, Mwajabu Salehe, alitaja baadhi ya vyakula vilivyopanda kuwa ni mchele ambao mwezi uliopita alikuwa akiuza kuanzia Sh. 2,600 hadi 3,500, lakini mwezi huu anauza Sh. 2,800 hadi Sh. 3,500, huku maharagwe akiuza kuanzia Sh. 3,400 hadi 4,500, ngano ya kilo tano anauza Sh. 13,000 kutoka Sh. 11,500.

"Bei ya mchele inabadilika kila siku, kila ukienda shamba unakuta bei imepanda katika kila aina ya mchele, sasa kwa hali hii wanaoteseka ni watu wa hali ya chini, kama mimi wa bei ya jumla nauza mchele kilo Sh. 2,700 hadi Sh. 3,200 rejareja atakwenda kuuza Sh. 3,000 hadi 3,500, mtu wa hali ya chini ataweza kumudu hiyo gharama? Serikali iliangalie suala hili kwa makini," alisema Salma.

Naye Mfanyabiashara Rajab Ramadhani, alisema ili kuzuia kupaa kwa bei ya nafaka hasa kupindi hiki cha msimu wa sikukuu, serikali igawe vyakula walivyohifadhi kwenye maghala vitakavyouzwa bei nafuu kwa wananchi.

"Sisi hatupendi kuuza bei ya juu, lakini mazingira yanatubana kwa hiyo kwa msimu huu wa sikukuu serikali ituletee chakula walichohifadhi kwenye maghala watuuzie bei nafuu ili na sisi tuwauzie watu wa hali ya chini bei ambayo wataweza kuimudu," alisema.

Mtaalamu wa mabadiliko ya tabianchi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Pius Yanda, alisema mabadiliko ya tabianchi yamesababisha mvua kutotabirika.

Aidha, alisema kuwa tabianchi pia inasababisha kuwapo kwa joto kali na kwa sasa limefikia nyuzi joto 1.09 ambalo husababisha kuwa kali na kuathiri ukuaji wa mazao, ukame na kukauka kwa vyanzo vya maji.

Wakati huo huo, ripoti ya Jopo la Kiserikali la Kimataifa linalishughulika na athari za mabadiliko ya tabianchi (IPCC), inatahadharisha kuwa kama joto hilo lisipodhibitiwa na kufika nyuzijoto 1.5 usawa wa bahari hali itakuwa mbaya zaidi.

Taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Septemba 2, mwaka huu, ilieleza kuwa maeneo ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani, lakini anajipa moyo mambo yatakuwa tofauti.

Vilevile, ilifafanua kuwa kutakuwa na ongezeko la joto katika msimu wa vuli hususani katika maeneo ya Kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar, Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

## Jela miaka 30, kazi ngumu kwa kumnajisi bintiye

**Na Friday Simbaya,** MUFINDI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Mufindi imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela na kazi ngumu Ayubu Nyigo (30) kwa kosa la kumnajisi mwanawe wa kumzaa ambaye ni mwanafunzi wa darasa la saba mwenye umri wa miaka 13.

Nyigo, mkazi wa Kijiji cha Itimbo wilayani Mufindi, alidaiwa kutekeleza tukio hilo Julai 7, mwaka huu, majira ya saa 4:00 usiku alipotoka kilabuni kunywa pombe. Baada ya kufika nyumbani kwake, alidaiwa kumfuata mwanawe chumbani alikokuwa amelala na wadogo zake kisha kwenda naye chumba kingine.

Mwathirika wa tukio hilo (jina linahifadhiwa) kwa sababu za kimaadili aliiambia mahakama kuwa baada ya kupelekwa kwenye chumba kingine, baba yake alimvua nguo kisha na yeye kufungua zipu ya suruali na kumziba mdomo hatimaye akaanza ukatili huo.

Mtoto huyo alidai kuwa baada ya kufanyiwa kitendo hicho, baba yake alitishia kumuua kama angetoa taarifa mahali popote.

Hata hivyo, asubuhi ilipofika baada ya kuona anapata maumivu ya tumbo, alikwenda kumweleza jirani yake ambaye ni mama yake mdogo, kwa kuwa nyumbani alikuwa anaishi yeye, wadogo zake na baba yao. Mama yao alifariki dunia miaka michache iliyopita.

Baada ya kumweleza mama yake mdogo, alilipeleka jambo hilo katika serikali ya kijiji na mtuhumiwa alikamatwa kisha kufikishwa mahakamani. Mtuhumiwa baada ya kufikishwa mahakamani, alikana kutenda kosa hilo licha ya kwamba uchunguzi wa daktari ulibaini kuwa mtoto huyo aliingiliwa kinguvu kwa kuwa alionekana ana michubuko katika sehemu za siri.

Kesi hiyo ya jinai imesimamiwa na Wakili wa Serikali mwandamizi Twide Mangula na ilikuwa na mashahidi watatu.

Akisoma hukumu hiyo juzi, Hakimu Mkazi Mwandamizi Edward Uphoro, alisema kutokana na ushahidi uliotolewa, mahakama imemtia hatiani Nyigo na kumhukumu kifungo cha miaka 30 jela na kazi ngumu ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye nia ovu kama hiyo.

Mtuhumiwa alipopewa nafasi ya kujitetea, aliiomba mahakama impunguzie adhabu lakini upande wa mashtaka uliomba mahakama kutoa adhabu kali.

# 'Dereva akinaswa amelewa, moja kwa moja mahakamani'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi limesema asilimia 75 ya ajali za barabarani nchini zinasababishwa na uzembe wa madereva kutokana na ulevi wakiwa safarini.

Kutokana na kadhia hiyo, jeshi hilo limesema madereva watakaobainika wamelewa wakati wakiwa safarini, moja kwa moja watafikishwa mahakamani badala ya kutozwa faini na adhabu nyingine.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, alibainisha hayo jana alipotoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu hali ya ulinzi na usalama nchi kuelekea sikukuu ya Krismasi.

Kamanda Misime alisema kuwa kutokana na utafiti uliofanywa muda mrefu na jeshi hilo, imebainika ajali nyingi za barabarani zinasababishwa na uzembe wa madereva wa vyombo vya moto.

"Jeshi limejipanga kuwashughulikia madereva wanaoleta uzembe barabarani, hatuhitaji kila wakati kumsingizia Mungu kila ajali inayotokea barabarani," alisema Misime.

Kuhusu kuwafikisha mahakamani madereva wanaovunja sheria za usalama barabarani, Misime ni hatua iliyofikiwa na jeshi hilo ili kudhibiti ajali nchini.

Alisema madereva wanabeba vinywaji na wanavitumia katika safari wakati wanajua vitawaathiri.

Alisema wameamua kufanya hivyo ili kuepusha ajali za barabarani zisizokuwa na vyanzo vya kueleweka.

Kuhusu hali ya usalama, Misime alisema iko shwari na askari wanaendelea na doria ili kuhakikisha raia wanakuwa salama.

Alisema jeshi hilo limewaomba viongozi wa dini kusaidia kuimarisha kamati za ulinzi na usalama ili kusaidiana kuzuia ajali zinazosababishwa na uzembe wa madereva.

Pia alizitaka mamlaka za serikali za mitaa kushirikiana na Jeshi la Polisi kuanzisha na kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi ili visaidie kufanya doria mitaani.

Misime pia aliwataka madereva kulinda usalama wao wenyewe badala ya kusubiri mpaka jeshi hilo liwakamate ndipo waanze kufuata sheria za usalama barabarani.




Miili ya askari wanandoa, Noah Simfukwe na Angness Kiyeyeu waliofariki katika ajali ya gari ndogo kugongana na basi eneo la Tanangozi Wilaya ya Iringa ikiagwa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Miili ya wanandoa askari yaagwa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MIILI ya askari wanandoa, Nohan Simfukwe (30) na Agnes Kiyeyeu ((27), waliofariki dunia baada ya gari ndogo waliokuwa wakisafiria aina ya Toyota Vits kugongana uso kwa uso na basi la Kampuni ya Luwinzo, iliagwa jana Iringa kwa ajili ya kwenda kuzikwa mkoani Mbeya.

Wanandoa hao walikutwa na mauti wakati wakisafiri kwenda Mbeya kwa ajili ya kusherehekea sikikuu ya Krismasi.

Akizungumza wakati wa ibada ya kuaga miili hiyo iliyofanyika katika viwanja vya polisi Wilaya ya Iringa, Kamishna wa Utawala na Rasilimali Watu wa Jeshi la Polisi nchini. Benedict Wakulyamba, alisema Mkuu wa Jeshi hilo, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, amesikitishwa na vifo vya askari hao na kwamba hilo ni pigo kubwa kwa jeshi.

Wakuyamba aliyemwakilisha IGP Wambura alisema kuondoka kwa askari mmoja pekee ndani ya jeshi hilo, ni pengo kubwa hasa ikizingatiwa jukumu kubwa la ulinzi wa raia na mali zao ambalo linapaswa kusimamiwa na askari mmoja.

Kwa mantiki hiyo, alisema pengo lililoko la kuondoka kwa askari hao wawili ni kubwa zaidi, hivyo kuomba wanandugu kuendelea kuwa na utulivu katika kipindi hiki kigumu ya maombolezo.

"Tunatambua vifo vyao ni mipango ya Mungu ambayo kila mwanadamu ataipitia pamoja na kuwa wameondoka kipindi ambacho taifa linawategemea pamoja na familia zao," alisema.

Awali, akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi (ACP) Allan Bukumbi, alisema askari hao walianza safari yao kutoka Arusha ambako ni kituo chao cha kazi kwenda Makongorosi, Chunya mkoani Mbeya.

Bukumbi alisema wanandoa hao waliofariki dunia katika ajali hiyo walikuwa watatu pamoja na abiria mwingine, Enock Mbata (35), mkazi wa Iringa ambaye mwili wake ulizikwa juzi mkoani hapa.

Kamanda Bukumbi alisema ajali hiyo ilitokea majira ya saa 3.05 asubuhi katika eneo la Tanangozi Wilaya ya Iringa, barabara kuu ya Iringa - Mbeya baada ya gari walilokuwamo aina ya Totoya Vits kupanda kwa kasi tuta kutaka kulipita lori lililokuwa mbele kabla ya kugongana uso kwa uso na basi la kampuni ya Luwinzo.

Baba Mdogo wa marehemu Agnes, Beatus Mbembe, alisema binti yake ndio alikuwa katika maisha ya mwanzo ya ndoa yao kwa kuwa alibariki ndoa Desemba 17, mwaka huu.

Mbembe alisema Agnes alizaliwa Septemba 17, 1995 na mume wake alizaliwa Desemba 2, 1992 na kwamba vifo vyao ni fumbo kubwa.

Alisema Agnes ni mtoto wake wa kufikia kwa kuwa baada ya baba yake kufariki dunia ndipo alipomuoa mama yake ambaye mwaka jana alipata ajali iliyosababisha miguu yake kuvunjika.

Kwa mujibu wa Mbembe, wakati wote Agnes alikuwa msaada mkubwa katika familia kwa kumuuguza mama yake, hivyo kifo chake ni pigo kubwa kwa familia.

# Ummy aunda tume kuchunguza ubadhirifu ujenzi wa hospitali

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameunda timu itakayoongozwa na Jaji Mstaafu Thomas Mihayo, kuchunguza ubadhirifu katika mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Ukerewe mkoani Mwanza.

Aliunda tume hiyo juzi alipotembelea mradi huo wilayani Ukerewe wakati wa ziara yake kwa ajili ya kukagua na kuchunguza mwenendo wa ujenzi wa mradi huo.

Waziri Ummy alifanya ziara hiyo baada ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kutembelea wilayani humo Novemba 25, mwaka huu, na kumtaka afike kukagua mwenendo wa ujenzi huo.

Akizungumzia mradi huo, Ummy alisema wamepokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu kitoridhishwa na gharama za ujenzi na kusisitiza kuwa hawajamshawishi na ujenzi huo kwa kuwa lengo ni wananchi wa eneo hilo kupata huduma za kibingwa na Hospitali ya Sekou Toure au Bugando.

Waziri alisema shida imeanzia kwenye ujenzi wa majengo hali ambayo itasababisha kukosa madaktari bingwa baada ya kumalizika.

"Niwakumbushe kuwa alichotaka Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa) tangia mwanzo ni kwamba wananchi wa Ukerewe wasisafiri tena kwenda mbali ndiyo maana tukaamua kujenga hospitali ya rufaa ya mkoa. Lakini mmeanza vibaya kama hili jengo la kliniki ya mama na mtoto ni la nini hapa wakati hata kwenye hospitali zingine tunaziondoa, hivyo bado hamjanishawishi kuwa baada ya ujenzi huu wana Ukerewe watapata huduma za kibingwa hapa," alisema Waziri Ummy.

Alisema marekebisho lazima yafanyike ili kupata huduma za kibingwa na kwamba wakiendelea hivyo hawatatua tatizo kwa kuwa huduma zinazotolewa hapo bado zipo kwenye hospitali ya wilaya.

"Kwa macho yangu siyo kama mtaalamu, binafsi nilipoona majengo haya hayaendani na gharama iliyowekezwa. Nimekuwa Waziri wa Afya kwa miaka sita, tumejenga vituo vya afya vya Sh. milioni 400 majengo saba. Naunda timu yangu ya tatu ambayo itakuwa na watu watano itanipa taarifa ya mwisho ikiongozwa na Jaji mstaafu Thomas Mihayo ." alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alisema kumekuwa na makosa tangu hatua za awali katika utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa alisema walichokifanya kwa hapo walikaa na timu ya wizara wakajaribu kuangalia kulingana na hali ilivyo na idadi ya watu walichokilenga ni huduma zote za kibingwa ziwapo, wakaangalia hospitali hiyo isiwe kubwa na waliangalia baadhi ya michoro ili iendane na huduma zote.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Dk. Getera Nyangi, alisema mwaka jana walikaa kikao kupanga namna ya kutekeleza mradi na walipendekeza kujengewa majengo ya ghorofa, lakini walipoambiwa kuwa haiwezekani kutokana na ufinyu wa rasilimali fedha, waliamua wajenge majengo 11 ya chini.

## Waziri ataka uhamasishaji umiliki ardhi

**Na Munir Shemweta**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amewataka makamishna wasaidizi wa ardhi nchini kuhamasisha wananchi ili wajue umuhimu wa kuchukua hatimiliki za ardhi.

Ridhiwani alitoa agizo hilo jana mkoani Dar es Salaam wakati akifungua mkutano baina ya ofisi ya kamishna msaidizi wa ardhi wa mkoa na kampuni zinazofanya kazi katika miradi ya urasimishaji makazi holela kwa lengo la kutatua changamoto za urasimishaji katika mkoa huo.

"Kama ninyi mtaona kazi yenu inaishia katika kufanya usajili wa michoro ya mipango miji na kuwawekea mawe wananchi mkaamini mmemaliza kazi, hii haitoshi. Mnachotakiwa ni kuwa na kazi ya kufanya ya kuhamasisha wananchi kuchukua hati," alisema.

Ridhiwani alielezea tofauti kubwa kati ya idadi ya viwanja vilivyopandwa mawe katika mkoa wa Dar es Salaam na vile vilivyotolewa hati kwamba hali hiyo kuwa hesabu zake zinakataa kabisa.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, idadi ya viwanja vilivyopandwa mawe katika mkoa wa Dar es Salaam ni 238,800 na viwanja vilivyopimwa na kuidhinishwa ni 106,000 huku vilivyotolewa hati ni 24,000 jambo ambalo halileti afya katika sekta ya ardhi.

"Kama tunaweza kuwa na viwanja 238,800 vinavyotakiwa kulipiwa huku viwanja 24,000 pekee vikilipiwa basi hapo kuna tatizo na hapa ni nani wa kuwaambia wananchi umuhimu wa kuwa na hatimiliki ya ardhi? Kama viongozi tunaweza kusema kupitia vyombo vya habari lakini wanaotazama ni wangapi?" Alihoji.

Alimtaka Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam, wataalamu wa sekta ya ardhi kwa kushirikiana na mameya na viongozi wa mkoa kuwa na kazi ya kufanya katika eneo hilo ili wananchi waweze kujua umuhimu wa kuchukua hati.

Pia alisema kamati za urasimishaji makazi holela kwa kushirikiana na viongozi wa halmashauri na manispaa za mkoa kusaidia kuwa sehemu ya uhamasishaji watu kwenda kuchukua hati.

Ridhiwani alisema kamati za urasimishaji zisiishie katika masuala ya kupanga miji ziende mbali hata baada ya miamala ya malipo inapokuwa imetoka basi wawe sehemu ya kuhamaisha watu waende kulipia ili wapate hati.



Mchuuzi wa kuni akijiandaa kuvuka barabara kwenda kusaka wateja mjini Korogwe jana. Hata hivyo, utumiaji wa nishati hiyo huchangia uharibifu wa mazingira. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wamiliki simu waagizwa kuhakiki namba kwa vitambulisho vya NIDA

**Na Mwandishi Wetu**

WATUMIAJI wa huduma za mawasiliano ya simu nchini wanapaswa kukamilisha uhakiki wa namba zao za simu zinazotumika kwa kutumia kitambulisho cha uraia ifikapo Januari 31, mwakani.

Lengo la uhakiki ni kuhakikisha watumiaji wa huduma za mawasiliano ya simu wanasalia kuwa salama muda wote wanapotumia huduma hizo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari, alisisitiza kuwa kila mtumiaji wa huduma za mawasiliano anapaswa kuhakiki namba zake zinazotumika kwa kutumia kitambulisho cha uraia.

"Hili ni zoezi muhimu linalolenga kuhakikisha tunapunguza watumiaji huduma za mawasiliano ya simu wasiosajiliwa kwa utambulisho wao binafsi. Baadhi wamekuwa wakitumia mwanya wa kutotambuliwa kwa usajili wao kufanya mambo yasiyotakiwa kwenye ikolojia ya Mawasiliano," alisisitiza Dk. Jabiri.

"Katika kufanya hivyo, mtumiaji anatakiwa kubofya namba *106# katika simu yake na utaweza kuhakiki usajili wa namba yake pamoja na kutazama idadi ya namba za simu zilizosajiliwa kwa namba yake ya kitambulisho cha taifa kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

"Baada ya kupiga namba *106# utapewa chaguzi kadhaa namba 1 hadi 5, ukichagua namba 3 utaweza kutazama idadi ya namba za simu zilizosajiliwa kwa namba yako ya Uraia iliyotolewa na NIDA. Mtumiaji wa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi akibaini namba za ziada, zaidi ya zilizosajiliwa kwa namba yake ya NIDA, atatakiwa kuchukua hatua," alisema. Dk. Jabir alisema uhakiki wa namba za simu kwa kutumia kitambulisho cha uraia una madhumuni ya kumlinda mtumiaji dhidi ya vitendo visivyofaa vinavyofanywa na watumiaji wengine mfano kutuma ujumbe wa vitisho, matusi na matendo ya kihalifu.

"Kila mmoja wetu akitekeleza kwa ukamilifu zoezi hili tutafanikiwa kuweka anga la Mtandao wa Mawasiliano, hasa Mawasiliano ya simu kuwa salama zaidi kwa kila mmoja wetu," alisisitiza.

Mamlaka hiyo imebainisha kuwa baadhi ya watumiaji huduma za mtandao wa simu wamekuwa wakikwepa kusajili laini za simu kwa sababu mbalimbali, ikiwemo kukwepa kubainishwa kwa matendo ya jinai wanayotenda kwenye mtandao hivyo hutumia mbinu ya kununua laini za simu zilizosajiliwa tayari kwa utambulisho wa watumiaji wengine wa huduma za Mawasiliano. Novemba, mwaka huu, TCRA ilitangaza kuzifungia jumla ya namba tambulishi 52,087, zikiwemo zile zinazohusishwa na wizi, utapeli na ulaghai kupitia mitandao ya simu; ambapo imesisitiza kampeni ya uhakiki wa laini za simu inayofanyika kipindi hiki inafanywa kwa ushirikiano na Watoa Huduma wote wa mitandao ya simu.

TCRA ilisisitiza kuwa itakapowadia Januari 31 mwakani namba za simu ambazo hazitakuwa zimehakikiwa zitazuiliwa kupokea na kutoa huduma za Mawasiliano.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tunawatakia maandalizi mema Sikukuu Krismasi, Mwaka Mpya

**ZIMEBAKI** siku mbili Wakristo washerehekee sikukuu ya kumbukumbu ya kuzaliwa mwokozi wao Yesu Kristo na pia ukisubiriwa kuagwa mwaka 2022 na kuukaribisha mwaka 2023.

Kipindi hiki cha sikukuu za mwishoni mwa mwaka ndicho wafanyabiashara hukitumia kufanya biashara kwa wingi na wengine hukitumia kupandisha bidhaa za vyakula na nguo wakijua kwa vyovyote lazima watu wanunue.

Shamra shamra za manunuzi zimepamba moto hasa kwenye maduka ya Kariakoo ambako ndio maarufu kwa maduka yanayouza bidhaa mbalimbali kwa bei nafuu.

Wafanyabiashara wengi hasa wenye maduka ya rejareja ya vyakula na yanayouza nguo, hupendelea kwenda kununua vitu vya jumla Kariakoo ambavyo huvipata kwa bei nafuu na kwenda kuuza kwenye maduka yao kuwarahisishia wale wasioweza vurugu za Kariakoo.

Huu pia ni muda ambao vibaka wanautumia kuwavizia watu wanaokwenda kununua bidhaa ili kuwapora, hivyo wanaokwenda huko ni lazima wazingaite umakini kwa kukumbatia vipochi vyao na simu za mkononi.

Familia nyingi hupendelea pia kwenda kufanya ununuzi kwenye maduka ya Kariakoo kwa kufuata unafuu na vile vile hupata fursa ya kuchagua vitu wanavyovipenda badala ya kutegemea kuletewa na wauza maduka ambavyo pengine sio chaguo lao.

Kipindi hiki basi kitumike vizuri, kisiwe cha kukomoana kwa kupandishiana bei kwa sababu wanunuzi na wafanyabiashara wanategemeana.

Kama wanunuzi watagoma kununua bidhaa kwa sababu ya bei kubwa maana yake wafanyabiashara watadoda na bidhaa zao.

Vile vile, kwenye bidhaa za vyakula, hiki kipindi lazima watu wafurahi na familia zao kwa kukaa pamoja, kula, kucheza na kufurahi.

Baadhi ya familia hukutana angalau mara moja kwa mwaka na kutambuana kwa sababu mwaka mmoja bila kuonana kuna mengi yanatokea. Watoto wapya wamezaliwa, wengine wameoa na kuolewa hivyo kuna umuhimu wa kujuana.

Wengine hukutana kwa kufanya tathmini ya kile walichokifanya kwa mwaka mzima na kama hajafikia malengo ni wapi amekwama ili ndugu waweze kumsaidia kusonga mbele.

Baadhi ya makabila wanatabia hiyo ya kukutana na kila mmoja katika familia hiyo hueleza mafanikio yake na kama hajafikia malengo yake wapi ameshindwa kufikia ili aweze kusaidiwa.

Tunapouaga mwaka 2022 ni lazima tujiulize tumefanya nini kusaidia wenzetu wasiokuwa na uwezo ili nao waweze kufanikiwa na wao waweze kusaidia wengine.

Lakini kwenye familia kuna watu ambao hata wakisaidiwa, hawaonyeshi shukrani na hawatosheki, matokeo yake ni kumjaza lawana anayesaidiwa kiasi cha kumvunja moyo.

Kama kuna watu wenye tabia hiyo, basi waiche na kuingia mwaka 2023 kwa mambo mapya yenye kuleta mabadiliko.

Mtu asiyekuwa na shukrani hata siku moja hawezi kubarikiwa na kila siku atakuwa mtu wa kulalamika na manung'uniko. Akiona mwenzake amefanikiwa anaumia na kujiuliza kwa nini isingekuwa yeye bila kujua kuwa malalamiko yake ndiyo yanayomfanya akwame.

Siku zote mtu anapofanya mema kwa mwenzake, hubarikiwa na kuzidishiwa kile kidogo alichotoa kikarudishwa maradufu.

Kila mmoja ajitathmini kwa kile alichokifanya 2022 na mwaka 2023 unapoingia ajirekebishe pale alipokosea na kama amefanikiwa awasaidie wenzake nao watoboe.

Kila la heri wakati tukisubiri kuumaliza mwaka 2022.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

## Nyie wa zama za 1990, mngeshuhudia mabehewa enzi zetu, mngebaki kimya!

**WAKATI** wa hafla ya kutia saini mkataba wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) Awamu ya Pili, Rais Samia Suluhu Hassan, pamoja na mambo mengine aliwashangaa wanaohoji ubora wa mabehewa hayo, akisema baadhi yao hawajui nchi ilipotoka.

Katika hafla hiyo iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam, Rais Samia alisema aliwahi kusafiri na treni na alipanda daraja la kwanza, ambalo hadhi yake hailingani na daraja la tatu la mabehewa hayo mapya.

Akasema wanaobeza wanapaswa kujua kuwa taifa limetoka mbali na lazima washukuru hatua iliyofikiwa sasa.

Kwenye utiaji huo wa saini mkataba huo awamu ya pili, kipande cha kutoka Tabora hadi Kigoma, Rais alisema mabehewa yaliyoonyeshwa kwenye video iliyochezwa Ikulu juzi ni ya kisasa na yamekarabatiwa vizuri tu.

Binafsi maneno ya Rais Samia yalinikumbusha miaka ya nyuma kabisa. Naweza kusema kuwa vijana waliozaliwa miaka ya 1990 na kuendelea, ambao wamekuwa wakiangalia picha nyingi za video kutoka nje ya nchi kutokana na maendeleo ya teknolojia, kama miaka ya nyuma kungekuwa na hizo video ambazo zingekuwa zinachukuliwa na kuhifadhiwa, wakaona jinsi gani mabehewa ya zamani au usafiri ulivyokuwa, wangelia.

Lakini, kwa wakati ule ilionekana kawaida kwa sababu ilikuwa hakuna sehemu ya kufananisha. Ilionekana kawaida tu. Kusema kweli kama alivyotamka Rais Samia hali ilikuwa ni ya kusikitisha.

Ninavyoona wanavyobeza mabehewa haya ya sasa unashangaa, lakini unawasamehe tu kwa sababu hawajui wanachokisema. Hawajawahi kuona abiria wanasafiri baadhi ya mabehewa yalikuwa na madirisha ambayo hayafungi. Mikoani kuna baridi, na porini kuna vitu vingi.

Kulikuwa na mabehewa ambayo hata nyuki wakitimka kwenye mizinga hayo hakuna sehemu yoyote ya kufunga ili wasiingie. Abiria walisafiri kwa kudra za Mwenyezi Mungu tu.

Wapo ambao walizaliwa miaka ya 1990 kurudi nyuma, lakini wanabeza tu kwa sababu zao binafsi, labda za kisiasa au zinazofanana na hizo, lakini baada ya kuwalisha watu uongo wanapokaa peke yao wakikumbuka, wanatambua kuwa kweli watu tumetoka mbali.

Tuliobahatika angalau kidogo kuona na hali ilivyo sasa, tunashukuru Mungu pamoja na serikali kuwa maendeleo yamefanyika na Tanzania taratibu inajiondoa kutoka ilipo na kwenda sehemu nyingine.

Rais Samia akasimulia yeye alipanda treni kwenye behewa la daraja la kwanza ambalo hadhi yake hailingani kabisa na mabehewa ya sasa ya daraja la tatu. Hapo nami namuunga mkono, ni kweli kabisa!

Yaani haya mabehewa ya sasa ambayo yanabezwa, ni mazuri na hadhi yake hailingani kabisa na yale ya daraja la kwanza la wakati huo.

Niwakumbushe tu kuwa zamani picha linaanza kwanza kwenye kukata tiketi. Iwe ya kwenda popote pale. Mfano kutoka Dar es Salaam kwenda Tabora, Kigoma, Mwanza au Mpanda.

Mpaka tiketi ipatikane abiria keshasota wiki mbili. Ukiingia kwenye mabehewa ya daraja la tatu unakutana na siti ambazo hazina sponji, feni na hata baadhi ya madirisha hayafungiki.

Ukikuta juu kuna feni hilo litakuwa limeharibika. Sijajua kama yaliyokuwa yakiharibika ndiyo yanahamishiwa daraja tatu au vipi, lakini msamiati wa feni tu huko haukuwepo.

Tofauti kubwa ya wakati ule wa daraja la kwanza, la pili na la tatu, ulikuwa ni idadi tu ya watu. Kwanza, kulikuwa na watu wachache ambao walikuwa wana uhuru wa kukaa bila ya bughudha na wana utaratibu wa kulala, la pili kulikuwa na watu wengi kidogo, wastani kama sita, lakini angalau wakikaa kwa utulivu.

Shughuli ilikuwa huko daraja la tatu, ambako ilifanana na jina palipobatizwa ambalo jina lenye ukakasi kidogo hata kulitamka. Kwanza, kulikuwa na mabehewa machache, hivyo abiria walikuwa wengi kiasi kwamba wengine siti hazikutosha, wakakalia mizigo yao, wengine chini ya sakafu, wapo waliokaa kwenye maungio ya mabehewa, jirani na chooni.

Huko ni kukaa tu, hakuna kuinukainuka kwenda sehemu nyingine kwa sababu utawakanyaga wenzako. Kutokana na 'nyomi' la watu, wizi ulikuwa mkubwa, watu kuibiana mizigo, pia ilikuwa ngumu watu wakijishauri kwenda chooni, hasa kinamama.

Kusema kweli hadhi ya mabehewa na mazingira yalikuwa magumu na ya kusikitisha. Siku hizi mabehewa yana feni, mpaka sehemu ya kuchaji simu, redio, na vitu vingine. Hapo ndipo kinanijia kiulizo, anayeponda haya anajua? Tuwasamehe bure, hawajui walitendalo na wanachokisema.

## HABARI KITAIFA

## Asakwa kwa madai ya kumuua mkewe

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linamsaka mtu mmoja aliyefahamika kwa jina la Abdallah ambaye alikuwa mume wa Pili Mang'ota, kwa madai ya kuhusika na mauaji ya mke wake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna msaidizi (ACP) Pius Lutumo, alisema mwili wa Pili uliokotwa Desemba 19, mwaka huu, Sanze wilayani Kisarawe ukiwa umeharibika.

Abdallah anadaiwa kumuua Pili ambaye alikuwa mfanyabiashara wa mboga ambaye aliaga kuwa anakwenda kuchuma mboga mashambani Visegese Desemba 15, mwaka huu, na hakuonekana hadi mwili wake ulipoonekana ukiwa umefukiwa huku umeharibika.

Mtuhumiwa anadaiwa kufanya mauaji hayo kutokana na wivu wa mapenzi baada ya mke wake kumtamkia kuwa mtoto wanayemlea pamoja si wake.

Katika tukio lingine lililotokea Desemba 19, Sungwi kata ya Masaki, wilaya ya Kisarawe, Lasmini Kondo (15), mwanafunzi wa kidato cha kwanza Shule ya Sekondari masaki, alikutwa akiwa amekufa kwa kujinyonga.

Inadaiwa mwanafunzi huyo alijinyonga kwa kutumia mtandio baada ya kuonywa na wazazi wake kuacha kujihusisha na mapenzi.

Kamanda Lutumo alisema Kondo alikutwa na barua aliyoandika kwenda kwa kijana aliyemtaja kwa jina moja la Simon akimtaarifu kuachana naye kimapenzi kutokana na kushindwa kuvumilia tabia zake.

Baada ya kuonywa na wazazi, inadaiwa aliondoka kwa hasira na hakurudi tena hadi mwili wake ulipoonekana akiwa amefariki dunia kwa kujinyonga.

**Inadaiwa mwanafunzi huyo alijinyonga kwa kutumia mtandio baada ya kuonywa na wazazi wake kuacha kujihusisha na mapenzi.**



Mwonekano wa Barabara ya Morogoro eneo la Mbezi Luis baada ya kuwekewa uzio pembeni, ili waenda kwa miguu wapite juu ya daraja. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Abiria wapewa rungu kudhibiti ajali

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KIKOSI cha Usalama Barabarani nchini, kimewapa 'rungu' abiria kutoa taarifa kwenye mamlaka ili kudhibiti madereva wanaokwenda mwendokasi na wale wanaoyapita magari sehemu zisizoruhusiwa.

Hatua hiyo ni sehemu ya kampeni maalum kudhibiti ajali katika kipindi cha msimu wa siku kuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Kampeini hiyo yenye kaulimbiu 'Safiri Salama Mwishoni mwa Mwaka Abiria Paza Sauti Dereva Anapokosea', iliendelea jana jijini Mwanza chini ya usimamizi wa Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ramadhani Ng'anzi, kwa kutoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva, mawakala na abiria katika vituo vya mabasi yaendayo mikoani na nje ya nchi.

Pia kampeini hiyo iliambatana na upimaji wa matumizi ya vileo kwa madereva wa mabasi katika vituo vya mabasi vya Nyegezi na Nyamohongolo mkoani hapo ili kudhibiti ajali zinazoendelea kutokea nchini hasa zinazosababishwa na baadhi ya madereva kutumia vileo wakati na kabla ya safari.

Akizungumza na abiria, mawakala, madereva na wamiliki wa mabasi, SACP Ng'anzi aliwataka madereva kuendesha kwa ustaarabu ikiwa ni pamoja na kufuata sheria na alama za barabarani pamoja na kuacha kuendesha vyombo hivyo kwa mwendokasi.

Ng'anzi aliwataka abiria kuhakikisha wanatoa taarifa pindi dereva anapovunja sheria ikiwa ni pamoja na kwenda mwendokasi barabarani na kuchepuka katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Katika hatua nyingine, Kamanda Ng'anzi alikemea vitendo vya baadhi ya wamiliki wa mabasi kusubiri kipindi cha sikukuu na kuanza kurejesha magari yenye matatizo barabarani, hivyo kusababisha ajali kwa kukata breki na kuzima ghafla.

"Tunataka abiria wasafiri salama na kufika bila kupatwa na matatizo yayote. Pia kila wakala wa basi akate tiketi kwa njia ya kelektroniki ili kuepusha wizi na utapeli usababishwao na baadhi ya mawakala vishoka," alisema Ng'anzi.

Wakizungumza wakati wa kampeni hiyo, baadhi ya madereva na viongozi wa stendi, aliahidi kufuata sheria na taratibu ili kudhibiti ajali za barabarani.

"Tutahakikisha tiketi zote zinakatwa kwa njia ya kielektroniki kuepusha usumbufu kwa wateja wetu ikiwa ni pamoja na kuhimiza madereva wetu kuhakikisha wanaendesha magari kwa kufuata sheria na alama za barabarani," alisema Thomas Njau, Mwenyekiti wa Stendi ya Nyegezi.

Nao baadhi ya abiria wameiomba serikali kuendelea na kampeni hiyo ili kuhakikisha wanadhibiti ajali za barabarani.

"Tutahakikisha tunatoa taarifa juu ya uvunjifu wa sheria pamoja na kuendesha mwendo kasi kupitia namba ya dharura pamoja na namba ya mkuu wa kikosi cha usalama barabarani nchini," alisema mmoja wa abiria hao, Eveline Allan.

## KABWELA

Fadhili Mohamed



# Kanisa laanzisha programu kuelimisha vijana, watoto

**Na Elizabeth Zaya**

KANISA Katoliki Dekania ya Mtakatifu Gasper na Mtakatifu Thomas More limeanzisha programu maalumu ya kuendesha makongamano ya kuwaelimisha vijana na watoto, kukabiliana na vitendo vya ukatili ambavyo vimeshamiri kwa sasa nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari katika kongamano la kuwaelimisha vijana hao waliokuwa kati ya 10 hadi 21, lililofanyika katika Kanisa Katoliki Bunju A, kiongozi mmojawapo kati ya dekania hizo mbili, Padri Dominic Somola, alisema wameamua kuanzisha programu inayolenga kujenga msingi na uelewa wa kunusuru kundi hilo na vitendo vya ukatili na unyanyasaji vinavyoendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kwa kushirikiana na Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA), tulinuia kufanya hili kusanyiko kubwa la watoto wenye umri kati ya miaka 10 mpaka 21, tukijikita katika mada za kuwasaidia kujitambua. Tunafahamu kwamba kwa sasa wazazi wanapitia changamoto kubwa ya malezi, ulimwengu umebadilika kwa kasi sana, kwa hiyo tumetumia nafasi hii kuwaweka pamoja, si Wakristo tu Wakatoliki, pia kuna watoto wanaotoka katika madhehebu mengine,"alisema Padre Somola.

"Kwa sababu suala la malezi na maadili linamgusa kila mtoto na kila familia na tatizo sasa hivi halichagui ni nyumba ya nani, kanisa lipi au imani ipi, kwa hiyo tunaamini kupitia makongamano haya yatasaidia kujenga msingi wa kizazi chenye maadili mazuri na tunaamini katika kipindi hiki cha likizo ni muafaka kwao na hili jambo litakuwa endelevu."

Mambo mengine ambayo alisema wameanza kuwafundisha watoto na vijana hao ni matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii.

"Kwa hiyo hii ni kampeni ambayo tumeanza na tuna mpango wa kufanya hivyo na kwa wazazi kwa sababu ni sehemu ya familia, lengo ni kuliandalia taifa kizazi cha raia wenye afya, maadili, kizazi cha watu wanaojitambua. Karibu kila nyumba inalia katika malezi ya watoto shuleni, nyumbani na hata katika jamii, matukio mbalimbali ya ukatili katika kundi hili yanaendelea kuripotiwa, kwa hiyo lengo hasa ni kujenga uelewa na uwezo wa kujiamini kwa kundi hilo la watoto namna ya kupambana na vitendo hivyo,"alisema Padri Somola.

"Tunataka watoto watambue namna ya kukataa jambo wanaloona haliko sahihi kwao, wawe na uwezo wa kukimbia, kusema, na hata kupiga kelele wanapoona viashiria vya kufanyiwa ukatili. Na ni sehemu ya kulipigia kelele suala hili na hatuwezi kukaa kimya kuona vitendo hivi vinaendelea, kila mmoja kwa nafasi yake achukue hatua." Alisema ni vema kila kanisa, kila imani, taasisi, walimu, walezi, na serikali kuungana kwa pamoja kupambana na vitendo hivyo vya ukatili kwa watoto ili kulisaidia kundi hilo kuwa salama, kuwa na misingi imara.

Mwenyekiti wa Wawata Dekania ya Mtakatifu Gaspar, Dorothy Malela, alisema kama kikundi cha kina mama katika kanisa hilo la Katoliki, wameguswa na tatizo la ukatili kwa kundi hilo na kuamua kushiriki kuanzisha programu hiyo kuwafundisha watoto stadi za maisha na namna ya kupambana na vitendo viovu vinavyozidi kuripotiwa kila mahali nchini.

"Hali kwa kweli siyo nzuri, tunapata taarifa mbalimbali, unyanyasaji wa watoto unaendelea kuongezeka siku hadi siku, kwa hiyo sisi Wawata kutoka Dekania za Mtakatifu Gaspar na Mtakatifu Thomas More, tukaonelea kwamba ni vema kuanzisha semina kama hizi za kujitambua kwa watoto wetu na tunataka iwe endelevu," alisema Dorothy.

Alisema zaidi ya watoto 3,000 walishiriki katika kongamano hilo kutoka maeneo tofauti katika mkoa wa Dar es Salaam.



Baadhi ya wafanyabiashara wa kuku wa kienyeji Manispaa ya Singida, wakipakia kuku kwenye fuso kuwasafirisha jijini Dar-es-Salaam kwa ajili ya sikukuu ya Krismasi. **PICHA: NATHANIEL LIMU**

## Maofisa tarafa wapewa mbinu za utendaji

**Na Veronica Mwafisi,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Xavier Daudi, amewataka maofisa tarafa 48 waliohudhuria mafunzo ya kujengewa uwezo kiutendaji, kuutumia vizuri muda wa kazi katika kuwahudumia wananchi.

Daudi alitoa wito huo kwa maofisa tarafa hao jana jijini Dodoma, wakati akifunga mafunzo yaliyoandaliwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili waendane na kasi ya utendaji kazi ya serikali.

Aliwataka kutotumia muda wa kazi katika mitandao ya kijamii wakati wana jukumu la msingi la kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa wananchi katika maeneo yao ya kazi.

Daudi aliongeza kuwa ofisi yake imeshirikiana na TAMISEMI kuandaa mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji kwa kutambua kuwa maofisa hao ni kiungo muhimu kati ya serikali kuu, serikali za mitaa na wananchi ambao ndio walengwa wakuu wa huduma zinazotolewa na taasisi za umma.

"Ninyi ni kiungo kikubwa cha kuiwezesha serikali kutoa huduma bora kwa wananchi, hivyo ukisikia serikali inalaumiwa kwa kutotoa huduma bora kwa wananchi au kupongezwa kwa kutoa huduma bora, ninyi maofisa tarafa mnahusika ndiyo maana tumeamua kuwapatia mafunzo ili mkatekeleze majukumu yenu kikamilifu," alisema.

Naye Kaimu Mkurugenzi, Idara ya Uendelezaji Rasilimali Watu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Edith Rwiza, alisema mafunzo kwa maofisa tarafa hao yametolewa kwa siku mbili yakilenga kuwajengea uwezo ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kutoa huduma bora na endelevu kwa wananchi.

# Halmashauri yanufaika na mradi mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

MRADI wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kupitia Mifumo Ikolojia (EBARR) unaotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, umewezesha kufanyika upimaji wa mipaka ya vijiji sita, utayarishaji wa ramani na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji vinne vya Halmashauri ya Simanjiro mkoani Manyara.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Christina Marwa, alibainisha hayo jana wakati kikao kazi kilipowasilisha Taarifa za Upangaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwenye vijiji hivyo vya Irkujit, Endonyongijape, Langa na Narosoito.

Aliwataka wajumbe wa menejimenti ya halmashauri na wataalamu wa wilaya hiyo kufuatilia kwa makini taarifa za Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwenye vijiji hivyo.

Christina amebainisha kuwa taarifa hiyo itasaidia katika uainishaji na utengaji wa maeneo unaozingatia mipango ya matumizi ya ardhi ya halmashauri na kuweka katika vipaumbele vyao ikiwamo kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi ya mabwawa, huduma za jamii, hifadhi ya misitu, mashamba, makazi, malisho na maeneo ya makaburi.

"Umuhimu wa kupata mrejesho wa taarifa hiyo umesaidia halmashauri katika kupima mipaka ya ardhi ya kijiji, utatuzi wa migogoro ya mipaka, utoaji wa vyeti vya ardhi ya vijiji, uandaaji wa ramani za msingi ya matumizi ya ardhi ya vijiji na uandaaji wa sheria ndogo za usimamizi wa matumizi bora ya ardhi, masjala ya wazi ya vijiji, utoaji, usajili na usimamizi wa hatimiliki za kimila pamoja na utatuzi wa migogoro ya miliki," alifafanua.

Akiwasilisha taarifa hiyo, Meneja Kanda ya Kati Dodoma wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Suzana Mapunda, alisema malengo makuu ya kazi hiyo ni kuongeza uthabiti wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi, kutambua uharibifu wa huduma za mfumo ikolojia na kutenga maeneo ya matumizi ya ardhi.

Alisema utaratibu mzima uliotumika katika uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi wa vijiji, ulizingatia hatua sita kulingana na mwongozo wa matumizi ya ardhi ya kijiji unaozingatia utekelezaji wa sera.

"Wilaya ya Simanjiro inakabiliwa na migogoro mingi ya mipaka ya vijiji kutokana na vijiji hivyo kutokupimwa na hivyo kusababisha kuwapo baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika kuandaa ramani ya mpango wa matumizi ya ardhi," alisema.

Alitaja migogoro mingine ni kutokupimwa kwa mipaka ya vijiji, ukosefu wa vyeti vya ardhi, mzozo mkubwa wakati wa upangaji mipaka ya vitongoji, wanakijiji na halmashauri ya kijiji kupokea wageni na kuwauzia maeneo makubwa.

Meneja huyo alisema kazi zitakazoendelea kufanyika ni kuandaa na kutoa vyeti vya ardhi ya vijiji, kuandaa mipango kwenye vijiji vya nyanda za malisho, kutoa Hati Miliki za Kimila (CCRO) na kuendeleza maeneo yaliyotengwa.

# Waziri ashangazwa wananchi kushindwa kuchangamkia fursa urasimishaji ardhi

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameonyesha kutoridhishwa na kasi ya wananchi wa Wilaya ya Ubungo mkoani Dar es Salaam kutochangamkia fursa ya kupatiwa hati kupitia urasimishaji makazi holela.

Alionyesha hali hiyo juzi wakati wa utoaji hatimiliki za ardhi kwa wananchi 1,081 wa maeneo tofauti wilayani Ubungo waliokamilisha taratibu za kumilikishwa ardhi kupitia urasimishaji makazi holela eneo la Stop Over, Kata ya Saranga.

Huku akieleza kupitia takwimu za urasimishaji katika wilaya ya Ubungo, Dk. Mabula alisema kazi kubwa imefanywa na ofisi ya ardhi katika halmashauri hiyo na hatimiliki 1,081 zimekamilishwa na kugawiwa kati ya viwanja 23,967 vilivyopimwa na kuidhinishwa.

"Wote waliotimiza wajibu wao hakuna hati inayodaiwa hapa. Wako waliotimiza wajibu na hawaendi kuchukua. Sasa unataka serikali ifanye nini?" Alihoji.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, changamoto ya urasimishaji makazi holela iko pande zote mbili za wananchi na kampuni zinazofanya kazi za urasimishaji na kusema haiwezekani hati 1,081 pekee ndizo zikamilishwe na kugawiwa wananchi kati ya viwanja 23, 967 vilivyoidhinishwa.

"Haiwezekani Ubungo idadi ya vipande vya ardhi vilivyotambuliwa ni 182,215 kutoka michoro 520. Idadi ya viwanja vilivyopangwa na kuidhinishwa ni 177,325. Idadi ya viwanja vilivyowekewa mawe 76,250.

"Vilivyopimwa na kuidhinishwa ni 23,967. Ankara zilizotoka 4,338, idadi ya maombi ya hati 7164, idadi ya hati zilizotolewa 6,885 na leo kuna hati 1,081 ukijumlisha hapo maana yake hakuna hati inayodaiwa katika ofisi ya ardhi," alisema Dk. Mabula.

Alisema kwa wale wote waliotimiza wajibu wao hakuna hati inayodaiwa mpaka wanagawa hati wilayani Ubungo lakini wako wale waliotimiza wajibu wa kulipa na kuandaliwa hati lakini hawaendi kuchukua na kuhoji hapo serikali ifanye nini na kuainisha kuwa ilichoamua wizara yake ni kuwafuata walipo kwa lengo ni kuhakikisha hakuna wanachodai ndani ya wizara.

Mbunge wa Kibamba, Issa Mtemvu, pamoja na kuelezea kuendelea vizuri kwa urasimishaji makazi holela kwa baadhi ya kata za jimbo lake na kuzitaja Saranga, Ukombozi na Mpakani, baadhi ya wananchi wanakabiliwa na changamoto za malipo ya kukamilisha ili kupatiwa hati na kuiomba wizara kuangalia namna ya kuwasaidia ili wapatiwe hati.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Lidovick Nduhiye, akizungumza katika uzinduzi wa mafunzo kwa watumishi wa Chuo cha Bandari Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Adha maji Madale, Mivumoni kwisha karibuni

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameagiza Mfuko wa Maji wa Taifa (NWF) kutoa Sh. milioni 500 kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa ajili ya kuwaunganishia maji baadhi ya wakazi wa Madale, Mivumoni, Goba, Wazo na Tegeta A ambao hawajafikiwa na mradi wa Makongo hadi Bagamoyo.

Aweso alitoa kauli hiyo jana wakati wa ziara ya kukagua mradi huo utakaohudumia wakazi 450,000 pamoja na mradi wa Mshikamano ambao unatarajiwa kukamilika Januari 15, mwakani, yote ikiwa imegharimu Sh. bilioni 75.

"Naagiza Mfuko wa Maji wa Taifa (NWF) kutoa fedha kiasi cha Sh. milion 500 ambazo nawakopesha ili kuwezesha kufanya maunganisho ya maji kwa wateja wa Tegeta A, Goba, Wazo, Madale na Mivumoni ili kuondoa sintofahamu kwa wakazi waliokaribu na mradi kukosa maji baada ya kukamilika kwa mradi wa Makongo hadi Bagamoyo," alisema Aweso.

Alisema katika maeneo ambayo yalimtesa kwa mwaka 2022 kutokana na changamoto ya upatikanaji wa maji ni Goba, Mivumoni, Bunju, Madale na Wazo, hivyo akaagiza DAWASA kuhakikisha wakazi wote wanaoishi karibu na miradi hiyo wanaonganishwa na mfumo wa maji.

"Miundombinu imekamilika ninachoomba hapa kwa DAWASA wananchi wapatiwe huduma ya maji. Kwa kuwa kazi ya ujenzi wa miundombinu ya maji imekamilika, niwatake DAWASA sasa pamoja na mipango mizuri mliyo nayo ya mwakani, kuhamishia nguvu yote kwenye kazi ya kufanya maunganisho ya maji kwa wateja kwa kuwa wananchi wanataka kuona maji yakitoka bombani," alisema Aweso.

Aweso alisisitiza kwa DAWASA na kwa mamlaka zote za maji nchini kuzingatia taratibu halisi za kufanya maunganisho ya maji kwa wananchi ndani ya muda unaotakiwa wa siku saba na si zaidi ya hapo ili wananchi wanufaike na huduma.

"Serikali imewekeza fedha nyingi ili wananchi waweze kupata huduma ya maji kwa wakati, hivyo ni muhimu sana kwa mwananchi kuunganishiwa maji ndani ya wakati kwa kuwa ni haki yake," alisisitiza.

Hata hivyo, Aweso alielezea kuridhishwa na utekelezaji mzuri wa miradi ya maji hiyo kupitia DAWASA na kuwataka wananchi na wanufaika wote wa mradi kulinda na kutunza miundombinu ya maji ili huduma iendelee kupatikana muda wote.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji ukiwamo wa Makongo hadi Bagamoyo unaoenda kuondoa shida ya maji kwa wananchi wengi wa wilaya hiyo.

## Marekani yawakumbuka wanawake wajasiriamali

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

BALOZI wa Marekani nchini, Donald Wright, amesema kuwajengea uwezo wa kiuchumi wanawake ndiyo njia ya haraka zaidi ya kuibadilisha jamii.

Wright aliyasema hayo jana mjini hapo wakati wa kufunga mafunzo ya miezi mitatu kwa wanawake wajasiriamali kutoka Wilaya ya Bagamoyo na mkoa wa Dar es Saalam.

Mafunzo hayo ambayo yamefadhiliwa na serikali ya Marekani kupitia programu ya mafunzo kwa Wajasiriamali Wanawake (AWE) inalenga kuwapa elimu na ujuzi na kuwajengea mtandao na kufungua fursa wanazohitaji ili kuwabadilisha mawazo yao na kuwa miradi halisi ya kuwaletea kipato.

"Jitihada za wanawake huwa na matokeo makubwa zaidi kwa jamii nzima kwasababu wanawake wanapofanikiwa watawekeza mapato yao katika familia na jamii zao, mafanikio yenu kiuchumi yatasaidia vizazi vijavyo na ubunifu wenu utaleta matokeo chanya kwa jamii na uchumi wa Tanzania," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Nickson Simon, aliishukuru serikali ya Marekani kwa kupitia programu ya AWE kuwezesha mafunzo hayo ambayo anaamini yatabadili uendeshaji wa shughuli za wanawake hao.

Simon alisema pamoja na serikali kutoa mikopo bado kuna kikwazo kwa kuwa asilimia kubwa ya biashara za wajasiriamali zinakufa na wengine wakikwama kurejesha fedha walizokopa.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Jesca Simon, alipongeza uwapo wa programu hiyo ambayo itawaimarisha wanawake wajasiriamali.

Jesca aliomba programu hiyo iwafikie na wataalamu ambao wanafika vijijini kuelimisha vikundi vya makundi yanayonufaika na mikopo ya halmashauri.

Mmoja wa wahitimu hao, Felista Mauya kutoka Elan Farm aliushukuru ubalozi wa Marekani kwa kuwajengea uwezo ambao utaenda kuboresha shughuli zao za ujasiriamali tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema pamoja na kuwa na fani yake ya sheria lakini alilazimika kuingia kwenye kilimo na ufugaji ambapo pia amekuwa akiwafundisha vijana kujikwamua kiuchumi kupitia shughuli hizo.

# Polisi kuwakamata watoto wanaoshindwa kwenda shule

Na Steven William, MUHEZA

JESHI la Polisi Muheza mkoani Tanga, limesema litawakamata watoto wote ambao wanafanya biashara ya kuuza karanga na mayai mitaani ambao kwa umri wao wanatakiwa kuwa shuleni.

Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Wilaya ya Muheza, Charles Ntenga, alisema hayo juzi baada ya kuwakuta watoto hao wakiuza karanga na mayai mitaani.

Alisema kunawatoto wadogo wanatakiwa kuwa shuleni lakini wanafanya biashara ya kuuza mayai na karanga mitaani wakati umri wao unawataka kwenda shuleni lakini wazazi wao wamewaachia kufanya biashara hiyo.

**Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Wilaya ya Muheza, Charles Ntenga, alisema hayo juzi baada ya kuwakuta watoto hao wakiuza karanga na mayai mitaani.**

Ntenga alisema kuanzia mwezi ujao, hataki kuona mtoto katika wilaya hiyo mwenye umri wa kwenda shuleni anauza karanga na mayai na kuonya kuwa atawakamata ili wazazi wao wafike polisi.

Alisema kuna baadhi ya watoto wadogo ambao alikutana nao mitaani wenye umri wa kwenda shuleni na kuwapa onyo na kwamba tayari wameshaondoka Muheza na kurudi kwao kuendelea na shule.

Ntenga alisema watoto wengi wanatoka wilaya za Lushoto na mkoa wa Kilimanjaro wanafika Muheza kufanya biashara hizo wengine wanatumikishwa na watu wazima na wengine biashara ni zao.

Alisema Rais Samia Suluhu anatekeleza sera ya elimu bure kuanzia chekechea na kuendelea mpaka kidato cha sita, hivyo lazima watoto wasome ili taifa liwe na wasomi wengi.

Ofisa huyo alisema anatoa onyo kwa wale watu wenye tabia ya kutumikisha watoto wadogo kufanya biashara mitaani wakati wanatakiwa kwenda shuleni na kuwataka waache mara moja kwa kuwa huo ni ukatili wa kijinsia kwa watoto wadogo.

Aliwataka wazazi wenye watoto wenye umri wa kwenda shuleni wawapeleke na atakayebainika hajampeleka mtoto wake atakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.




Meneja wa Benki ya Exim Iringa, Michael Richard (wa pili kushoto), akiwa na maofisa wengine wa benki hiyo, Aziza Msangi (kushoto) na Emanuel Bayo (kulia), wakikabidhi zawadi ya simu janja aina ya Iphone 14 Pro kwa Emanuel Lutambi mkazi wa mkoa huo, baada ya kuibuka mshindi wa droo ya mwezi ya kampeni ya "Chanja Kijanja, Kimasta Zaidi" inayolenga kuhamasisha wateja wa benki hiyo kutumia kadi za Mastercard katika manunuzi ya mtandaoni au kufanya malipo kupitia mashine za malipo (POS). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Operesheni yanasa nyara za mamilioni

Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa limetoa taarifa ya operesheni zilizofanyika katika kipindi cha Januari hadi Novemba, mwaka huu, na kukamata vitu mbalimbali zikiwamo nyara za serikali zenye thamani ya Sh. milioni 298.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Theopista Mallya, alisema operesheni hizo zilifanyika katika wilaya zote za mkoa huo na watuhumiwa wako katika hatua mbalimbali za kisheria.

Kamanda Mallya alisema katika kipindi hicho, polisi walifanikiwa kukamata meno 11 ya tembo, nyama ya nyati vipande 56 na nyara zingine ambazo zote zinathamani ya Sh. milioni 298.

Kwa mujibu wa Mallya, katika kipindi hicho pia walikamata bangi kilo 17.9 na kuteketeza shamba la bangi lenye ukubwa wa ekari 8.5.

Mallya alisema kuwa katika msako huo polisi pia walikamata lita 4,260 za pombe haramu ya moshi aina ya gongo na mitambo 42 ya kutengenezea pombe hiyo.

Kamanda Mallya alisema jeshi hilo pia lilikamata silaha za aina mbalimbali zilizokuwa zikitumika katika matukio ya kihalifu na silaha zingine wananchi walizisalimisha wakiwa wanatii agizo la serikali.

Alisema zilikamatwa silaha bunduki 49 zilizokuwa zikitumika katika matukio mbalimbali, risasi 75 za bunduki aina ya shotgun, bunduki 17 zilisalimishwa katika vituo vya polisi kwa lengo la kutii agizo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

# DED asisitiza kasi ya uandikishaji wanafunzi

Na Elizabeth John, NJOMBE

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Sunday Deogratius, amewataka walimu kuendelea kuandikisha wanafunzi wa elimu ya awali na darasa la kwanza pamoja na kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani wanaripoti katika shule walizopangiwa.

Alitoa rai hiyo juzi wakati akipokea msaada wa vifaa mbalimbali zikiwamo taulo za kike kutoka Shirika la KLF kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Milo na Shule ya Sekondari Mavala.

"Shirika la KLF wameona umuhimu wa kuwaletea vifaa hivi kama taulo za kike, madaftari, viatu na mikoba kwa lengo mwaka 2023 kila mwanafunzi ahakikishe anahudhuria shule na kuongeza bidii ya kusoma," alisema Deogratius.

Ofisa Elimu Awali na Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Daniel John, alisema vifaa hivyo vitasaidia kuwahamasisha wanafunzi kusoma na kuhudhuria vipindi kila kwa wakati.

"Kipekee nawashukuruni sana kwa ujio wenu. Kipindi kijacho cha mwaka 2023 tumejipanga vyema kuwapokea wanafunzi wapya na mazingira salama ya kuwafundishia wanafunzi hawa yako tayari. Kila mwanafunzi atasoma katika mazingira salama na tumeanza vyema kutekeleza mradi wa BOOST kwa kuanza uandikishaji wa wanafunzi wa awali na darasa la kwanza kwa mwaka mpya 2023," alisema.

"Uandikishaji wa wanafunzi wa awali kwa mwaka ujao tulikadiria kuandikisha wanafunzi 4,419 na hadi sasa tumeandikisha wanafunzi 4,281 sawa na asilimia 96.87, kwa upande wa uandikishaji kwa wanafunzi wa darasa la kwanza, tulikadiria kuandikisha wanafunzi 4,053 na tumeandikisha wanafunzi 4,036 sawa na asilimia 99.43. Kufikia Desemba 31, tutakuwa tumeandikisha wanafunzi wa awali na msingi kwa asilimia 100," aliongeza.

Mkurugenzi Mtendaji wa KLF, Ally Seif, alisema kuelekea sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, wametambua umuhimu wa kutoa taulo za kike katika shule kwa kuwa zitawasaidia wanafunzi kujisitiri pindi wanaporejea shuleni.

## Matatani kwa kujitambulisha mshauri wa Rais Samia

**Na Oscar Assenga,** TANGA

JESHI la Polisi mkoani Tanga, linamshikilia Zainabu Kagoso, mkazi wa Ukonga, jijini Dar es Salaam (50), kwa tuhuma za kujitambulisha kuwa mshauri wa Rais Samia Suluhu Hassan wa masuala ya kijeshi.

Aidha, Kasongo anatuhumiwa pia kutumia wadhifa huo kufanya utapeli katika ofisi za serikali na maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Kilindi ili kujipatia manufaa binafsi.

Jana, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Hendry Mwaibambe, alisema mtuhumiwa huyo, baada ya kukamatwa alidai kuwa yeye ni Ofisa Usalama wa Taifa na yuko Tanga, kwa kazi maalum.

"Katika operesheni zetu tumefanikiwa kumkamata mtu mmoja mwanamke ambaye amesema amekuja mkoani Tanga, hasa Wilaya ya Kilindi akiwa anaenda ofisi mbalimbali za serikali, akidai kwamba yeye ni ofisa usalama wa taifa na amekuja kwa kazi maalum.

"Kwamba yeye ni mshauri wa Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, katika mambo ya kijeshi. Ametueleza kwamba amekuja kuangalia kazi mbalimbali aliyotumwa," alisema Kamanda Mwaibambe.

Katika hatua nyingine, Kamanda Mwaibambe, alisema katika Wilaya ya Lushoto, watu wanne wamekamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na mauaji ya ndugu yao, Ally Zayumba (52), aliyeuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani hadi kupasuka kichwa.

Alisema baada ya kutokea tukio hilo, jeshi hilo lilifanikiwa kuwakamata watu hao kwa tuhuma ya mauaji yaliyotokea Novemba 14, mwaka huu katika Kijiji cha Sunga.

Alimtaja mmoja wa waliokamatwa kuwa ni Omary Issa (25), ambaye ni ndugu wa marehemu na katika mahojiano, alikiri kwamba yeye na ndugu zake wengine, ndiyo walioshiriki katika mauaji ya ndugu yao.

Vilevile, katika Wilaya ya Handeni, Kamanda huyo alisema jeshi hilo limefanikiwa kumkamata Habibu Botela (49), akiwa na meno manne ya tembo, akiyasafirisha kwa pikipiki.

Mtuhumiwa huyo alikamatwa katika eneo la Kwediboma, Wilaya ya Handeni, majira ya saa 7:00 mchana akiwa na meno hayo yaliyokuwa ameyahifadhi kwenye mfuko wa sandarusi na kupakiwa kwenye pikipiki yenye namba za usajili T 273 DKT.

# DIT, TEMDO kufanyakazi kwa ushirikiano

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

TAASISI ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) na Taasisi ya Usanifu na Ubunifu wa Mitambo (TEMDO), zimeingia makubaliano ya kufanya kazi kwa kushirikiana ili kuendeleza na kuzalisha bunifu zilizobuniwa na Watanzania, hasa utengenezaji wa vifaa tiba.

Mkuu wa Taasisi ya DIT, Prof. Preksedis Ndomba, alisema kuwa makubaliano hayo yanakuja kujibu mwarobaini wa tatizo la vifaa tiba kukosekana katika hospitali mbalimbali nchini.

Prof. Ndomba alikuwa akizungumza jana jijini Arusha, wakati wa hafla ya utiaji saini makubaliano hayo ya kufanya kazi pamoja ili kuongeza tija na thamani ya bidhaa zinazozalishwa Tanzania.

"Tunazo bunifu zilizopo tayari, ambazo zitazalishwa kibiashara kwenye karakana ya vifaa tiba ya Taasisi ya TEMDO. Kwa sababu kwa sasa inazalisha vifaa tiba vyenye ubora na viwango uliothibitishwa na Bohari Kuu ya Dawa nchini (MSD) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba nchini (TMDA).

"Aidha, Taasisi ya DIT imekuwa ikifanya bunifu nyingi, lakini zikishindwa kufanyiwa kazi kutoka kwenye nadharia kwenda kwenye uhalisia, hivyo mashirikiano hayo yatasaidia bunifu nyingi zilizowekwa muda mrefu kufanyiwa kazi, kwa kuwa TEMDO wana wataalamu wengi pamoja na mashine nyingi za kutengeneza bunifu hizo kwenda kwenye uhalisia."

"Tukiambatana nao maana yake ni kama wanatushika mkono kwenye mamlaka na kama watazikubali tafiti zetu tutakazo waletea au tukikubaliana kuboresha baadhi ya bunifu basi maana yake zinaweza kufika huko zinapohitajika. Tuna tafiti nyingi sana tumefanya kama nilivyosema," alisema.

Alisema mpaka sasa kuna bunifu nyingi za vifaa tiba walizofanya hivi karibuni na kwa kuwa TEMDO wamepata jukumu la kutengeneza vifaa tiba, na wao bunifu walizonazo za vifaa tiba ni zile bunifu ambazo hatua zilizofika wameridhika nazo.

Alisema kuwa katika taasisi yao, wameanzisha chumba maalumu cha kuhifadhi bunifu hizo, lakini mara nyingi zinaishia hapo, kwa sababu hawana mashine za kuendeleza bunifu kama walizo nazo TEMDO.

Vilevile, alisema wamelazimika kuingia makubaliano hayo, pia kwa sababu hawana bahati ya wataalamu ambao wanaoweza kuzipeleka hizo bunifu kwenye hatua ya kuendelezwa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TEMDO, Prof. Fredrick Kahimba, alisema kuwa makubaliano hayo yatasaidia watafiti wa TEMDO na DIT kufanya kazi za kitafiti kwa pamoja, ikiwa ni pamoja na kubadilishana wataalamu ili kujifunza na kuwaongezea umahiri.

"Hizi taasisi zimekutana kushirikiana kupata uzoefu wa walichokuwa nacho wao. Sisi hatuna na tulichonacho sisi wao hawana," alisema Kahimba.



Mwenyekiti wa klabu ya waandishi wa habari wa Mkoa wa Manyara (MPC), Zacharia Mtigandi, akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa waandishi Mjini Babati juzi, kushoto ni Makamu Mwenyekiti, Mary Margwe na Katibu Jaliwason Jasson. **PICHA: GIFT THADEY**

# Serikali yahamasisha kampeni kutumia madawati kijinsia

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

SERIKALI mkoani Manyara, imeanza kudhibiti matukio ya ukatili wa kijinsia, baada ya kuanzisha kampeni maalum ya kuihamasisha jamii kutumia madawati ya jinsi ya Jeshi la Polisi, kutoa taarifa za matukio hayo na kuwataja kwa siri wanaoingia makubaliano ya kumaliza matatizo hayo kienyeji.

Dhamira inayoonyesha utashi wa serikali wa kushughulikia kesi hizo. Ilitangazwa jana na Mkuu wa mkoa huo, Makongoro Nyerere, alipokwenda kuzindua ofisi za Dawati la Jinsia na Watoto la Kituo cha Polisi cha Orkesment kilichoko, Wilaya ya Simanjiro.

"Tumieni dawati lililozinduliwa leo (jana) ili kukomesha vitendo hivi, ambavyo vinatia aibu mkoa wetu. Niko tayari wakati wote kuongoza vita hii katika Mkoa wa Manyara, na hapa nawapongeza Jeshi la Polisi pamoja na wafadhili waliofanikisha ujenzi wa jengo hili, ambalo kwa kweli litaongeza chachu katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia Wilaya ya Simanjiro," alisema Makongoro.

Ofisi hizo maalum za kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia, zimejengwa na Shirika la Umoja wa Mataifa, linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) na Shirika la Utu wa Mtoto (CDF).

Kwa mujibu wa Makongoro, mkoa huo unaongoza kwa mambo mazuri, lakini inamuumiza kuona Manyara ikitajwa katika nafasi za juu kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia. "Kutokana na takwimu zinazoitaja Manyara kwa ukatili, kila kiongozi anapaswa kukemea matukio hayo ili kuiondoa Manyara kwenye nafasi ya pili kitaifa kwa matukio ya ukatili wa kijinsia," alisisitiza.

Awali, Kamishna wa Polisi (CP), Faustine Shilogile, ambaye anayesimamia Kamisheni ya Polisi Jamii nchini, alisema ofisi hiyo ya Simanjiro inafikisha idadi ya ofisi zilizoko nchini kwa sasa kufikia 58, ambazo zimejengwa nje ya vituo vya polisi.


Alisema hatua hiyo inatokana na mwongozo wa uanzishwaji wa madawati ya jinsia na watoto, ambao unataka mazingira rafiki yanayozingatia usiri katika kutoa huduma kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia.

Alisema mkakati wa Jeshi la Polisi ni kuendelea kutoa huduma bora kwa kuweka mazingira bora ya utendaji kazi yanayomfanya mteja anapofika kutoa taarifa aweze kuwa na amani hivyo ujenzi wa madawati hayo utaendelea kwa kushirikiana na wadau wengine wanaopinga vitendo hivyo.

Aidha, Mwakilishi wa Shirika la UNFPA), Dk. Majaliwa Marwa, alisema shirika hilo liliguswa kusaidia mradi wa ujenzi wa ofisi hiyo ili kuongeza nguvu ya wadau na serikali kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Dk. Marwa alisema pamoja na madawati yaliyojengwa Mkoa wa Manyara, pia wamefanikiwa kusaidia ujenzi majengo ya dawati la jinsia na watoto manane katika Mikoa ya Mara, Kigoma na Zanzibar.

Katika hafla hiyo, Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alilipongeza Jeshi la Polisi, kwa hatua ambazo wamekuwa wakiendelea kuzichukua kwa watu wanaofanya vitendo vya ukatili ikiwamo vilivyotokea hivi karibuni katika wilaya hiyo.



# Wafurahia utaratibu wa kuletwa madaktari kutoka nchini India

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WANANCHI wa mikoa ya Arusha na Mwanza, wamesema utaratibu ulioanzishwa na kupata baraka za Wizara ya Afya kuwaleta madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Apollo ya India, unawasaidia kuokoa fedha nyingi za safari ya kwenda nchini humo kupata matibabu.

Aidha, wameiomba serikali kwa kushirikiana na Hospitali ya St. Joseph ya jijini Arusha kuendelea kuwaleta madaktari hao nchini ili kusaidia watu mbalimbali wanaoteseka na magonjwa yanayowalazimu kwenda nchini India kuwafuata madaktari hao.

Akizungumza jana katika Hospitali Teule ya St. Joseph iliyoko jijini Arusha, Anneth Mushi, alisema utaratibu wa kuweka kambi za kuhudumia wagonjwa nchini mzuri, kwa kuwa umemsaidia kuokoa fedha nyingi alizokuwa azitumie kwenda India kuwafuata.

"Mimi nina tatizo kubwa mwilini mwangu ndugu zangu walichangishana na kupata fedha za kwenda nchini India wakati najiandaa kufanya utaratibu wa safari nikapata taarifa madaktari bingwa wa Hospitali ya Apolo ambayo nilikuwa nawafuata wanakuja Arusha nilishukuru na kuamua kuja hapa wamenipima nimepata matibabu nawashukuru sana," alisema.

Alisema ujio wao umemsaidia kupata matibabu kwa gharama nafuu na ni vyema serikali ikawa na utaratibu wa kuwaleta madakatari hao nchini kusaidia kupunguza gharama kwa wananchi.

Naye John Masanja kutoka mkoani Mwanza, alisema ni miongoni walionufaika na ujio wa madaktari hao kwa kuwa alikuwa katika maandalizi ya siku za mwisho kwenda nchini India kuwafuata.

"Nikiwa najiandaa nikapata taarifa wanakuja Arusha nikaanza safari ya kuja, nashukuru wamenihudumia na tatizo langu linaenda kuisha, kweli nimefurahi naomba serikali iendelee kushirikiana na wadau wa afya kuwaleta madakatari hawa nchini ili kutusaidia sisi wanyonge kuepukana na gharama za safari ya kuwafuata India," alisema.

Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Mkoa wa Arusha, Dk. Silvia Mamkwe, akizungumzia utaratibu huo, alisema serikali kwa sasa kila mara inashirikiana na wadau wa afya kuwaleta madaktari bingwa kutoka nchi mbalimbali ili kuwasaidia wananchi.

Alisema ni muhimu kwa kila mwananchi kufanya uchunguzi wa miili yao kutokana na magonjwa yasiyoambukiza kushika kasi na kusumbua watu wengi.

"Kama hapa Arusha tuna asilimia 30 ya magonjwa yasiyoambukiza ambayo yanasumbua watu mbalimbali na haya kwa asilimia kubwa husababishwa na mfumo wa maisha bwete tunayoishi wengi," alisema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali Teule ya St. Joseph, Dk. Thobias Mkina, alisema wanaunga mkono jitihada za serikali za uboreshaji huduma za afya kwa kuingia makubaliano na Hospitali ya Apollo ya kuja nchini mara kwa mara ili kuwasaidia wananchi wenye uhitaji wa kuonana nao.

Miongoni mwa madaktari bingwa waliokuja hivi karibuni katika Hospitali Teule ya St, Jospeph kutoka Hospitali ya Apollo ni Dk. Vijaya Rajakumari, bingwa wa upasuaji na upandikizaji figo.

Mwingine ni Dk. Raguaya Mir, bingwa wa saratani ya matiti, damu, koo, kizazi na upasuaji na walishughulika na magonjwa mengine pia ya tezi dume, utumbo, ngozi, ini na kibofu cha mkojo.



Baadhi ya wanachama wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga wakifurahia katika kongamano la kumpongeza Rais Samia lililofanyika siku tatu na kuhitimishwa jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Wanawake kupewa elimu utumiaji rasilimali mazao

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

WANAWAKE 2,520 wa vijiji sita katika Halmashauri ya Mji wa Babati, mkoani Manyara, wanatarajia kupatiwa elimu ya kutumia rasilimali za mazao ya kilimo na mifugo ili waweze kunufaika nazo, badala ya kundi moja la wanaume kunufaika peke yao, baada ya kuzalisha.

Akizungumzia mkakati huo, Ofisa Mradi wa Shirika la COSITA, anayeratibu Mradi wa Haki za Wanawake katika Mazao ya Kilimo na Mifugo, Rozina Julius, alisema lengo lao ni kudhibiti unyanyasaji unaofanywa na wanaume kwa wenza wao, kwa kuuza mazao ya kilimo na mifugo na kutafuna fedha bila familia kunufaika.

Alisema mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja katika vijiji vya Sigino, Daghailoy, Kiongozi, Haraa, Malangi na Hala.

"Mfano unakuta mwanamke anazalisha mazao ya shambani na anafuga ng'ombe, ila wakiuza mazao au maziwa fedha anachukua baba mama na watoto wanaambulia utupu," alisema Rozina. Alisema baada ya kuwapatia elimu ya kujitambua na kujua haki zao wanawake watanufaika na ardhi yao na uzalishaji wanaoufanya.

Ofisa mradi huyo, alisema elimu hiyo watakuwa wanaitoa kwenye mikutano mbalimbali na watashirikisha vikundi vya wanawake na kila kijiji watakuwa na vikundi vitatu.

Pia, alisema wanategemea baada ya kutolewa kwa elimu ya haki kwa wanawake, unyanyasaji wa wanaume utadhibitiwa na kila mwanamke atanufaika na uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo atakaokuwa anafanya.

Diwani wa Vitu Maalum, Zainab Sige, akizungumzia mradi huo, alisema elimu hiyo isitolewe kwa wanawake pekee bali iwafikie hata wanaume ili isaidie kuweka usawa kwa familia. Sige, alisema katika jamii kuna mfumo kandamizi kwa wanawake unaendelea na kuwanyima haki wanawake licha ya wao kuwa vinara wa uzalishaji.

Ofisa Kilimo na Umwagiliaji wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Daniel Luther, alisema haki ya mgawanyo wa mali iko sekta zote na asilimia kubwa ya mgawanyo wa mali upo katika kilimo na mifugo.

# Mongella aridhishwa ujenzi wa madarasa shule 13

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, amesema ameridhishwa na ujenzi wa vyumba vya madarasa 17 katika shule 13 za sekondari katika Halmashauri ya Meru, wilayani Arumeru mkoani humo.

Alikuwa akizungumza jana na watendaji na wananchi wa Wilaya ya Arumeru, wakati wa hafla ya makabidhiano ya vyumba hivyo iliyofanyika katika Shule ya Sekondari Muungano.

Aidha, alisema ujenzi wa vyumba hivyo umezingatia thamani halisi ya matumizi ya fedha na vinaongoza kwa ubora kati ya halmashauri zote saba za mkoa huo.

Licha ya kuridhishwa na ujenzi huo, aliwasihi viongozi wa mkoa huo, kujituma na kushirikiana ili kufikia azma ya serikali katika hatua ya kuwaletea maendeleo wananchi.

"Tumeona ufuatiliaji na ushirikiano ulioko kati ya Serikali, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wananchi Meru, mmefanya kazi nzuri sana hongereni kwa uwajibikaji huu wenye kuleta tija kwa maendeleo ya taifa letu," alisema Mongela.

Pia alisema uboreshaji wa sekta ya elimu unaofanywa na serikali unalenga kutoa elimu bora kwa kila mtoto wa kitanzania, huku wanafunzi wote wa kidato cha kwanza mwaka 2023 kuripoti shule Januari 9, mwaka 2023 bila kuchelewa.


Akisoma taarifa ya ujenzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Meru, Zainabu Makwinya, alisema halmashauri hiyo, ilipokea Sh. milioni 340 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 17 vya madarasa na samani zake ikiwamo viti 50 na meza 50 katika shule 13 za sekondari.

Aliishukuru serikali kwa kuwa vyumba hivyo vitawanufaisha wanafunzi 6,914 wa kutwa waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Zelothe Steven, amewapongeza Mkuu wa Wilaya ya Arumeru na uongozi wa halmashauri hiyo, kwa kutekeleza Ilani ya chama hicho, inayolenga kuwaletea wananchi maendeleo kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Akizungumza kwa niaba ya wazazi na walezi wa wanafunzi wa eneo hilo, Samweli Kinga mkazi wa Usa-River, alisema ujenzi wa vyumba vya madarasa hayo, utawapunguzia mzigo wa kuchangishwa fedha za ujenzi.

"Tunafarijika kuona watoto watu wanasoma katika mazingira bora na rafiki kwa kuwa serikali imefanikisha kujenga vyumba hivi kwa kutoa fedha za ujenzi na za kununua viti na meza," alisema Kinga.




Taaluma hii ya habari si lelemama, si ya yeyote






# Meya; Manispaa Ilemela tunapambana na madeni tuliyorithi kwa Jiji Mwanza

**Na Anthony Gervas, Mwanza.**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Ilemela jijini Mwanza, iligawanywa na kuanzishwa mwaka 2012 kutoka jiji hilo, ambayo ilijitegemea kuwa Wilaya ya Ilemela chini ya Mkuu wa Wilaya mstaafu mwanzilishi, John Gachocha.

Baada ya kugawanywa ilihama na madeni yaliyokuwa sehemu yao, kama vile madai fidia ya ardhi na viwanja vilivyokuwa vimepimwa na kutwaliwa na serikali kabla ya kulipwa wananchi maeneo yao.

Meya wa Manispaa hiyo, Renatus Mulunga, anafafanua zaidi kuwa wakati wanakabidhiwa wilaya, walibaki na madeni ya jiji la Mwanza, katika maeneo waliyopo hadi sasa, zikiwamo fidia za ardhi zinazoendelea kudaiwa na wananchi kila kuchapo.

"Katika mambo yanayoniumiza kichwa na kuninyima usingizi, hili la fidia ya maeneo ardhi ya wananchi hapa Manispaa Ilemela, kila mwezi tunalipa shilingi milioni 100 fidia maeneo yaliyotwaliwa na serikali, wakati tukiwa Jiji la Mwanza," anasema Mulunga.

Anaeleza walikabidhiwa wilaya wakati huo madeni yaliyopo na mali zingine, sehemu kubwa ya ardhi ilikuwa upande wao. Mulunga anadai maeneo mengi ardhi yanayodaiwa fidia, yalitwaliwa na serikali kwa ajili ya ujenzi shule na taasisi tangu mwaka 2006 wakiwa sehemu ya Halmashauri ya jiji hilo,kabla hawajagawanywa kwenda kujitegemea.

Meya Mulunga anashauri suluhisho mahususi la kutatua migogoro ya ardhi ni halmashauri kuchukua hatua madhubuti kuendelea kulipa madeni hayo polepole, huku akikiri haitajirudia tena kutwaa ardhi ya wananchi kabla hawajalipa fidia.



Mstahiki Meya Manispaa Ilemela,Renatus Mulunga akizungumza neno. **PICHA;ANTHONY GERVAS,MWANZA.**

Tofauti na hapo, anashauri serikali iwakopeshe fedha ili waendelee kupima maeneo na kulipa fidia, hata watakuwa wanarejesha taratibu fedha hizo za serikali, wanapokusanya mapato ya ndani.

Maeneo ambayo yanaweza kupimwa kwa sasa anayataja kuwa ni kata za Shibula, Bugogwa, Kahama, Kayenze na Nyamhongolo, ambako walau bado yana uwazi.

Pia, anawaonya watumishi wa serikali wanaojimilikisha viwanja maeneo ya wananchi kupitia migongo ya watu, wakibainika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao, ikiwemo kunyang'anywa viwanja hivyo.

Anawataka wananchi wanaolalamika wafike na ushahidi wa hoja zao,siyo kutoa tuhuma mitaani, kwa sababu viwanja hugawiwa na kutangazwa siku 90 kulipia walioomba kupewa na serikali, vinginevyo vinatangazwa upya kuuzwa.

Meya huyo anataja mpango mkakati wao kuelekea mwaka 2025 mpango, ni kuhakikisha upimaji viwanja vya makazi ya watu katika kata mbalimbali unatekelezwa katika sura ya ufanisi na kupunguza migogoro ya ardhi isiyo ya lazima.

**MPANGOMKAKATI**

Anatamka makusanyo ya ndani katika bajeti iliyopo, 2022/23 ni Sh. bilioni 13.1 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani, ikiwamo ushuru na Ilemela imelenga kuimarisha miundombinu ya barabara, kila kata imetengewa kiasi cha shilingi milioni 63 kulingana na vipaumbele vyake. Kuna jumla ya kata 19.

Fedha hizo zinatarajiwa kutumika kupitia mfuko wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), zitokanazo na makusanyo ya ndani vya halmashauri. Anasema, vyanzo vikuu vya ukusanyaji mapato ndani ni mialo ya samaki Igombe, Kayenze, Bwiru, masoko,stendi kuu ya mabasi Nyamhongolo,stendi za daladala za abiria,soko la samaki mwaloni Kirumba pamoja na ushuru wa mazao mbalimbali.

Vilevile anataja ushuru wa madini ya ujenzi, mawe, mchanga, kokoto,ushuru huduma za service levy,viwanda mbalimbali vya samaki kama sangara, viwanda vya nondo,vinywaji, mwalo wa Kabangaja na gereji.

Anataja, pia mradi binafsi wa ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba unaofanyika katika mwalo wa Igalagala ulioanza mwaka 2022,ambao huvunwa samaki baada ya miezi minane.

**CHANGAMOTO.**

Meya anasema, kuna changamoto nyingi kutoka kwa wananchi, ambazo ni uelewa mdogo wa baadhi ya jamii kutokuwa na mwamko wa kulipa kodi zinazowahusu, ukiukaji sheria za kujenga maeneo yasiyopimwa na yaliyopimwa.

Pia, anataja matumizi ya eneo bila kufuata taratibu za mipango miji, kama vile majengo ya miradi na biashara, kwenye makazi ya watu, sambamba na uharibifu wa mazingira sehemu mbalimbali, ujenzi holela, kukatwa miti kunakosababisha uharibifu wa mazingira, ufugaji holela mjini pasipo kuzingatia sheria au taratibu pamoja na malisho yasiyokuwa rasmi.

Kuhusu usafi wa mazingira, Mulunga anasema taka hukusanywa na mawakala majumbani katika makazi ya watu, kisha kupelekwa dampo kuu Buhongwa ambapo mawakala hao huilipa halmashauri ya Ilemela asilimia 30, huku asilimia 70 wakichukua mawakala hao.

**KUONGEZEKA WANAFUNZI.**

Mulunga anaeleza jambo jingine linalomtesa, ni kuongezeka wanafunzi shule msingi na sekondari, hata kukabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa, madawati na walimu, zikiwamo nyumba za kuishi.

Anasema halmashauri ya manispaa hiyo, inadhamiria kujenga maghorofa ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi, pia anasifu ushirikiano uliopo kati ya mbunge wa jimbo hilo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk,Angelina Mabula, akihitimisha kwa kauli mbiu "Ilemela ni yetu tushirikiane kuijenga"

BIASHARA

# Wenye vitalu vya utalii Longido walia ukame kuhamisha wanyama

**Na Jenifer Gilla**

SAA mbili kamili asubuhi, Jaffary Mohamed, Mkurugenzi wa Kampuni ya Uwindaji ya A Class Hunting and Safaris Ltd, iliyoko Kiteto, amekaa ofisini akisubiri kundi la watalii waliojisajili kupatiwa huduma ya utalii wa uwindaji, huku akiwa ametawaliwa na lindi la mawazo .

Kwa kawaida mwezi Oktoba ni wa furaha, lakini kwa Jafary, anayemiliki Kitalu cha Uwindaji cha Talamai kilichoko mkoa wa Manyara, safari hii hofu yake kubwa ni namna atakavyohudumia watalii hao, kwa sababu hakuna wanyama wa kutosha wa kuwindwa katika kitalu chake .

Jaffary anasema, hofu inatokana na wanyama wengi kuhama kutoka kitalu chake kuelekea maeneo mengine kutafuta maji na chakula, sababu kuu ni ukame uliokithiri mkoani Manyara, unaotokana athari za mabadiliko ya tabiachi.

"Unajua wanyama wanakaa mahali ambapo watapata malisho na maji na panalindwa, hawataki kukaa mahali wanapopata usumbufu wa aina yeyote. Sasa kwa mwaka huu, hakukunyesha mvua kwa misimu mitatu ukame umetawala hakuna malisho yoyote, wanyama wanakimbilia nyanda za juu kama Simanjiro," anasema Jafary.

Mkurugenzi huyo anasimulia hali hiyo inamuathiri kipato chake, kwa kuwa idadi ya watalii inapungua kutoka watalii 10 hadi kufikia watano ndani ya wiki kwa msimu wa watalii wengi.

"Sasa hivi watalii wengi wamehamia kwenye utalii wa kupanda mlima au kuona tu wanyama, kwa sababu huku kwenye uwindaji wanaona wanapoteza pesa zao, kwa kuwa hawapati wale wanyama waliokuwa wanategemea kama vile swala, kwa hiyo sisi hata kile kipato kimeathirika," anasema.

Mwingine Alli Jumbe, mwenye kitalu cha utalii wilayani la Longido, anasimulia ukame huo umempotezea takribani asilimia 50 ya watalii waliokuwa wanamtembelea kila mwaka na kurudisha nyuma malengo yake.

Anasema gharama za kuwinda wanyamapori katika vitalu hivyo kwa mwaka jana, siku tano ilikuwa Sh. milioni tano, ikihusisha muwindaji mmoja na watalii watazamaji watatu.

"Nilikuwa na mipango ya muda mrefu ya kuongeza kitalu kingine cha utalii wilayani Kiteto kutokana na watalii wengi niliokuwa nikiwahudumia miaka ya nyuma, lakini kwa hali inavyokwenda nimeona niache kwanza, watalii wa uwindaji wamepungua sana, " anasimulia



Wanyama vivutio kwenye ukanda wa utalii wa uwindaji, kunakoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: JENIFER GILLA**

Ally ambaye ni Mwenyekiti wa TLHA, anasema baadhi ya wanyama wanakufa kutokana na njaa na kiu kali inayotokana na ukame huo, hali inayowatia hasara wao pamoja na serikali.

"Tunapotembea huko porini hapa na hapa unakutana na mizoga ya nyumbu, unakutana na mizoga ya pundamilia na sisi tunaiona, jambo hilo si la kawaida. Kuna wanyama wengine hata twiga, lakini zaidi wanaoongoza kwa mizoga ni pundamilia," anasema, akitaja wanyama kama vile tembo, swala, nyumbu na digidigi nao wamekufa vitaluni.

Aidha, Jafary anasema, wanyama hao hawapendi kukaa penye usumbufu wa binadamu, ikiwamo ujangili. Anafafanua: "Katika vitalu vyetu tunavyowinda hasa 'open areas' (maeneo ya wazi), huwa wanyama wanahama kwenda sehemu ambako watapata malisho na maji. Pia huwa wanaenda mahali ambako kuna usalama na hakutakuwa na 'human conflict' (usumbufu wa binadamu) kama ujangili na shughuli nyingine za kibinadamu kama ulimaji mashamba."

Mkurugenzi na Mmiliki wa Kampuni ya Uwindaji ya Mantheakis Safaris Ltd iliyoko Longido, Arusha, Michael Mantheakis, anasema uhaba wa malisho ya wanyamapori unachangiwa na shughuli za kulisha mifugo zinazofanywa na wafugaji wa maeneo jirani.

Michel, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wenye Vitalu vya Uwindaji Tanzania (TAHOA), jamii jirani zina idadi kubwa ya mifugo, ilhali hawana sehemu ya kulisha, hata kulazimika kuvamia vitalu vilivyopo kwenye mapori tengefu ya kulishia wanyama.

Anasema mifugo inapokuwa mingi, hula mpaka nyasi zisizokomaa na kutoa mbegu zinazosababisha kuota nyasi nyingine, jambo linaloua ustawi wa nyasi, maana hazioti tena, hali inayoathiri sehemu nyingi.

### HALI YA HEWA?


Taarifa ya mwenendo wa hali ya hewa iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ya Septemba mwaka huu, inaeleza maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua yanatarajiwa kupata mvua kati ya wastani ulizoeleka hadi chini ya wastani, lakini Michael anajipa moyo, huenda mambo yatakuwa vizuri.

Pia, taarifa inagusa matarajio ya kuongezeka joto katika maeneo ya kaskazini mkoani Morogoro, pia mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar, Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

### HATUA STAHIKI

Mtaaluma wa Tabianchi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Pius Yanda, anashauri kukabili hali hiyo ya mabadiliko kuchimbwe mabwawa ya maji yatakayotumika kunywesha mifugo kipindi cha ukame.

Vilevile anashauri kutolewe elimu kwa wananchi na vijiji vinavyozunguka vitalu vya uwindaji kuhusu uhifadhi huo, kuepukana na ajali za moto, kupunguza magugu vamizi na kulinda usalama wa maeneo yote yaliyohifadhiwa kuwa ni vitalu.




Hali ya Utalii 2021/2022

Pia, anasema kuendelezwe uhamasishaji wa kutosha kutunza mazingira, ikiwamo kuhifadhi misitu ambayo ina mchango mkubwa kunyonya hewa ya kaboni, kuleta mvua na kuzuia madhara yatokanayo na mafuriko, ikiwamo mmomonyoko wa udongo.

Ally Jumbe, anakubaliana na kauli ya Prof Yanda, akisema mabwawa yakijengwa, yatawavuta wanyama wasihame kwenda maeneo mengine. Mdau, Michael anaishauri serikali iweke mikakati kuishawishi jamii jirani kupunguza idadi ya mifugo, ibaki wanayoweza kuihudumia.

Hadi sasa, Tanzania ni nchi ya pili Afrika, kwa kuwa na mifugo mingi ikitanguliwa na Afrika ya Kusini, lakini bado ndiyo nchi pekee Kusini na Mashariki mwa Afrika, isiyotumia minada ya wazi kupanga maeneo ya uwindaji.

Kamanda wa Mifumo Ikolojia ya Mto wa Mbu, iliyo chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Nchini (TAWA), Augustino Ngimilanga, anasema ukame umegusa maeneo mengi, hasa ukanda wa kaskazini mwa nchi na kufanya shida ya malisho na maji na mpaka sasa kuna mabwawa machache yanayotumiwa kunywesha binadamu, mifugo na wanyamapori.

Rai yake, hali ikiendelea ilivyo sasa kuna hatari ya kukauka na ukame huo, pia unaathiri serikali kwa sababu ya wanyama watakufa na kuikosesha pato serikali.

### MIKAKATI YA NEMC

Ofisa Mazingira wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Kanda ya Kaskazini, Albert Loti, anasema sasa wanatoa elimu kwa ya upandaji miti, kuzuia shughuli za binadamu kando kando ya maeneo yote yaliyohifadhiwa na kuzuia uchafuzi wa mazingira.

"NEMC huwa tunashirikiana na wadau mbalimbali na pale penye uharibifu tumekuwa tukiweka nguvu kurejesha uhalisia wa awali. Kwa mfano kwenye maeneo tengefu kama hayo yenye rasilimali ya wanyama na viumbe tunashughulikia tatizo kulingana na eneo husika, " anasema Albert.

### HALI YA WATALII

Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS), inaonyesha kuanzia Januari hadi Julai mwaka huu, jumla ya watalii 742,133 walitembelea vivutio nchini, ikilinganishwa na watalii 456,266 wa kipindi kama hicho mwaka jana, ikiwa ni sawa na asilimia 62.7.

BIASHARA

MSHAHARA WA LAKI TANO...

# Simulizi ya serikalini Zanzibar mapambano ya biashara haramu usafirishaji binadamu

• Waathirika na dokezo la kilichomo nyuma ya pazia



Sehemu ya Bandari ya Zanzibar, mlango wa kuingia Unguja ambao unatumika kuchuja usafirishaji haramu wa watu. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Rahma Suleiman, UNGUJA**

TANZANIA kama zilivyo nchi zingine duniani, inaathiriwa na janga la biashara ya usafirishaji haramu. Waathirika wakuu wa biashara hiyo ni wanawake, wasichana na watoto ambao kwa sasa usafirishaji haramu wa binadamu umekithiri zaidi ndani ya nchi.

Akizungumza na Nipashe mjini Unguja, Ofisa Mwandamizi wa Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ahmad Said Mwindat, anasema Tanzania hakuna mkoa ulio salama katika usafirishaji huo.

Mwindat anasema sababu za usafirishaji huo, zinajumuisha umasikini na ulaghai wa kupewa ujira mkubwa kazini, akitoa mfano wa kazi za ndani za nje ya nchi, Watanzania huahidiwa ujira mkubwa, ambao huwa ni wastani wa fedha za huko, nchini Oman Riyali 90 sawa na Sh. 500,000 inayowaridhisha.

Anataja sababu nyingine, ni uelewa mdogo kwa jamii kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu na ndoto ya kubadilisha maisha kwa kutegemea kazi zenye mshahara mkubwa.

Ofisa huyo anasema, ili kudhibiti hali hiyo, lazima jamii ielimishwe uhalisia uliopo na mitandao ya kihalifu inayotumika, pia wanaohusika wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Lazima wananchi wanapogundua hali hiyo kutoa taarifa, pia jamii kuchunga familia na kuhakikisha watoto wanapata elimu, kuepuka migogoro ndani ya familia kwa sababu migogoro mingine inawahusisha watoto kufanyiwa vitendo vya ukatili ndani ya familia zao na matokeo yake huamuwa kutoroka," anasema.

**KUTOKA SERIKALINI**

Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii Zanzibar, Abdallah Saleh Omar, anasema hali bado ni mbaya na kwa kipindi cha mwaka mmoja, serikali ya Zanzibar imeokoa wahanga zaidi ya 150 waliokamatwa Bandarini Malindi, Unguja, asilimia 90 ni watoto na wasichana, kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, kwa ajili ya kazi za ndani.

Mkurugenzi huyo anasema, kuna madalali wa kuwavusha, huku waendako yanawakuta hata vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia, mateso na manyanyaso. Anataja hatua walizozichukua, ni kuwaunganisha na jamaa zao kuwarejesha walipotoka, wakiwagharamia nauli na chakula wakati wote wa safari.

Sharifa Hamadi Makame, ni Ofisa anayeshughulika Usafirishaji Haramu wa Binadamu katika Bandari ya Malindi, Zanzibar, anasema wimbi kubwa la watoto na wasichana husafirishwa kutokea Tanzania Bara mwisho wa mwaka, baadhi yao wamemaliza mitihani yao ya darasa la saba.

Anasema tangu Agosti mwaka 2021 hadi Oktoba mwaka huu, wameshawakamata watoto na wasichana 120 bandarini wakitoka Tanzania Bara, kwa ajili ya kutumikishwa katika kazi za ndani, kinyume na Sheria ya Mtoto nchini inavyotamka.

"Watoto wa miaka 13 huletwa Zanzibar kuja kufanya kazi za ndani na ubaya zaidi, unamkuta mtoto huyo kaachishwa masomo na kima cha mishahara wanachoahidiwa ni kidogo sana, ukilinganisha na matatizo anayopitia na wengine huwa hawapewi kabisa huo mshahara," anaeleza ofisa huyo.

Anaeleza kuwa, uwapo wa bandari bubu ni kati ya changamoto zinazokwamisha udhibiti wa usafirishaji huo haramu, kwa sababu baadhi huzitumia walengwa hao; watoto na wasichana, wakishushwa na boti kutoka Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, wakati boti ikitoka Dar es Salaam, kuna ukaguzi wa watu kila mtu na kitambulisho chake ukifanywa na maofisa wa Uhamiaji, boti kutoka Pemba hazina ukaguzi.

"Baadhi ya wahalifu huzitumia meli zinazotoka Pemba kwa kusafirisha watoto na wasichana kuleta Unguja, huwapitisha katika bandari ya Tanga hadi Pemba na Pemba hadi Unguja,"anaeleza.

**WADAU & WANAHARAKATI**

Mwenyekiti wa Mtandao wa Kitaifa wa Kuzuia Usafirishaji Haramu Tanzania, Edwin Mgambila, anasema usafirishaji watu haramu uko juu, kama zilivyo nchi zingine, vitendo vimekithiri kwa wasichana kuchukuliwa kwenda mkoa mwingine au nje ya nchi.

Anasema wasichana hao hupitia manyanyaso na mateso makubwa wanapotumikishwa bila ya kupewa ujira na wengine hata hupoteza maisha, wakiathirika kiafya, baadhi wanapewa maradhi ya ngono.

Mgambila anasema, usafirishaji haramu wa ndani ni mkubwa zaidi kuliko wa nje ya nchi na maeneo yanayoongoza ni ajira kazi za ndani, pia ngono kwa kushirikishwa katika kazi za saluni, kufanya kufanya masaji, sehemu za starehe na sekta za uzalishaji kama uvuvi na viwanda.

Anataja sababu za biashara ya usafirishaji haramu binadamu kunawiri duniani, ni kwamba inawaingizia wadau kipato kikubwa zaidi, huku ripoti ya takwimu za serikali ya Marekani mwaka jana, inataja imezalisha Dola bilioni 150 (wastani Sh. trilioni 353) kwa mwaka.

Hapo anataja hatua zilizochukuliwa na serikali nchini, ni kupitishwa sheria yenye adhabu kali ya kifungo miaka 30 au zaidi kumsafirisha mtu mzima na adhabu kali zaidi kwa mtu mwenye ulemavu.

Anafafanua uzoefu wake, kwamba usafirishaji huo unaongeza wimbi la uhalifu nchini, ikiwemo vikundi viovu kama 'Panya Road na vikundi vya watumiaji dawa za kulevya.

Rutta Mtakiawa, ni Mkurugenzi asasi ya Rome Justice Tanzania, anasema, mkakati ulipo sasa ni kuwasaidia wahanga wa biashara hiyo haramu, kupata elimu sahihi, warudi katika familia zao kuepukana na mateso.

Anasema tangu mwaka 2019 hadi Oktoba mwaka huu, wameshawasaidia wahanga 764 kutoka mikoa yote ya Tanzania bara na Zanzibar, akisema huwa wanawagundua wanaosafirishwa, hasa wale wanaofika mjini Dar es Salaam, katika Stendi Kuu ya John Magufuli, wakitokea mikoa mbalimbali.

**SAUTI YA WAHANGA**

Amina (siyo jina lake halisi) ni mhanga wa biashara haramu ya binaadamu, aliyechukuliwa kutoka kwao mkoani Kigoma mwaka 2014 hadi Zanzibar, anakofanya kazi za nyumbani na mtu aliyemuamini, lakini anasema alichokutana nacho ni tofauti.

"Mwajiri wangu alinitumikisha kazi ngumu na mara nyingine alinitaka kimapenzi," anasema Amina, mwenye umri sasa miaka 18, akifafanua biashara hiyo inafanyika kwa kiasi kikubwa, ila wengi hawana ufahamu halisi.

"Unapomuajiri mtoto hiyo ni biashara haramu, kwa sababu hajawa na maamuzi yake binafsi, lakini tulio wengi hatufahamu na tunaona ni jambo la kawaida tu," anasema.

Christina (siyo lake halisi), naye alichukuliwa kutoka mkoani Mtwara mwaka 2012 wakati huo akiwa na miaka 10, mwajiri wake alimuahidi kumsomesha, lakini kama alivyo Fatma alichokutana nacho ni tofauti.

"Hakuwahi kunipeleka shule na nilipomuuliza alinitolea lugha kali, alininyima haki zangu ikiwemo mshahara wangu," anasema, sasa akiwa na umri miaka 20.

Husna Ali (siyo jina lake), ana historia ya kwenda kufanya kazi nchini Oman anasema, naye alilazimika kurejea Zanzibar, baada ya mwajiri wake kuvunja mkataba wa makubaliano ya kazi.

Anafafanua, makubaliano yao yalikuwa kufanya kazi za ndani pekee, lakini baada ya kufika huko alikutana na mateso na manyanyaso, akifanyishwa kazi usiku na mchana bila ya mapumziko.

"Kwa kweli hali hiyo ilinishinda, maana fedha ninazolipwa ni ndogo hazilingani na kazi ninazozifanya, maana nahudumia nyumba mbili kwa ajili ya kazi za ndani," anasema.

• *Soma zaidi Uk. 16.*

BIASHARA

# Hii ndiyo ajira ya Dubai na ushuhuda wa watu wanavyovushwa kinyemela kutoka nyumbani

**Na Christina Mwakangale, aliyekuwa Dubai**

"WATANZANIA wanaosafiri kutoka nchini wazingatie sheria, ikiwamo pasipoti na kupita vituo halali," ni tamko la wikiendi, kutoka kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini.

Ni kauli inayomrejesha mwandishi wa makala hii mwezi mmoja juu ya alama, akiwa katika jiji maarufu linalotikisa biashara ya duniani, Dubai, ambako alipatwa na kiulizo ajira ya watu wanaosafirishwa kufanya kazi huko majumbani.

Kimsingi, dhima kuu ya swali ilikuwa kudadisi kwa nini wanahitajika kwa wingi huo, haki zao kisheria na kiusalama zikoje?

Nipashe ikiwa bado ndani ya mitaa ya jiji hilo, hasa eneo maarufu kwa Waafrika, Deira, inakutana na Mtanzania anayejitambulisha kwa jina moja la Amina, 'mwenyeji fulani' wa huko anafafanua sababu:

"Dubai kwa kuishi maisha ni rahisi sana, ila ili utoke Tanzania uwe na pesa ya nauli na pasipoti, ukifika huku kuna mawakala wakukutafutia kazi au kama una mtaji wa kununua vitu unanunua na kumtumia mtu aliyepo Tanzania na anakuuzia.

"Kadri unavyozoea una fahamu namna ya kupata kazi zenye kipato kikubwa. Mimi nilipokuja huku nilianza kufanya kazi za ndani kwa mshahara wa Sh 500,000 kila mwezi.

"Wenzetu hawana ubabaifu nafikiri kutokana na wana imani sana, hivyo wanakulipa ujira wako ikifika tarehe. Ila baadhi huwa wanahofia kupotelewa na vitu ndani mwao, ukifika huko kama ni Mtanzania bosi wako ataishikilia pasipoti kwa usalama wake."

Amina, ambaye hulka yake kwa sasa ni 'mjanja wa Dubai', anasimulia utaratibu wa kumtunza 'dada wa kazi' wenye nyumba wanapotoka, humfungia ndani mtumishi huyo, ama kwenye nyumba kuu au ndani ya mazingira ya kazi, wakihofu asitoroke au kuwaibia.

Kwa mujibu wa Amina, imani iliyoko kwa wenyeji wa Dubai, tabia ya wizi haipo miongoni mwao, bali wanayo wageni ambao ni wengi jijini humo, ikizingatiwa inatajwa wastani wa theluthi tatu ya wakazi wake ni wageni.

**WAENDAO DUBAI?**

Ikirejewa nyumbani, yametawala malalamiko ya ama safari au usafirishaji haramu wa Watanzania na kwingineko duniani, umma unaotinga nchi za kiarabu kusaka maisha, kukiwemo Dubai.

Hapo ndipo dodoso la Nipashe ndani ya siku 30 tangu ikanyage mguu nyumbani ukirejea kutoka Dubai, ilitaka kupata ukweli wa kinachojiri na mzizi wa sababu za safari hizo za nchi za Uarabuni, pengine na kwingineko kwa misingi inayokinzana na kile anachokiwekea angalizo, Naibu Waziri Sagini, msomi wa ualimu na mtaalamu wa saikolojia ya watoto ngazi ya juu.

Hapo ndipo, inakutana na simulizi ya Aisha Abdallah (si jina halisi), aliyemuacha mtoto wa miezi mitatu kwenda Uarabuni kufanya kazi, hajaishi naye tena leo hii ni mhitimu wa darasa la saba, mwezi ujao anagonga hodi shule ya sekondari.

Mama Rose (si jina lake halisi), anayemfahamu vyema na hata kushirikiana katika ajenda hiyo, anataja sababu kuu ni kipato, akipigania mshahara wa Sh. 500,000 iliyomrusha roho itamnusuru na shida zake.

Mama Rose anasimulia kuwa Aisha, mkazi wa Ilala, jijini Dar es Salaam, ni miongoni mwa wengi waliochukua hatua ya namna hiyo, wanasafirisha watu kibiashara na wao wenyewe wanajitosa kwa safari hiyo.

Ni kasi inayochukuliwa kuwania ajira hizo zenye viulizo, huku jarida la kimataifa la Forbes, likidokeza biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu duniani kote, inawafikia watu milioni 30. Pia, inanukuu takwimu za Shirika la Kazi Duniani (ILO), kuwazalishia wakala faida ya Dola za Marekani bilioni 150 kila mwaka.

Kadhalika, mtaalamu wa sheria za kimataifa, Prof. Khoti Kamanga wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), anaainisha kundi la wahamiaji wanaoongezeka siku zote hasa kutoka nchi zinazoendelea wanajumuisha; wakimbizi, waomba hifadhi, biashara haramu ya binadamu.

"Uhamaji ni tatizo la siku nyingi hata katika maandiko limo. Changamoto ni kupoteza rasilimali watu ambamo kuna wasomi, Je, uhamiaji ni fursa au kikwazo, unatumikaje kukuza uchumi, diaspora imesaidiaje Afrika, nchi wazawa?," anasema Prof. Kamanga, mshauri wa masuala ya wahamiaji.



Soko mojawapo lililoko Dubai, UAE.

Shirika la Uhamiaji Duniani (IOM) linasema mwaka 2019, kila moja ya kwa mabara haya, Ulaya na Asia ilikuwa mwenyeji wa wahamiaji wa kimataifa karibu milioni 82 na milioni 84, idadi inayojumuisha asilimia 61 ya jumla ya idadi ya kimataifa ya wahamiaji wote pamoja.

IOM inakadiria hadi mwaka 2019 duniani kulikadiriwa idadi ya wahamiaji ni milioni 272, ambao ni sawa na asilimia 3.5 ya idadi ya watu duniani, huku sababu ya kuhama ikitajwa zinazohusiana na kazi, familia na masomo.

**SAFARI YA AISHA**

Aisha mwenye umri wa miaka 32, akiwa na miaka saba ughaibuni, elimu yake iliishia sekondari kidato cha nne pasipo kuwa na stadi za ziada, akaamua kujikita katika ujasiriamali mdogo.

Mama Rose anayemfahamu fika, anamuelezea kwamba alipenda sana kufanikiwa hata akawa na wivu wa maendeleo, lakini akasuasua na kipato cha chini cha nyumbani kwao.

"Siku moja tukiwa tunapiga stori na wenzangu, mmoja akasema kwa hali hii si tutafute maisha nje, mmoja akauliza nauli ya ndege utaipata wapi?," Mama Rose, anadokeza chimbuko la safari.

Anaendelea na simulizi ya Aisha: "Mmoja akajibu kuna namna unaweza kwenda kufanya kazi za ndani Uarabuni, ukalipwa mshahara mzuri, ukatoboa."

Hapo ndipo hulka ya safari ya kiuchumi ilipomtawala Aisha tangu siku hiyo akaingiwa na dhamira ya safari, mtaji wa kwanza ni kilekile Nipashe ilidokezwa jijini Dubai; kupata nauli na pasipoti.



.Mwonekano wa jiji la Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), na mandhari yake ya hivi karibuni. **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE.**

Anaendelea kusimulia "kupitia tu mtandaoni akaunganishwa na ajenti (wakala) Mtanzania, anaishi huko Uarabuni, ambaye 'hu-deal' (hushughulika) na wanaotaka kazi za ndani."

Kwa mujibu wa Mama Rose, swali la kwanza la wakala alitaka kujua Aisha alivyojiandaa, naye akajibu hana pesa, akiahidi angetafuta.

Aisha alimjuaje Mama Rose? Hapo msimulizi huyo anaifafanulia Nipashe, kwamba ujirani na ushoga kati yao, ingawa kuna tofauti ya umri, ulimfanya Aisha amfuate na kuomba mkopo wa Sh. milioni 2.3, kukidhi hitaji lake la nauli na pasipoti na hakumficha dhamira ya safari yake.

Mama Rose anasema kwa mara ya kwanza hakuweza kumkopesha hakuwa na kiasi hicho, lakini mara ya pili ikiwa miezi kadhaa imepita, yeye akiwa amestaafu utumishi wa umma na kupata mafao.

Anasimulia kwamba Aisha katika mawasiliano yake na wakala, safari hiyo akamhitaji atafute timu ya watu 10, jukumu wa kwenda Dubai, pia aratibu mkopo wa kufanikisha safari zao, ambao marejesho yake yangefanyika kwa faida kiasi pindi watakapoanza kazi Uarabuni.

Mama Rose anasema alishawishika na akiwa mstaafu alimega sehemu ya pensheni yake kufadhili mkopo wa safari hiyo na anakiri kundi la watano waliondoka kwanza alirejeshewa fedha zake kwa utaratibu waliokubaliana.

Anafafanua, kila mwezi alitumiwa Sh. 600,000 na Aisha hakuwa katika hao walioanza safari kutumikia kazi za ndani, akirejea maelezo ya wakala kwamba walitakiwa mabinti wenye umri mdogo zaidi.

Kwa mujibu wa Mama Rose, walikubaliana na Aisha kuongeza idadi ya mabinti wa kazi kufika 10 ilikuwasafirisha Uarabuni, yeye akiwa amenogewa na faida ya riba kutoka kwenye uwekezaji wake.

**MKWAMO WAANZA**

Mama Rose anakumbuka mwaka 2009 maandilizi kwa ajili ya safari ya hao mabinti, walifanikiwa kupata pasipoti na dhamira ya maombi ya safari yao ni kwenda kutalii.

Anasema ujanja uliotumika kuwapitishia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), walivuka kwa awamu tofauti, ili wasijulikane kundi la rika fulani la ujana lina safari tata.

Mama Rose anasimulia, kuna siku kundi la wachache wakiwa katika awamu yao kuvuka uwanja wa ndege, mmoja alishindwa kuhimili maswali ya udadisi ya Uhamiaji, hata akazuia safari yake, huku msindikizaji akiwa Aisha.

Mama huyo anarejea maswaii yaliyomkwamisha binti huyo, ni pale alipojibu hajui anakoenda, ila anasafiri kwenda kufanya kazi na anayemsafirisha akamtaja kwa jina la 'mwenyeji wake' hapo akimaanisha Aisha,

"Ndege iliondoka na mabinti watatu, wakabaki hao wawili na kule makubaliano ni waende 10 na pesa ilishapokelewa na ajenti," anasimulia Mama Rose.

Ni hali iliyoleta msuguano kati ya Aisha na wakala Uarabuni, kisa kikuu pengo la idadi ya watu, jambo lililomfanya Aisha aamue kuliziba kwa kufunga safari mwenyewe siku nyingine.

Kimsingi halikuwa jambo jepesi, kwani Aisha alilazimika kuuza kila kitu nyumbani kwake kupata nauli, huku mwanawe wa miezi mitatu akimuachia mdogo wake na daima hajawahi kumrejea hadi sasa akiwa mhitimu wa shule ya msingi.

**KIBAO CHAGEUKA**

Mfadhili huyo wa safari ya kina Aisha, anasema naye akajikuta amefilisika pensheni yake yote, hata mara kadhaa alipoenda katika makazi ya ndugu za Aisha, akafahamishwa hupiga simu mara chache na kuna kipindi hapatikani kwa miezi mingi.

Vivyo hivyo ndivyo anavyotuma pesa, akiwa na ujumbe 'pesa kidogo apelekewe anti' kwa maana ya Mama Rose. Anaeleza hali ilivyomuwia ngumu, hata akalazimika kuomba ufadhili kwenye familia hiyo alikokaribishwa akaishi, akahamia ambako nako kijamii hapakuwa nafuu kwani akageuzwa kimya kimya kuwa mwangalizi wa watoto.

**MIKATABA KIMATAIFA**

Azimio la Umoja wa Mataifa (UN), kuhusu Haki za Binadamu la Desemba, 1948 baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, lina makubaliano 30 ya ulinzi kiutu.

Hapo inajumuisha uhuru wa watu, hadhi na haki zao ni sawa; kuondokana na utumwa au utwana, haki ya kwenda na kuishi kokote duniani.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Taaluma hii ya habari si lelemama, si ya yeyote






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

DESEMBA 17 mwaka huu, ni siku iliyoweka alama kubwa kwenye tasnia ya habari nchini. Ni siku ambayo wanahabari wote waliwakilishwa kwenye kongamano kubwa la maendeleo ya sekta ya habari.

Katika kongamano hilo lililofanyika kwenye ukumbi maarufu wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, wakongwe na chipukizi wa masuala ya habari na wadau wa tasnia hiyo walihudhuria na kutoa yao ya moyoni, kwa lengo la kuendeleza sekta.

Changamoto ziliibuliwa kuhakikisha tasnia hii inabaki kuwa 'mhimili wa nne' kutokana na umuhimu na dhima yake katika jamii, ikielimisha, kuhabarisha, kuburudisha na sasa kukosoa kama msingi wa kuwapo kwake.

Katika jamii, kupongezana na kukosona kupo, lakini kukosoana huwa na tija zaidi ya kupongezana na kusifiana. Hivyo, kwa muktadha uliokuwapo siku ile, egemeo kubwa lilikuwa kwenye kukosoa na kuambiana jinsi ya kukabiliana na changamoto zilizopo.

Suala la uchumi kwa wana habari liliibuka zaidi huku likisindikizwa na la weledi, maadili na ujuzi wa kazi yenyewe kwa wanahabari. Si uongo, kwamba wanahabari leo wana hali mbaya sana kiuchumi.

Lakini, pia si siri kuwa weledi kwa wanahabari wengi umepungua sana, kutokana na mazingira ya kazi lakini pia maandalizi wanayopata wakiwa katika maeneo ya mafunzo na hivyo kushajihisha usemi wa Kiingereza: "Taka ndani, taka nje".

Kama ukweli ulivyotamalaki siku ile ya kongamano, wanahabari wengi wanaishi kwa kubangaiza kutokana na kukosa kipato cha kuridhisha kunakosababishwa na kufanya kazi bila mikataba na kuwapa fursa waajiri kuwanyonya.

Si siri kuwa kuna wanahabari hivi sasa nchini wanachangia vyombo vya habari si ili kupata kipato, lakini basi tu kusikiwa na vyanzo na kupata anuani, kwamba ukinitaka niko mahali fulani naandikia au natangazia. Kwa kifupi hawalipwi hata senti kwa mchango na jasho lao.

Ni hali hii iliyojibainisha zaidi katika kipindi fulani, vyombo vya habari vilivyokuwa vingi hususani binafsi, vilielemewa kiutendaji na hata kuzua malalamiko mengi, kukiendana na kutojiamini kitaaluma.

Mbali na hilo la uchumi, hili la kitaaluma nalo linasababisha matatizo makubwa ya kushuka kwa heshima ya vyombo kwa kutoka kwenye reli ya taaluma na kufanya mambo kienyeji katika utangazaji na uandikaji wa habari.

Hivi sasa katika vyumba vya habari utadhani hakuna usimamizi. Lakini, yawezekana hakuna kama ilivyokuwa zamani, kwani sasa mambo yanajiendea kama yalivyo kwa mtu kuamka asubuhi hana mpango na kuingia studio kutangaza chochote alicho nacho kichwani kufurahisha baraza.

Mtu sasa anaandika habari, huyo huyo anaihariri na huyohuyo anaipanga kwenye ukurasa, hakuna mikutano katika vyumba vya habari ili kupanga nini kiandikwe na nani, saa ngapi na kutoka wapi kwa nani. Matokeo yake bidhaa inayotoka inakuwa haina uzito na hivyo kukosa soko na kuathiri kipato.

Hivi nani hasikilizi redio zetu hizi zinavyotangaza, televisheni zetu hizi zinachoonyesha kwa hadhira? Hivi tukilinganisha kiumakini ilivyokuwa Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) enzi hizo na hizi zetu za leo tunagundua umakini upo kweli?

Watangazaji wanakaa kama wako kijiweni na kubishana, kutambiana na hata wengine kutoleana matusi, wengine kukurupuka kukimbia kana kwamba kuna tafrani, eti nia ni kufurahisha wasikilizaji na watazamaji!

Mtangazaji anatangaza ;Kiswanglish' katika redio ya Kiswahili hasa wajiitao wachambuzi wa michezo! Anakohoa bila kuzima kifaa cha sauti, anapiga chafya waziwazi! Zamani akiwapo msimamizi kuhakikisha ukikohoa unazima msikilizaji asisikie!

Leo hii msanii mchekeshaji eti anachukuliwa moja kwa moja kuwa mtangzaji redioni au kwenye luninga! Kisa mchekeshaji atavutia wasikilizaji na watazamaji! Huku kama si kubaka taaluma ni nini? Sawa na kumchukua nahodha wa mtumbwi akaendeshe boti kwa sababu anajua kushika kasia!

Sawa na kumchukua dereva wa mabasi yaendayo haraka akaendeshe treni kwa sababu tu mabasi nayo ni marefu kama treni, kweli? Hapo ndipo taaluma ilipoanza kuchechemea. Mwandishi wa habari na mtangazaji hawajui lugha wanayoitumia, kweli watakuwa watangazaji na waandishi wa habari?

Mtangazaji anashindwa kutangaza majina ya kigeni, lakini anakutangazia fainali za Kombe la Dunia; Argentina anaitamka Argentina hivyohivyo, Mexico anatamka Mekiko, unamsikia eti Giroud anamtamka Yiruu! Kweli? Kwanini asijiandae kwa kuuliza wenye lugha yao wanayatamkaje ili atunufaishe wasikilizaji wake?

UCHUMI

## MAPINDUZI UFUGAJI BAGAMOYO

# Mjenzi wa barabara awapa 'ofa' wafugaji malambo, kiwanda machinjio chajengwa

**Na Julieth Mkireri, BAGAMOYO**

HALMASHAURI ya Chalinze, wilayani Bagamoyo, ni kati ya maeneo yenye wafugaji wengi katika mkoa wa Pwani. Kwa sasa Wilaya ya Bagamoyo, inakadiriwa kuwa na mifugo zaidi ya milioni moja, kwa wastani ng'ombe zaidi ya 30,923, mbuzi 158,402, kondoo 65,828, nguruwe 10,372, kuku 512,193 na punda 1,614.

Katika ufugaji huo, kama ilivyo kwingineko kumekuwapo migogoro kati ya wafugaji na wakulima, inayochangiwa na uhaba wa malambo kwa ajili ya maji ya mifugo na maeneo ya malisho.

Migogoro hiyo imekuwa ikishamiri hasa kipindi cha kiangazi, pale jamii ya wafugaji inafikia hatua ya kutembea umbali mrefu na wengine kuhama makazi yao, kwenda kusaka malisho na vyanzo vya maji.

Ni hatua ambayo matokeo yake inakwaza jamii ya wakulima na serikali kwa jumla, kwani usafirishaji mifugo hiyo hupita kwenye mashamba ya wakulima na kunafanyika uharibifu wa mazao.

Katika kukabili shida hiyo, kwenye kata ya Vigwaza Bagamoyo amejitokeza mdau ambaye ni mkandarasi, kampuni ya ujenzi ya Estim, inayojenga barabara eneo hilo akiwasaidia wafugaji wa eneo hilo.

Mkandarasi huyo tangu mwaka jana, amekuwa akitoa huduma ya maji kila siku kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na mifugo, pia majani, pumba na kuchimba malambo ya kusaidia mifugo kupata chakula na maji.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (mwenye suti nyeusi), baada ya kuweka jiwe la msingi katika Kiwanda na Machinjio ya kisasa inayojengwa Kwazoka Vigwaza, Bagamoyo. **PICHA ZOTE: JULIETH MKIRERI.**

### WAZIRI MIFUGO

Hapo ndipo anajitokeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akitoa mapendekezo kadhaa kwa jamii ya wafugaji. Akiwa kijijini Kwazoka, Vigwaza akiweka jiwe la Msingi la ujenzi wa Kiwanda na Machinjio ya kisasa, mradi unaotekelezwa na kampuni ya Union Meat Abottoirs, anawataka wafugaji kumiliki mifugo wanayomudu kuihudumia.

Waziri Ndaki anasema, ufugaji wa kizamani umepitwa na wakati, kinachotakiwa sasa ni kubadilika kwa kuwa na idadi ya mifugo inayowakwamua kiuchumi. Anafafanua kuwa, hiyo inafanyika kupitia njia za kuinenepesha, ili ipate soko kwenye machinjio yanayoanzishwa kwenye masoko nje ya nchi.

"Soko la mifugo kwa sasa limepanda, hivyo ni vema wafugaji wakajitafakari na kufuga kisasa mifugo michache watakayomudu, kuiweka kwenye afya nzuri kuinenepesha iuzike," anasema waziri akiwa na msisitizo "hii habari ya kuswaga mifugo kwa masafa marefu inaanza kupitwa na wakati ng'ombe huyo hatafaa kwa machinjio hii."

Waziri Ndaki anayempongeza mwekezaji kwa hatua ya kujenga machinjio, anasema wizara yake imejiandaa kuanza kutoa elimu ya ufugaji kisasa wenye tija na maofisa mifugo watawezeshwa kusambaa nchi nzima kutoa elimu hiyo, akiamini itasaidia pia kupunguza migogoro kati ya wafugaji na watumiaji ardhi, waliozungukwa na idadi kubwa ya wafugaji.

### WENYEJI KISERIKALI

Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, ambaye pia ni Naibu Waziri mwenye dhamana na ardhi, pia msomi wa sheria anaunga mkono uwapo wa machinjio hayo, akisema unakaribisha mapinduzi katika suala la machinjio ambayo hayakuwapo katika halmashauri hiyo.

Aidha, anaeleza matarajio yake kwamba, kuwa na machinjio ya kisasa yatawabadilisha wafugaji kuhamia kufuga kisasa, kwa kuwa na mifugo michache hali inayotoa dira ya kupunguza migogoro kwenye jamii ya jimbo lake.

Naibu Waziri huyo wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, anamuomba Waziri wa Mifugo, kusaidia kukabili vitendo vya baadhi ya wafugaji wanaogeuza kila eneo kuwa la kufuga, pasipo kufuata taratibu, naye akiwakumbusha ujio wa machinjio ni neema kuwabadilisha na kuwakwamua kiuchumi.

"Tubadilishe mifugo yetu iwe fedha, serikali itengeneze mkakati wa kuona inasaidia wafugaji wenye mifugo mingi, pia kuwezesha wawekezaji wa machinjio kama haya yasikose mifugo," anasema Ridhiwani.

Anafafanua kuwa Chama cha Wafugaji nacho kina wajibu wa kuwaelimisha wanachama wao kuwatumia wataalamu kuandaa mifugo yao kisasa, iweze kupata soko, hususani kwenye machinjio hayo na maeneo mengine.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Kasilda Mgeni, anasema kuna vijiji tisa vya wafugaji, sita vimo katika Halmashauri ya Chalinze, ambavyo ni Lukenge, Chamakweza, Miono, Kihangaiko, Mindutulieni na Magulu Matali na vijiji vitatu vya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, ni Mkenge, Kidomole na Fukayosi.

Anaeleza kuwa sekta ya mifugo katika mwaka wa fedha uliopita, imechangia Sh. milioni 371,580,400 kwa mapato ya wilaya ya Bagamoyo, fedha zilizokusanywa kutokana na ushuru wa mifugo mnadani, machinjioni na ukaguzi wa nyama choma mnadani.

Kasilda anaainisha makusanyo hayo, kwamba Halmashauri ya Bagamoyo ilikusanya Sh. milioni 72,828,800 na Halmashauri ya Chalinze Sh. milioni 298,751,600, akisema uwekezaji wa mradi huo wa machinjio, umegharimu Sh. bilioni 14.

Diwani wa Vigwaza Mussa Gama, anapongeza kuwepo kwa mradi huo ambao utapunguza kikwazo cha ajira katika kata hiyo lakini pia fursa kwa wafugaji kujikwamua kiuchumi.



Ng'ombe wakinywa maji yanayosambazwa na Mkandarasi kampuni ya ujenzi ya Esti, iliyoko Bagamoyo.

Aidha Gama anaiomba Wizara ya Mifugo, kuona namna ya kuwachimbia malambo kwenye kata hiyo yaweze kusaidia wafugaji kupata urahisi wa kunywesha mifugo yao kutokana na kikwazo cha maji kilichopo sasa.

Diwani huyo, pia anawaomba makandarasi wanaopata kazi kuiga mfano wa Mkurugenzi wa Estim, waisaidie jamii kutatua kero zinazowakabili, ikiwemo vyumba vya madarasa, maji na uchimbaji wa malambo na visima.

Mwenyekiti wa Chama Cha Wafugaji Mkoa wa Pwani, Ngobere Mfamau, anasema kuanzishwa mradi huo ni fursa kwa wafugaji na kwamba watatoa ushirikiano kwa mwekezaji huyo pale inapohitajika.

### WENYE KIWANDA

Mkurugenzi wa Kiwanda hicho, Mariam Ng'wani, anasema kampuni hiyo inamilikiwa kwa ubia wa wawekezaji wazawa wa nje ya nchi na imewekezwa katika kiwanda hicho, kwa kutambua fursa ya wingi wa mifugo nchini.

Anasema hadi mradi kukamilika, utagharimu kiasi cha Dola za Marekani milioni sita, sawa na Sh. Bilioni 14 utakapoanza na utakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 2000 pamoja na mbuzi na kondoo 7000 kwa siku.

"Mradi huu umegawanyika katika maeneo matatu ambayo ni machinjio, uchakataji, uhifadhi na usafirishaji pamoja na unenepeshaji," anasema mkurugenzi huyo.

Anaendelea: "Kampuni yetu inalenga kuleta mapinduzi katika tasnia ya nyama nchini kwa kufungua masoko ya ndani na nje ya nchi, pamoja na kuwa na vibali vya kimataifa tutashughulika, pia kuhifadhi na kusafirisha nyama kwa kutumia vifaa na mitambo ya kisasa."

Mkurugenzi huyo anatumia nafasi yake kumuomba Waziri wa Mifugo, kupatiwa eneo katika Ranchi ya Ruvu, lenye ukubwa wa hekta 1000, watakalolitumia kupumzisha mifugo na mradi wa unenepeshaji, ili kupata nyama bora itakayoshindana katika masoko kimataifa.

"Mradi wa unenepeshaji, utaenda sambamba na ujenzi wa miundombinu ya kulishia pamoja na ulimaji wa nyasi, pia utatumika kama shamba darasa kwa wafugaji wa jirani katika kukabiliana na upungufu wa malisho unaowakabili," anasema.

Kwa mujibu wa Mariam, mradi utaajiri wataalamu katika sekta ya malisho na wafugaji watafundishwa mbinu za kitaalamu kuandaa na kuhifadhi malisho, itakayosaidia kuondokana na vifo vya mifugo kwa kukosa malisho na maji.

UCHUMI

# Mbadala wa kunusuru punda kwa kuwekeza ranchi zao wasitoweke



Punda wakiwa katika matumizi yao yaliyozoeleka. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

KAMPENI yenye vielelezo vya kibiashara, lakini hasa ni maadili inaendelea katika nchi kadhaa za Afrika hasa ukanda wa Afrika Mashariki ulio na mifumo ya ushirikiano katika sekta tofauti.

Ni jitihada ya kuzuia punda wasiteketee kutokana na kutafutwa sana kwa ngozi yao ambayo huko Mashariki ya mbali, inatakiwa kutengenezea dawa za kienyeji na nyama yake inauzwa kama kawaida. Ni jitihada inayojikita katika kumtumia mnyama huyo kama sehemu ya uchumi wa jadi wa jamii tofauti za Afrika Mashariki kote.

Jitihada hizo zinaingia katika wakati mgumu kwani wanyama hao, tofauti na ng'ombe huzaana kwa taabu na kwa uchache, hivyo hawafugwi kwa ajili ya nyama kwani hawataongezeka inavyotakiwa. Sehemu yao kubwa ni katika uchumi wa kifamilia kama mnyama wa kubeba mizigo, kama ngamia alivyo katika maeneo ya jangwani na utumiaji huo wa punda sasa uko mashakani.

Kazi zilizokuwa zinafanywa na punda zinaweza kuelekezwa kwingine, kwa mfano kupeleka mizigo sokoni, au mazao kutoka shambani hazimhitaji tena mnyama huyo baada ya kuenea kwa pikipiki tofauti, zile za abiria, za mizigo na za matairi matatu.

Si habari tena kusikia kuwa punda wako hatarini kupotea kama aina ya mnyama kwani wanatafutwa sana Mashariki ya mbali, eneo la dunia linalofahamika kwa vyakula vya kiaina, na pia kwa dawa za asili zenye vianzio vya kushangaza. Kupanuka kwa biashara kati ya China na nchi nyingine kumewezesha kuuzwa kwa punda wengi na kupungua kwa kasi kupatikana wanyama hao maeneo ya vijijini.

Punda ni mmyama aliye karibu na binadamu, asiyeweza kuishi porini ambaye muda wake wa kutumika katika mandari ya familia kiuchumi umekaribia mwisho. Kwa maana hiyo, linazuka swali kama mnyama huyo aachiwe nguvu ya soko auzwe kiholela amalizike au kutoa zuio la jumla la kutouzwa wanyama hao, hata pale walio nao majumbani hawawahitaji.

Wataalamu wamekuwa katika makongamano ya hapa na pale miaka kadhaa sasa kujadili suala hilo, wakilenga zaidi zuio la kuuzwa wanyama hao kwa ajili ya ngozi yao, kwani hawana sifa maalum kwa upande wa uvunaji wa nyama zao. Suala ni walengwa wa miito hiyo, kujua kama inaendana na mahitaji yao halisi, au kuzuia mauzo ni kuisaidia tu serikali.

Bado utafiti unaendelea ni kwa kiwango gani kasi ya kuuzwa punda maeneo mengi inaweza ikawa imeathiri mazingira ya wanawake na watoto maeneo tofauti ya vijijini. Wanawasaidia kubeba mizigo kupeleka sokoni au kutoka huko, pia shambani, hivyo punda anapouzwa inaweza kuwa ni kwa manufaa ya wanaume ambao ndiyo wenye sauti na mamlaka katika nyumba.



Punda wanapokuwepo ni kama kubeba mizigo bure kwa upande wa wanawake na watoto, wakati wanaume ni rahisi zaidi kuchangamkia bei inayotolewa na mfanyabiashara kutoka mbali. Hata wangelipa kana kwamba wananunua ng'ombe, hawapati hasara kwani ng'ombe wanauzwa kwa uzani ili kuuza nyama, ngozi ikiwa ni bidhaa ya ziada isiyo na thamani kubwa.

Kuuza punda ni suala tofauti, kwani nyama yake ni ya kawaida na hakuna uhakika ina soko la kawaida au inaweza kubaguliwa, ila ni rahisi kutazamia kuwa ina soko la kawaida. Soko lake la ngozi ni kitu tofauti, kwani hapo inakuwa bidhaa maalum, tofauti na ngozi ya ng'ombe na mbuzi.

Endapo kuna ukweli kuwa, wanawake na watoto wanapata tabu zaidi wanaume wanapouza punda kwa wanunuzi kutoka mbali au kwa mawakala wao, inawezekana wakuu wa maeneo husika kukemea tabia hiyo.

Akiuzwa punda mtu anaweza labda kuulizwa kulikoni, kama kanuni zinaweza kutungwa za kuhitaji vibali vya kuuza wanyama hao na kimsingi hakuna vibali maalum vya kuuza wanyama wa kufugwa. Ni jitihada inayoweza kuendana na hitaji la kupunguza ugumu wa majukumu ya wanawake na watoto, ambayo mara nyingine hukaribia ukatili wa kijinsia, kwa mfano punda auzwe halafu kina mama ndiyo wabebe mizigo.

Liko eneo jingine, ambalo wawekezaji wa mifugo hawajalizungumzia sana, yaani kufungua ranchi za punda kama zilivyo za ng'ombe, au kuongeza punda katika ranchi za kawaida kwani mauzo yake inaelekea yana faida kubwa sana masoko ya mbali. Punda mmoja ni malighafi ya kiasi fulani cha dawa kwa kutumia ngozi yake na ili kurahisisha upatikanaji wa punda bila kuwaegemea sana wafugaji wa jadi wa mnyama huyo, mkakati wa kufungua ranchi za wanyama hao ni budi uwepo.

Suala hapa ni aina gani ya wawekezaji watalenga biashara kama hiyo, iwe ni upanuzi, ongezeko la ranchi za sasa kuongezea bidhaa hiyo, au wageni wanaweza kufanya kazi hiyo vyema zaidi kwa kulijua soko katika nchi hizo.

(mwisho)

# Mbadala pembe viboko kuziba pengo la ndovu kunawahatarisha kutoweka

**Na Mwandishi Wetu**

Kuongezeka kwa vikwazo vya usafirishaji wa pembe za ndovu kumesababisha kuongezeka kwa biashara ya meno ya kiboko, wanaharakati wa wanyamapori wanaonya uwezekano wa madhara makubwa kwa spishi ambayo tayari imeorodheshwa kama "katika hatari ya kutoweka".

Wakati Uingereza ilipotangaza mwezi wa sita mwaka jana kuwa inapiga marufuku biashara ya pembe za ndovu, shirika la usaidizi la ustawi wa wanyama lilichunguza kile kilichotokea katika soko la mtandaoni.


"Tuligundua ongezeko la biashara ya pembe za ndovu nchini Uingereza ndani ya mwezi mmoja baada ya kutangazwa kwa marufuku ya pembe za ndovu kuanzishwa," anasema mtafiti Frankie Osuchi.

Ripoti inasema, ilikuwa ushahidi wa ongezeko la mahitaji ya pembe za ndovu kutoka kwa viboko, ambao idadi yao porini iko hatarini. Watafiti wanasema mtindo huu ulikuwa wazi tangu mwaka 1989, wakati marufuku ya kimataifa ya biashara ya pembe za ndovu ilikubaliwa kwa mara ya kwanza na imeongezeka huku serikali zikileta hatua mpya za kuimarisha marufuku hiyo.

Kama ilivyo pembe za ndovu, meno ya kiboko ambazo mara nyingi hutumiwa kwa michongo ya mapambo, bei yake ni nafuu na rahisi kupatikana.

Sehemu za mwili wa kiboko bado zinaweza kuuzwa chini ya Mkataba wa Biashara ya Kimataifa katika Viumbe vilivyo Hatarini Kutoweka (CITES), ingawa mauzo yote ya kimataifa yanahitaji kibali cha kuuza nje.

Imehesabiwa kuwa kati ya mwaka 1975, wakati rekodi za CITES zilianza, na 2017, kilo 770,000 za meno ya kiboko ziliuzwa



Kiboko akiwa ndani ya maji. **PICHA: MTANDAO.**

kisheria. Pia, kuna biashara haramu.

Mwaka 2020, meno ya kiboko yalikuwa kati ya sehemu za mwili wa mamalia ambazo mara nyingi hukamatwa katika EU, kulingana na ripoti ya Tume ya Ulaya.

"Kuna visa vya mbwa wanaonusa kubaini meno ya kiboko katika viwanja tofauti vya ndege barani Afrika siku hizi na kugunduliwa hakumaanishi kuwa wote wamekamatwa, labda ni nusu tu," anasema Philip Muruthy, Makamu wa Rais wa Shirika la Wanyamapori la Afrika.

Utafiti wa Muungano wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Mazingira (IUCN) mwaka 2016 ulikadiria kuwa idadi ya viboko duniani kote ilikuwa kati ya 115,000 na 130,000 - kushuka kwa asilimia 30 tangu 1994.

Nchi 10 za Afrika Magharibi na Kati zinasema kumeendelea kupungua kwa kasi kwa idadi ya wanyama hao, kutokana na ujangili na uharibifu wa ardhi. Walipendekeza kupigwa marufuku kabisa kwa biashara katika maandalizi ya mkutano wa CITES huko Panama mwezi uliopita, lakini ingewezekana tu chini ya sheria za CITES ikiwa kungekuwa na kupungua kwa zaidi ya asimilia 50% ya idadi ya viboko katika miaka 10 iliyopita. uchambuzi wa IUCN haukuunga mkono hitimisho hili.

Nchi 10 za Afrika Magharibi na Kati, zilipendekeza hatua inayoitwa "dokezo" ambayo ingesababisha upendeleo wa sifuri kwa vielelezo pori vinavyouzwa kwa madhumuni ya kibiashara. Ni pendekezo lisiloungwa mkono na Umoja wa Ulaya (EU) na nchi za Afrika Mashariki na Kusini, ambazo zinasema idadi ya viboko inasalia katika kiwango kizuri.

Baadhi ya nchi za Afrika Mashariki na Kusini; Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe zinatajwa ni chanzo cha robo tatu ya viboko wanaokadiriwa kufikia 13,909 ambao sehemu na bidhaa zao ziliuzwa kati ya 2009 na 2018.

Joanna Swabe, Mkurugenzi Mkuu wa Masuala ya Umma wa asasi ya Human Society Iternational, anadokeza kuwa kazi ndogo imefanywa tangu 2016 kuanzisha nambari za viboko.

"Kumekuwa na utafiti mdogo sana wa kisayansi juu ya idadi halisi ya viboko katika nchi hizi zote," anasema na kufafanua: "Wakati huohuo, nchi mbalimbali zinajua kinachoendelea na viboko hao ndani ya maeneo yao, hivyo haipaswi kupuuzwa."

Viboko wana kiwango cha chini cha kuzaliwa, huzaa mtoto mmoja tu kila mwaka, hivyo kupungua kwa idadi yao kunaweza kuwa na athari ya muda mrefu.

**UKWELI UNAOWAHUSU**

Viboko wengi wanaishi Afrika na kuna aina mbili ya viboko; wa kawaida ambao idadi yao inakadiriwa kuwa 115,000 hadi 130,000 mwaka wa 2016 na kiboko wanaofahamika kama 'pygmy' ambao wako 2,000 hadi 3,000.

Kiboko wa kawaida aliainishwa kuwa "katika hatari ya kutoweka" kwenye orodha ya wanyama wanaotoweka ya Muungano wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Mazingira (IUCN) mwaka wa 2016.

Sehemu na mazao ya viboko wanaokadiriwa kufikia 13,909 yaliuzwa kihalali kati ya 2009 na 2018 - robo tatu ya viboko hao walitoka Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe. Kunatajwa, kilo 770,000 za meno ya kiboko yaliuzwa kihalali kati ya mwaka 1975 na 2017 - ukubwa wa biashara hiyo haramu haujulikani.

Wataalamu wa wanyamapori wanasema, biashara halali na haramu ya meno ya kiboko inahitaji kufuatiliwa kwa karibu. Kiboko wa kawaida ameorodheshwa katika Kiambatisho II cha CITES kumaanisha kwamba anaweza kutishiwa kutoweka isipokuwa kama biashara itadhibitiwa kwa karibu.

Nchi 10 zinazotaka kupigwa marufuku duniani kote kwa noti ya biashara zinasema kwamba kuna ushahidi dhabiti wa "kuchanganya pembe za ndovu halali na haramu", ikipendekeza kuwa pembe za ndovu zilizowindwa "zinauzwa katika soko halali".

Wana kampeni wanaonya viboko wanaweza kushiriki hatima ya tembo, ambao wamekuwa hatarini - au walio katika hatari kubwa ya kutoweka kwa tembo katika misitu ya Afrika - kwa sababu wengi waliuawa na wawindaji haramu kwa ajili ya meno yao.


**Kwa mujibu wa BBC.**

## CHEMSHABONGO NA -00 35 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com


Dondoo: Kulia
1. Kinyume cha wewe
5. ami
7. Muskati ni mji wake mkuu
8. mpaka, hadi
9. Lugha aliyozungumza Yesu
12.dumu
13.kitu kisicho cha zamani
14.toa uhai wa kiumbe
16.Jiji la pili kwa Ukubwa Tanzania
17.Pengine, labda

Chini:
1. Mungu
2. kuwa madhubuti
3. mzazi wa kike
4. pindishwa mgongo huku uso ukielekea chini
6. Mke wa mfalme
10.kanya
11. hisani
14.uwazi mwembamba ukutani
15. Balaa




Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

PANYA
PUNDA
NYATA
AZANIA
UBWABWA
ZIBA
NYAMA
MANDELA
TANGA, WAA
AMANI, PETE
DAKWA, KWAA
AALI, MBEYA




maoni SMS: 0787 00 97 94





## Serikali yaonya upotoshaji wanaoondolewa hifadhini

**Na Mwandishi Wetu,** MBARALI

SERIKALI wilayani Mbarali mkoani Mbeya imewatahadharisha watu wanaowapotosha wananchi wa vijiji vinavyotakiwa kuondolewa ndani ya Hifadhi ya Taifa Ruaha wakiwataka kuendelea kukaa kwenye maeneo hayo kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alitoa tahadhari hiyo juzi, akibainisha kuwa kuna baadhi ya watu wanaojifanya wanasheria wanawashawishi wananchi waendelee kuishi kwenye maeneo wanayotakiwa kuondoka.

Alisema hivi karibuni jopo la mawaziri wanane wa kisekta lilitembelea maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo na kutoa utaratibu, hivyo wananchi wanatakiwa kuwasikiliza viongozi wa serikali na sio watu wengine.

Alisema baada ya maelekezo yaliyotolewa na mawaziri, kinachofuata ni uwekaji wa mipaka mipya ambayo itasaidia kuondoa mwingiliano wa shughuli za uhifadhi na shughuli za kibinadamu.

"Hatutasita kuchukua hatua za kisheria kwa wale watakaobainika kuwapotosha wananchi, ninawataka wananchi watusikilize sisi viongozi wao na sio hao wapotoshaji," alionya.

Mfune alisema kumekuwa na mgogoro wa mpaka kati ya wananchi na hifadhi tangu mwaka 2008 baada ya kutolewa kwa Tangazo la Serikali namba 28 ambalo lilikuwa linaainisha mipaka mipya ya hifadhi hiyo.

Serikali imetenga zaidi ya hekta 74,000 kwa ajili ya shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo na ufugaji kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya Mbarali wakiwamo watakaoondolewa kwenye vijiji vya kwenye hifadhi.

# Washtukia ukatili kwenye vituo vya malezi ya watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa makuzi na malezi ya watoto mkoani Mbeya, wameomba serikali kufuatilia utendaji wa vituo vya kulelea watoto, wakidai kuwa baadhi ya watoto walio kwenye vituo hivyo wanafanyiwa ukatili.

Waliwasilisha hoja hiyo jana wakati wa kikao cha tathmini ya makuzi na malezi ya watoto wenye umri wa kati ya miaka sifuri na minane mkoani Mbeya.

Mmoja wa wadau hao, Michael Malecela ambaye ni Kaimu Ofisa Elimu wa Wilaya ya Rungwe, alisema baadhi ya watoto wanaolelewa kwenye vituo hivyo wamekuwa wakinajisiwa, jambo ambalo linahatarisha usalama wa kundi hilo.

Alisema vitendo hivyo vinafanyika kutokana na baadhi ya walezi wa vituo hivyo kutokuwa na maadili ya kazi na hivyo akaiomba serikali kuchunguza kwa umakini ili kubaini wanaotekeleza unyama huo dhidi ya watoto.

"Wote ni mashahidi tumekuwa tukisikia taarifa nyingi za watoto kunajisiwa na kulawitiwa kwenye hivi vituo, sasa tuwaombe maofisa ustawi wa jamii watusaidie kukabiliana na matatizo haya," aliagiza Malecela.

Alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto vinasababisha matatizo mbalimbali ikiwamo watoto kuathirika kisaikolojia pamoja na matatizo mengine yakiwamo ya kiafya, hasa kupata magonjwa ya zinaa.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mkoa wa Mbeya, Aika Temu, alibainisha mkoa huo una vituo vya kulelea watoto zaidi ya 200 ambavyo vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria na vinafanya kazi.

Alisema wanapobaini kuwapo ukiukwaji wa maadili kwenye vituo hivyo, huwa wanachukua hatua kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja na kuvifungia vituo hivyo.

"Ni kweli vipo vituo ambavyo huwa vinakiuka sheria na vingine tumeshavichukulia hatua kwa kuvifungia, vingine tunaendelea kuvisajili na vingine tunavifuatilia ili tukijiridhisha tuvichukulie hatua endapo tutabaini ukiukwaji huo wa sheria," alisema Temu.

Aliwataka wamiliki wa vituo hivyo kufanya kazi kwa kufuata sheria ili kuepuka kukumbwa na mkono wa sheria, akisisitiza serikali inaendelea kufanya kazi yake kwa kushirikiana na wadau.

Mwakilishi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Leah Mwakasobe, aliwataka maofisa ustawi wa jamii walio kwenye halmashauri kujiridhisha kwanza na vigezo kabla ya kusajili vituo hivyo vya kulelea watoto.

Alisema wizara huwa inavisajili vituo hivyo kwa kutegemea mapendekezo ya maofisa ustawi wa jamii na hivyo akawataka kuwa makini kwa maelezo kuwa wakitoa maoni hayo wizara huwa haiwezi kubadili mtazamo.

Katibu Tawala Msaidizi Mipango wa Mkoa wa Mbeya, Emmanuel Kilundo, aliwataka wadau wote wanaotekeleza programu hiyo, kuhakikisha wanafanya kazi kwa kushirikiana ili kuhakikisha inatekelezwa kwa ufanisi.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akipanda mti katika Hospitali ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya ikiwa ni ishara ya kuhamasisha upandaji wa miti na utunzaji wa mazingira jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wafanyakazi halmashauri watoa msaada kituo cha kulea watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UMOJA wa wanawake wafanyakazi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya umetoa msaada wa vitu mbalimbali kwa watoto yatima wanaolelewa kwenye kituo cha kulelea watoto cha Nuru kilichoko Uyole jijini hapo.

Watumishi hao wametoa vyakula, vinywaji, nguo, mafuta na vitu mbalimbali kwa ajili ya malezi ya watoto hao ambao baadhi yao ni wachanga waliochukuliwa kwenye maeneo mbalimbali.

Msaada huo ulitolewa juzi ikiwa ni sehemu ya kuwafariji na kuwasaidia kusherehekea sikukuu za mwishoni mwa mwaka ambao ni utaratibu wa kila mwaka.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Triphoni Kisiga, alisema asilimia kubwa ya watoto hao hawana wazazi wa kuwafariji na hivyo wao waliamua kuchukua majukumu ya kuwafariji.

Aliwataka wananchi wengine wenye uwezo, kwenda kwenye vituo hivyo kwa ajili ya kuwafariji na kuwasaidia watoto hao ili na wao wajisikie kuwa sehemu ya wanajamii na washerehekee vizuri sikukuu za mwisho wa mwaka.

"Kipindi hiki cha sikukuu watoto wengi huwa wanatulia na wazazi wao lakini hawa waliopo hapa sisi ndiyo wazazi wao, kwa hiyo tulikubaliana sisi kama wanawake kuja kujumuika nao ili tuchukuwe nafasi ya wazazi wao," alisema Kisiga.

Meneja wa Kituo hicho, Mary Emily, alisema kituo hicho kina watoto 30 ambao wana umri tofauti, baadhi yao wanasoma sekondari na wengine ni wachanga.

Alisema kati ya watoto hao, watano ndiyo wanaosoma sekondari, tisa wanasoma shule za msingi na chekechea wako wanne ambao wote wana uhitaji wa vitu mbalimbali kwa ajili ya masomo.

Alisema watoto hao wanahitaji sare za shule, madaftari na baadhi yao ambao wana ulemavu, wanahitaji viti mwendo kwa ajili ya kuwasaidia kwenda shuleni na kurudi.

"Lakini tuna watoto wachanga ambao wanahitaji uji wa lishe, tunahitaji nguo za kuwasitiri, malezi ya watoto hawa ni magumu sana, hivyo tunahitaji sana misaada," alisema Mary.

Alisema mpaka sasa kituo hicho kina watoto wenye ulemavu wanne ambao kati yao wawili hawatembei na wawili hawaongei, hali ambayo inawapa ugumu kwenye malezi.

Aliwaomba wadau mbalimbali kuwasaidia kwenye malezi ya watoto hao ili kuwapunguzia mzigo ambao wanao hasa kwa watoto wachanga na wenye ulemavu.

Alisema katika kituo hicho baadhi ya watoto wamekuwa wakichukuliwa na watu mbalimbali kwa makubaliano ya kwenda kuwalea kama watoto wao lakini tatizo lipo kwa upande wa wenye ulemavu ambao wazazi wengi huwa hawako tayari kuwachukua.





# Serikali yatoa tahadhari ajali za barabarani nchini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Afya imewataka watumiaji wote wa vyombo vya moto barabarani katika kipindi hiki cha kuelekea sikukuu za mwishoni mwa mwaka na mwaka mpya kuchukua tahadhari ili kuepuka ajali zinazosababisha vifo, ulemavu wa kudumu na kuipa serikali mzigo mkubwa wa kutoa huduma kwa waathirika.

Imebainisha kuwa takriban theluthi mbili ya wagonjwa hao, hawana bima ya afya na hushindwa kulipia huduma waliyopata, hivyo serikali hubeba mzigo huo wa matibabu ambao ni mkubwa kutokana na gharama za matibabu.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi alipozuru kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kutembelea wodi za wagonjwa wa upasuaji ambapo zaidi ya asilimia 70 ni wagonjwa wa ajali.

Prof. Makubi aliwaagiza waganga wakuu wa mikoa nchini kushirikiana na Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani kuwapima madereva afya ya mwili na akili ili wanaogundulika kuwa na tatizo waende hospitalini kupata tiba stahiki.

"Shirikianeni kuendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya moto ili vile vitakavyobainika kuwa na hitilafu vizuiwe kutoa huduma kwani ajali zinapotokea kazi kubwa inahamia hospitalini," aliagiza Prof. Makubi.

Alisema takwimu kutoka Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) zinaonyesha katika kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka huu, wagonjwa wa ajali walikuwa 1,917 na kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka huu, wagonjwa wa ajali walikuwa 2,410, hivyo katika vipindi viwili hivyo asilimia 70 zilikuwa ajali za barabarani.

Alisema takwimu hizo kutoka hospitali moja tu zinaonyesha ongezeko la ajali 493.

"Gharama za kutibu wagonjwa wa ajali MOI waliopata mivunjiko ya mifupa mirefu (fracture) na kulazimika kufanyiwa upasuaji na kuwekewa vyuma (implants) hugharimu takribani Sh. milioni mbili ambapo wagonjwa waliopata ajali na kuumia kichwani hasa ubongo (Traumatic Brain Injury) na kulazimika kufanyiwa upasuaji, hugharimu Sh. milioni sita hadi milioni 20 kutokana na kuhitaji huduma ya ICU baada ya upasuaji na kukaa hospitalini kwa wastani wa siku 20," alifafanua.

Katika hatua nyingine, Prof. Makubi alieleza kuwa wizara imejipanga kuwa na magari ya kutosha ya dharura kwa wagonjwa ili ajali zinapotokea yatumike na tayari serikali imenunua magari zaidi ya 660 yatakayosambazwa nchi nzima na yanatarajiwa kufika nchini Juni 2023.

Kutokana na hatua hiyo, alisema wizara itakuwa na mfumo wa kufahamu gari la wagonjwa liko wapi ili ajali inapotokea gari hilo lifike mapema eneo la tukio kuchukua majeruhi kwa ajili ya matibabu zaidi.



Ofisa Elimu Mkoa wa Dodoma, Gift Kyando, akizungumza kwenye kikao kazi cha kuzungumzia maendeleo ya elimu katika mkoa huo kilichofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Bilioni 28/- zakusanywa mapato ya halmashauri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI nane za Mkoa wa Dodoma zimekusanya mapato ya ndani ya jumla ya Sh. biliini 28.443 sawa na asilimia 39 ya malengo ya kukusanya Sh. bilioni 72.718 kwa mwaka wa fedha wa 2022/23.

Kiasi hicho cha fedha kimekusanywa katika kipindi cha miezi mitano kuanzia Julai hadi Novemba mwaka huu.

Katibu Tawala Msaidizi - Mipango na Uratibu Mkoa wa Dodoma, Charles Mdume, alibainisha hayo jana alipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/23 hadi kufikia Novemba 2022 kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Alisema Halmashauri za Wilaya za Chamwino na Kongwa zimekusanya fedha za mapato ya ndani zaidi ya asilimia 42 ya lengo kwa miezi mitano.

"Kwa mwaka wa fedha wa 2022/23, Mkoa wa Dodoma na Halmashauri zake nane umeidhinishiwa bajeti ya Sh. bilioni 372.065 na katika kipindi cha Julai hadi Novemba mwaka huu. Mkoa umepokea na kukusanya Sh. bilioni 168.294 sawa na asilimia 45.

"Kwa upande wa miradi ya maendeleo, zimeidhinishwa Sh. bilioni 126.894 na kwa kipindi cha Julai hadi Novemba 2022, Mkoa umepokea Sh. bilioni 62.454 sawa na asilimia 49," alibainisha.

Kuhusu upelekaji wa asilimia 40 na asilimia 60 za mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo katika halmashauri, Mdume alisema halmashauri hizo nane zimepeleka Sh. bilioni 8.192 kati ya Sh. bilioni 31.231 zilizoidhinishwa kwa mwaka huu wa fedha.

Kuhusu upelekaji wa asilimia 10 ya mapato ya ndani kwenye vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, Mdume alisema halmashauri hizo nane zimepeleka Sh. milioni 509.927 sawa na asilimia 36 ya fedha zilizoidhinishwa kupelekwa Sh. bilioni 1.397.

Akizungumzia mafanikio, Mdume alisema serikali kuu imetoa Sh. bilioni 32.766 sawa na asilimia 83 ya bajeti ya mwaka 2022/23 katika utekelezaji miradi ya maendeleo.

Alisema serikali kuu pia imetoa Sh. bilioni 25.498 kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 49 katika Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Pia alisema serikali kuu imetoa fedha Sh. bilioni 80.342 kwa ajili ya kulipa mishahara sawa asilimia 42 katika Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa huku ikitoa Sh. bilioni 6.78 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 339 katika shule 127 za sekondari ambazo hazikuwapo kwenye bajeti ya mwaka 2022/23.

"Serikali Kuu pia imelipa fedha Sh. milioni 210.248 za malimbikizo ya mishahara kwa watumishi," alibainisha.

## Halmashauri zapongezwa utekelezaji mradi wa afya

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la World Vision Tanzania limezipongeza wilaya za Bahi na Chemba kwa kufanya vizuri katika utekelezaji wa Mradi wa Afya ya Mama na Mtoto uliotekelezwa kwa miaka mitano.

Akizungumza wakati akitoa tathmini ya mradi huo Meneja Mradi wa Afya ya Mama na Mtoto mkoani Dodoma, Daud Gambo, alisema wilaya hizo zimefanikiwa kupunguza kwa asilimia kubwa vifo vya mama na mtoto kutokana na kuzingatia maelekezo ziliyopewa na wataalamu wa afya.

Gambo alisema kuwa kabla ya mradi huo, mahudhurio ya kinamama kliniki yalikuwa chini lakini hivi sasa baada ya mradi wamekuwa wengi, wanahudhuria kliniki pamoja na kupeleka watoto kupata chanjo mbalimbali.

"Tunawashukuru Shirika la World Vision Tanzania kwa kuleta mradi huu kupitia wafadhili, wamesaidia sana kuokoa maisha ya kinamama," alisifu.

Gambo alisema hivi sasa wengi wao wamekuwa wataalamu wa kushauri wengine ambao ni wavivu kuhudhiria kliniki kwa ajili ya kupata maelekezo ya namna ya malezi ya mtoto pamoja na umuhimu wa kuhudhuria kliniki kwa ajili ya kupata matibabu mbalimbali.

Hata hivyo, aliwataka wananchi wa eneo hilo kuendelea na utaratibu huo pamoja na kuwa mradi huo unaelekea ukingoni.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Nelson Bukulu, alisema serikali haiwezi kushindwa kutekeleza mradi wowote unaoletwa nchini kwa manufaa ya wananchi.

Alisema hiyo ndiyo sababu wamekuwa wakitoa ushirikiano kwa wadau wanaoleta miradi ya maendeleo nchini.

Aliwapongeza World Vision Tanzania kutokana na kuleta mradi huo huku akiwaomba kuendelea kutafuta miradi mingine kwa ajili ya wananchi.

Alisema wakifanya hivyo, Watanzania watazidi kuelimika katika suala zima la masuala ya afya, hivyo kufanya jambo kubwa katika kupunguza vifo vya mama na mtoto kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Alisema suala la afya ni muhimu na ndiyo maana serikali inatoa kipaumbele kwenye sekta ya afya.



## ZAWA yaagizwa kumsimamisha kazi mkandarasi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, ameutaka uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kusimamisha kazi Kampuni ya Ms/ Sapphire Engineering pamoja na kufuta mkataba baada ya kuidanganya serikali kwa kuchelewesha kufikisha tangi la maji eneo la Raha Gando Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alitoa agizo hilo juzi katika kikao kazi cha kujadili maendeleo ya mamlaka hiyo kilichofanyika makao makuu ya ZAWA Malindi Zanzibar.

Hemed alisema kitendo cha kuidanganya mamlaka hiyo kuhusu kuchelewesha kufikisha tangi hilo ni kitendo cha kuonesha udhaifu wake katika kazi hizo na kuitaka mamlaka husika kuchukua hatua za kisheria.

Alisema serikali imetenga fedha nyingi kwa kuwafikishia huduma ya majisafi na salama wananchi kwa muda wote na kushangazwa kuona baadhi ya watu kwenda kinyume na juhudi hizo.

Hivyo aliitaka mamlaka hiyo kupitia mikataba ya usambazaji wa vifaa na kuwachukulia hatua za kisheria wasambazaji wote ambao hawaheshimu mikataba hiyo kwa manufaa yao binafsi.

Pia aliutaka uongozi wa mamlaka hiyo ya maji kuongeza uwajibikaji ili kuzidisha mapato na hatimaye kujiendesha pamoja na kufikia kutoa gawio kwa serikali.

Alisema: "Ili kuzidisha upatikanaji wa mapato ZAWA ni vyema mhakikishe kila mtumiaji wa maji anapata mita itakayoweza kusaidia kujua kiwango cha maji wanachokitumia."

**Hemed alisema kitendo cha kuidanganya mamlaka hiyo kuhusu kuchelewesha kufikisha tangi hilo ni kitendo cha kuonesha udhaifu wake katika kazi hizo na kuitaka mamlaka husika kuchukua hatua za kisheria.**

# Rais Mwinyi awataka wahitimu vyuo vikuu kufanya utafiti

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema shughuli za utafiti zipo nyuma ikilinganishwa na shughuli zingine, hivyo amewataka wahitimu wa elimu ya juu kufanya shughuli hiyo ili kulisaidia taifa.

Aliyasema hayo katika mahafali ya 20 ya Chuo Kikuu cha Zanzibar University (ZU) kilichoko Kibele Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kutokana na mabadiliko ya dunia, wasomi wana jukumu la kusaidia maendeleo ya taifa lao.

Rais Mwinyi alisema licha ya shughuli hiyo kuwa inahitaji gharama ya kifedha lakini lazima wasomi kufanya utafiti na shughuli za ushauri.

Alisema mambo hayo yatawaongezea maarifa zaidi ya kitaaluma na kuwawezesha kupanda vyeo sambamba na kusaidia kutatua matatizo mbalimbali ndani ya jamii inayowazunguka.

Rais Mwinyi alisema inapendeza zaidi kuona wataalamu wa ndani ya nchi wanashiriki katika utafiti mbalimbali na kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayoikabili nchi.

Pia aliwataka wahitimu hao watambuwe kuwa kiwango cha taaluma walichofikia wanakifanyia kazi kwa sababu nchi inahitaji kizazi kipya cha wasomi wenye upeo na uthubutu wa kutatua matatizo yaliyokuwapo katika ngazi mbalimbali ya jamii.

Alisema serikali inahitaji aina mpya ya wasomi wanaojituma wenye ubunifu na wasiosubiri kuhimizwa.

Kuhusu sekta ya elimu Rais Mwinyi alisema elimu itaendelea kubaki kuwa nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo siyo kwa jamii ya Zanzibar pekee bali ni kwa dunia nzima.

"Elimu ni moja ya ajenda zilizopewa kipaumbele katika ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025 kwa lengo la kuchochea kasi ya maendeleo ya watu wetu kwani ni vigumu kufikia maendeleo yaliyokusudiwa bila ya kuwa na watu wenye elimu bora," alisema.

Aidha, alikipongeza chuo hicho kwa kuanzisha kozi ya shahada ya sayansi katika afya ya jamii na kuahidi kwamba serikali itahakikisha inawaunga mkono kufanikisha malengo yao katika kozi hiyo kwa ufanisi mkubwa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohammed Mussa, alisema pamoja na serikali kuwekeza katika dhana ya uchumi wa buluu lakini bado kuna upungufu wa wataalamu katika nyanja hizo.

Hivyo alitumia fursa hiyo kuviomba vyuo vilivyokuwapo Zanzibar kuanzisha programu ambazo zinaendana na mahitaji ya soko ya sera ya uchumi wa buluu ili kuunga mkono juhudi za serikali katika kupata wataalamu ambao watawezesha mafanikio makubwa ya Dira ya Maendeleo ya mwaka 2050.

Mkuu wa Chuo hicho, Mhandisi Dk. Abdulqadir Othman Hafiz, alisema matarajio yao chuo hicho kusifika kwa kutoa elimu bora ndani na nje ya nchi.

Jumla ya wanafunzi 568 wakiwamo wanaume 251 na wanawake 317 wamehitimu masomo katika ngazi ya cheti, stashahada na shahada ya kwanza.



Kisiwa cha Chumbe ambacho Desemba 16, mwaka huu, kimepata tuzo ya kifahari ya kimataifa kwa usanifu wake wa mazingira, utalii na usimamizi wa uhifadhi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kisiwa cha Chumbe chapewa tuzo ya kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

KISIWA cha Chumbe kimepokea tuzo ya kifahari ya kimataifa kwa usanifu wake wa mazingira na utalii wenye kaboni kidogo na usimamizi wa uhifadhi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kisiwani humo, kuhusu tunzo hiyo, Meneja Msaidizi wa Uhifadhi na Elimu wa Kisiwa cha Chumbe, Salim Abdallah, alisema tuzo hiyo ni muhimu, siyo tu kwa Chumbe lakini kwa Zanzibar kama kikomo cha safari.


Alisema tunzo hiyo imeonyesha kiwango cha kimataifa mfano athari za chini za utalii kama Chumbe imeongoza njia katika kuelekea kufikia mfumo wa utalii ambao haupunguzi tu athari zake, bali inachangia kikamilifu katika kuunda upya nafasi za asili na kanuni za msingi za uchumi wa buluu. "Jukwaa la kimataifa lilisema kwamba ikoloji ya Kisiwa cha Chumbe imetoa mafanikio madhubuti na muundo unganisha wa mazingira na uhifadhi wa bioanuwai na utalii endelevu wa kiikolojia,"alisema.

Alisema Kisiwa cha Chumbe kimekuwa kikifanya ufuatiliaji programu kwa ajili ya bioanuwai kisiwani, ambayo ni muhimu katika kuongoza uwajibikaji wa shughuli za kitalii na kudumisha uadilifu na utofauti wa ikolojia.

Jukwaa la Kimataifa la Makazi ya Binadamu, kwa kushauriana na Umoja wa Mataifa wa Kiuchumi na Kijamii Halmashauri, imekitambua Kisiwa cha Chumbe kuwa muhimu duniani chini ya kipengele cha "utalii (Scenic spot) na urejesho wa kiikolojia".

Katika taarifa kutoka jukwaa la kimataifa, Chumbe ilieleza kuwa ni mfano wa kuigwa ulimwenguni na miongo miwili na nusu ya kuchangia katika uhifadhi wa asili na viumbe vya baharini."

Ilieleza kulingana na jukwaa hilo adhimu, Chumbe imeweka uhifadhi, elimu na uendelevu katika msingi wa usimamizi na uendeshaji" na imepata "maendeleo yasio na kifani kwa kuweka mlolongo wa kaboni ya chini na kijani anzilishi, kama vile nishati ya jua, matumizi ya maji ya mvua, taka kutengeneza mboji, na ushirikishwaji wa jamii".



# Wawili jela miaka 20 kwa kukutwa na meno ya tembo

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WAKAZI wawili wa Kijiji cha Wachawaseme Wilaya ya Mlele waliokuwa wakituhumiwa kwa kukutwa na meno manne ya tembo pamoja na bunduki mbili wamehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 20 jela kila mmoja.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mkoa wa Tabora, Jovith Kato kwa watuhumiwa wawili ambao ni Baliwe Benjamin (32) na Shaban Petro (31).

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kato alisema ametoa adhabu hiyo ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye dhamira ya kutumia vibaya rasilimali za taifa bila kufuata utaratibu.

Katika kesi hiyo upande wa mashtaka uliongozwa na Wakili wa Serikali, Alice Thomas, uliiambia mahakama hiyo kuwa washtakiwa walitenda kosa hilo Mei 2, mwaka 2021.

Wakili Thomas aliiomba mahakama hiyo itoe adhabu kali kwa washtakiwa kwani vitendo vya kuua wanyamapori kwa tamaa ya kujipatia fedha nyingi haviwezi kufumbiwa macho.

Aliongeza kuwa wanyama ni rasilimali ambayo inaliingizia taifa fedha za kigeni kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa uchumi wa nchi na kwamba kosa hilo ni hatari kwa uhifadhi wa rasilimali nchini.

Wakili Thomas pia aliiomba mahakama itaifishe silaha hizo ili zisiwafikie wahalifu wengine ambao wanaweza kuzitumia kuwadhuru wananchi.

Washtakiwa hao wakijitetea waliomba mahakama iwaonee huruma kwa vile wanafamilia zinazowategemea.



Mkurugenzi wa Shirika la OPE, Wiliam Shayo, akiongoza zoezi la upandaji miti katika Shule ya Msingi Ng'hama Kata ya Mwalukwa wilayani Shinyanga jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Waziri Ummy aunda timu kuchunguza ujenzi hospitali

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameunda timu itakayoongozwa na Jaji mstaafu, Thomas Mihayo, kuchunguza ubadhirifu katika mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Ukerewe mkoani Mwanza.

Ummy aliunda timu hiyo juzi alipotembelea mradi huo wilayani Ukerewe wakati wa ziara yake kwa ajili kukagua na kuchunguza mwenendo wa ujenzi wa mradi huo.

Waziri Ummy alifanya ziara hiyo baada ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kutembelea wilayani humo Novemba 25, mwaka huu na kumtaka afike kukagua mwenendo wa ujenzi huo.

Akizungumzia mradi huo jana, Ummy alisema wamepokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu kutoridhishwa na gharama za ujenzi huo.

Alieleza kuwa hajashawishika na ujenzi huo kwani lengo ni wananchi wa eneo hilo kupata huduma za kibingwa katika Hospitali ya Sekou Toure au Bugando.

Alisema shida imeanzia kwenye ujenzi wa majengo na hiyo itasababisha kukosa madaktari bingwa baada ya kumalizika.

"Niwakumbushe kuwa, alichotaka Waziri Mkuu tangu mwanzo ni kwamba wananchi wa Ukerewe wasisafiri tena kwenda mbali na ndiyo maana tukaamua kujenga Hospitali ya Rufani ya Mkoa," alisema.

Alisema yupo kwenye sekta ya afya kwa miaka sita na wamejenga majengo mengi kama hayo na kwamba anashangaa wao kujenga jengo baya.

"Kwa macho yangu siyo kama mtaalamu binafsi nilipoona majengo haya hayaendani na gharama iliyowekezwa, nimekuwa Waziri wa Afya kwa miaka sita tumejenga vituo vya afya vya Sh. milioni 400 majengo saba.

"Naunda timu yangu ya tatu ambayo itakuwa na watu watano itanipa taarifa ya mwisho ikiongozwa na Jaji Mstaafu Thomas Mihayo," alisema Ummy.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alisema kumekuwa na makosa ya ujenzi tangu hatua za awali za utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa, alisema kulingana na hali ilivyo na idadi ya watu walichokilenga ni huduma zote za kibingwa ziwepo.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Dk. Getera Nyangi, alisema mwaka jana walikaa kikao kupanga namna ya kutekeleza mradi na walipendekeza kujengewa majengo ya ghorofa, lakini walipoambiwa kuwa haiwezekani kutokana na ufinyu wa rasilimali fedha waliamua wajenge majengo 11 ya chini.

## Wakulima, wafanyabiashara walia uhaba pembejeo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa mazao ya chakula na biashara mkoani Shinyanga, wamewaomba wasambazaji wa pembejeo za ruzuku kufika katika maeneo ya vijijini ili kuwapunguzia umbali wa kuzifuata mjini.

Walitoa ombi hilo jana kwa nyakati tofauti wakati wa ziara ya Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Hamisi Majogoro, akikagua maendeleo ya ugawaji pembejeo.

Lengo la ziara hiyo ni kuhakikisha kila mkulima aliyejiandikisha na kupata namba anapata pembejeo hizo.

moja wa wakulima kutoka Kata ya Kinamapula Halmashauri ya Ushetu, Neuster Paul, alisema wanalazimika kusafiri umbali wa kilometa 50 kutafuta pembejeo katika maduka wakati wasambazaji wana uwezo wa kuwafikia katika kata zao na kuwauzia kwa bei elekezi iliyopangwa na serikali.

Alisema mfuko mmoja wa pembejeo wanaununua kwa Sh.70,000 badala ya Sh.140,000, lakini gharama wanazozitumia kutoka kijijini hadi mjini na kurudi ni zaidi ya kiasi hicho.

Mkulima mwingine, Metherius Anthony wa Kata ya Mirambo Wilaya ya Kaliuwa alisema, anasafiri kilometa 300 kutafuta pembejeo baada ya Mkoa wa Tabora kutokuwa na pembejeo.

"Pembejeo hizi zimekuwa adimu sana na kila mkulima anahitaji, mkoa wetu wa Tabora madukani zimekwisha kabisa hali inayosababisha sisi kufika Kahama kuchukua pembejeo na kwenda kunusuru mazao yetu shambani yasinyauke kwa kukosa mbolea," alisema Anthony.

Mmoja wa wasambazaji wa ruzuku Mjini Kahama, Paul Mathias, alisema baadhi ya wakulima wanakuja na namba za usajili ambazo hazisomi katika mifumo yao na wakati mwingine zinaweza kusoma ila kitambulisho alichonacho siyo cha kwake hali inayowapa mashaka ya kuwapatia mbolea.

Alisema tangu kuanza kwa ugawaji wa mbolea, wametoa tani 300 katika Kata ya Kagongwa mkoani Shinyanga na Wilaya ya Mbongwe mkoani Geita.

Mwenyekiti wa KACU, Hamisi Majogoro, alisema pembejeo zipo za kutosha na ili kuwaondolea adha wakulima kusafiri umbali mrefu, atahakikisha anazifikisha AMCOS vilivyopo nchini ili wakulima waweze kuzipata.

Alisema msimu huu KACU inatarajia kuzalisha kilo milioni 17 za tumbaku kulinganisha na msimu uliopita.

# HABARI PICHANI



Watoto ambao majina yao hayakupatikana, wakinawa na kufua viatu kwa kutumia maji machafu yaliyotuama eneo la Nyerere Square, jijini Dodoma kama walivyokutwa jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Wananchi wakikwepa kupitia kwenye daraja la kuvukia na kujaribu kupitia chini ya vyuma hali inayoweza kuhatarisha maisha yao katika eneo la Mbezi Mwisho, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Xavier Daudi (katikati), akifurahia jambo wakati akiagana na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ramadhani Kailima (kulia), baada ya kufunga mafunzo ya kuwajengea uwezo kiutendaji maofisa tafara yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa Informatics, Chuo Kikuu cha Dodoma. Kushoto ni Mkurugenzi Idara ya Uendelezaji Rasilimaliwatu Ofisi ya Rais – UTUMISHI, Dk. Edith Rwiza. **PICHA: MPIGAPICHA**



Baadhi ya waongoza watalii Mlima Kilimanjaro kutoka Kampuni ya Utalii ya ZARA Tanzania Adventures, wakiongozwa na Faustine Chombo (katikati), wakifurahia jambo katika eneo la Shira wakati wa safari yao ya kurudi kutoka kilele cha Uhuru, juzi. **PICHA: JAMES LANKA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OMEGA MENAS MNALI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 183 BNX – TOYOTA HILUX.** Chassis namba **JT133LNA409049994.** Engine namba **2L4239019.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MTW/MTW/RB/474364/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na……70/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: FRANK RAPHAEL KIMOLETA WA MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA:WITNESS RAPHAEL KIMOLETA**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 27 Mwezi 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 22 mwezi 12 mwaka 2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA
MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na……69/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: AISHA M. MSOMPA WA DODOMA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: ALLY MOHAMED MSOMPA**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 27 Mwezi 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 20 mwezi 12 mwaka 2022

Imetolewa leo tarehe 20 Mwezi 12 Mwaka 2022

MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA
HAKIMU

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**

**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO….19….OF 2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ELIWAJA GIDION KINDURI**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETER OF ADMINISTRATION**
**BY ELIKUNDA YOHANA MAZINDE**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be field on or before the 17 day of January 2023

Dated at Korogwe this 16 day of December 2022

DISTRICT COURT
KOROGWE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

---

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 140 OF 2022**

**In Matter of the Estate of the Late**
**OSCAR ENDENI MSANGI**

**By 1. LETISIA SIMON**
**2. ………………………………**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grand should be field on or before the **04TH** day of **January / 2023.**

Dated at **Morogoro**, this **07th** day of **DECEMBER 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

---


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**



**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# DIAMOND

## AONYESHA UPENDO KWA ZARI

BOSI wa WCB, Diamond Platnumz, kwa mara nyingine ameonyesha upendo mkubwa kwa mzazi mwenzake, Zari Hassan.

Jumatano, Diamond alitumia ukurasa wake wa Instagram wenye wafuasi zaidi ya milioni 15.5 kutangaza shoo ya 'Zari The Boss Lady All White Party' ambayo imeratibiwa kufanyika leo Alhamisi usiku.

Diamond alichapisha bango la tangazo la shoo hiyo na kuwahimiza Waganda kujitokeza kwa wingi .

Shoo hiyo itafanyika katika Jiji Kuu la Uganda, Kampala na mdhamini mkuu ni Belaire.

Tiketi zinauzwa kutoka shilingi 75,000 za Uganda hadi milioni nne.

Zari na mpenzi wake wa sasa, Shakib Cham Lutaaya, wamekuwa wakiitangaza sana shoo hiyo ambayo wanatarajiwa kuandaa pamoja.

Diamond pia ameandaa shoo kubwa ya kufunga mwaka pamoja na msanii wake, Zuchu ambayo itafanyika siku ya mkesha wa mwaka mpya.

Hivi majuzi kumekuwa na tetesi kuwa mastaa hao wa Bongo ambao wanadaiwa kuwa wapenzi wanapanga kufunga pingu za maisha siku hiyo.

Mwishoni mwa Novemba, Zari alikuwa amedokeza kwamba atakuwa nchini Tanzania katika msimu wa Krismasi.

## MOBETTO ALIKOROGA



HATUA ya Hamisa Mobetto kukiri mahaba mazito kwa mshambuliaji matata wa Ufaransa, Kylian Mbappe, huenda imeibua matatizo katika penzi lake.

Jumatatu, mama huyo wa watoto wawili alidokeza kuwa anavutiwa na Mbappe na kudai kwamba anajifunza Kifaransa kwa ajili yake.

"À se damner (Nakukufia)," aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Najifunza Kifaransa kwa ajili ya #mbappe," alieleza.

Mpenzi huyo wa zamani wa staa wa Bongo, Diamond Platnumz na ambaye ni mzazi mwenza wake, aliambatanisha ujumbe huo na picha yake nzuri inayoonyesha akiwa ameshika tumbo lake huku akionekana mwenye mawazo.

Baadaye Jumanne, mwanamitindo huyo aliandika jambo lililoonyesha kuwa kwenye mgogoro wa mapenzi baada ya kukiri kumpenda Mbappe.

"Mume wangu kipenzi nywele zimefumuka kesho nataka kwenda kusuka naomba hela," mwanadada mmoja alimwandikia ujumbe mwanaume aliyemuita mumewe kwenye mtandao wa WhatsApp.

Katika maelezo yake, Mobetto aliweka wazi kuwa hali si shwari kwake.

## SAUTI SOL WAOMBA RADHI



WASIMAMIZI wa Bendi ya Sauti Sol na Sol Fest, wamejitokeza kuomba radhi mashabiki kufuatia ghasia za umma kuhusu uchezaji wao wa muda mfupi katika toleo la pili la mwaka huu, huku wakiahidi "wakati mwingine bora zaidi."

Tamasha la kila mwaka, ambalo Sauti Sol na Sol Generation huburudisha mashabiki, lilifanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Kenyatta (KICC) jioni ya Desemba 17, mwaka huu.

Washiriki wa tamasha walielezea masikitiko yao mtandaoni wakilaumu kwamba kundi hilo la nne, likiwa tendo kuu la usiku huo, lilipoteza muda wao jukwaani.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari, timu hiyo ilitetea matokeo hayo, ikisema kuwa lengo lao lilikuwa kutoa muda wa kutosha kwa kila mchezaji.

"Nia yetu ilikuwa kufanya tukio la kuvutia, kuhakikisha kila msanii na kikundi kinapata muda wa kutosha ili kutoa maonyesho yao bora zaidi kwa mashabiki wote.

"Pia tuliangazia zaidi talanta za ndani ambao walikuwa wakiigiza na wageni wetu wa kimataifa. Tunakubali kwamba hii inaweza kuwa ilisababisha kucheleweshwa kwa onyesho kwa wakati ufaao na tungependa kuwahakikishia mashabiki na wafuasi wetu kwamba tutajipanga vema zaidi katika siku zijazo," walisema.

Baada ya usiku mrefu wa matarajio yasiyoisha, wavulana wa usiku, vizuizi vya shoo, Sauti Sol, walipanda jukwaani saa tisa usiku.

# NYOTA WAPYA SINGIDA BIG STARS KUTAMBULISHWA MAPINDUZI CUP

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Singida Big Stars umeweka wazi kuwa nyota wao wapya waliowasajili kipindi cha dirisha dogo wataanza kuonekana rasmi katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar.

Singida Big Stars katika michuano hiyo ya Mapinduzi wako Kundi B, pamoja na timu ya Yanga na KMKM ya visiwani Zanzibar huku wakitarajia kufungua pazia dhidi ya KMKM Januari 2, mwakani.

Nyota wapya ambao wako katika rada na kuhusishwa na usajili ndani ya kikosi cha timu hiyo ni aliyewahi kuwa Mshambuliaji wa Al Masry ya Misri, Francy Kazadi, ambaye ni raia wa DR Congo.

Wengine ni Ennock Atta Agyei, ambaye aliwahi kucheza soka nchini akitumikia kikosi cha matajiri wa Chamazi na Ibrahim Ajib kutoka Azam FC ambao wameachana naye rasmi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Singida Big Stars, Hassan Massanza, alisema benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Hans van Pluijm, limekabidhi ripoti na mapendekezo ya usajili yamefanyiwa kazi.

Alisema mchakato wa usajili unaendelea na tayari wameshaanza kusajili baadhi ya wachezaji ambao wataonekana na kutambulishwa rasmi kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi Januari mwakani, visiwani Zanzibar.

"Tumefanya usajili mzuri kulingana na mapendekezo ya benchi la ufundi na tunatarajia wachezaji hao kuonekana rasmi katika mashindano ya Mapinduzi kwa kupata nafasi ya kucheza," alisema Massanza.




Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya NBC, Elvis Ndunguru (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya shilingi milioni moja pamoja na tuzo kwa mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, baada ya kutangazwa Mchezaji Bora wa Ligi Kuu ya Soka ya Tanzania Bara kwa mwezi wa Novemba. Anayeshuhudia kulia ni Mjumbe wa Bodi ya Ligi, Azim Khan, mapema kabla ya mchezo wa ligi hiyo kati ya Yanga na Coastal Union kuanza katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Jumanne wiki hii. **MPIGAPICHA WETU**

# Mayele ajazwa noti NBC

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), ambayo ni mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu ya Soka ya Tanzania Bara, NBC Premier League, imekabidhi zawadi ya pesa na tuzo kwa Mchezaji Bora wa ligi hiyo wa Novemba, Fiston Mayele, kutoka Klabu ya Yanga.

Makabidhiano ya zawadi hizo yalifanyika muda mfupi kabla ya kuanza kwa mchezo kati ya Yanga na Coastal Union uliofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumanne wiki, mchezo ambao ulikamilika kwa timu yao kuibuka na ushindi wa mabao 3-0.

Mabao ya Yanga katika mchezo huo mawili yalifungwa na Mayele na la tatu likizamishwa nyavuni na Feisal Salum 'Fei Toto'.

Katika tukio la makabidhiano ya zawadi hizo, lilishuhudiwa na Mjumbe wa Bodi ya Ligi, Azim Khan, ambapo Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya NBC, Elvis Ndunguru, alikabidhi hundi yenye thamani ya shilingi milioni moja kwa mchezaji huyo wa Yanga pamoja na tuzo

Akizungumza baada ya kukabidhi zawadi hizo, Ndunguru alisema NBC itaendelea kutoa hamasa kwa wachezaji na makocha kwa kila mwezi ili kuleta ushindani kwa wachezaji na makocha wote wanaoshiriki ligi hiyo.

"Tuzo hizi za kila mwezi tunazitoa kwa kuleta hamasa kwa wachezaji na makocha wa kila timu zinazoshiriki Ligi Kuu ili wafanye vizuri na kujitangaza kimataifa, pia kusaidia kuboresha mchezo huu wa soka hapa nchini," alisema Nduguru.

Pia, akifafanua zaidi mipango ya

benki hiyo, alisema ni kuboresha udhamini wake ambapo wapo katika hatua za mwisho kuanza kutoa mikopo ya mabasi kwa klabu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu ili kuzirahisishia usafiri.

"Pia, NBC tunaendelea kudhamini michezo mingine zaidi hapa nchini kama riadha kupitia NBC Dodoma Marathon na mashindano ya mchezo wa gofu tukidhamini Klabu ya Lugalo , lengo letu ni kusaidia sekta ya michezo nchini kuwa na kiwango cha kimataifa na pia kuboresha maslahi ya wanamichezo kwa ujumla."

Kwa upande wa Mayele, alishukuru kupatatuzo hiyo na kuahidi kuwa atazidi kuongeza bidii kuwa kinara katika timu yake na kusaidia kupata ushindi kila mechi.

"Napenda kuwashukuru NBC kwa kutoa tuzo hii, inaongeza sana hamasa kwa upande wangu na wa wachezaji wote na makocha pia, nawashukuru benchi la ufundi na wachezaji wenzangu kwa pamoja wameniwezesha kupata tuzo hii na nitazidi kufanya vizuri," alisema.

## Mpole atoa somo wachezaji Bongo

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

STRAIKA za zamani wa Geita Gold ambaye kwa sasa amejiunga na Klabu ya FC Saint Eloi Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, George Mpole, amewataka wachezaji wa Kitanzania kuchangamkia fursa kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi kwa ajili ya manufaa ya Timu ya Tanzania, Taifa Stars baadaye.

Akizungumza jana, Mpole ambaye alikuwa mshindi wa Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu msimu uliopita, alisema wachezaji wengi wa Tanzania wana uwezo wa kucheza soka la kulipwa nje, lakini tatizo inakuwa ni dhamira, hivyo kuwataka kutumia fursa hiyo pale wanapoipata kama alivyofanya yeye.

"Kucheza FC Lupopo kwangu ni fursa, kucheza nje ya nchi siyo kila mtu au kila mchezaji anapata nafasi hiyo, na hii imekuwa ni kama ndoto ya wachezaji wengi nchini, ni kitu ambacho tunachokihitaji ili tupate timu ya taifa bora, hatuwezi kupata timu bora ya taifa kama wachezaji wengi wataendelea kubaki ndani.

"Nawasihi wachezaji wenzangu watumie fursa kama hizi zikipatikana kwa sababu uwezo wa kucheza nje ya nchi wanao, tatizo ni dhamira tu, kwa hiyo naamini fursa hii niliyoipata kwangu itaniongezea vitu vingi kwenye maisha yangu ya soka.

Nawashukuru watu wote wa Geita na Klabu ya Geita Gold, Wanamichezo na Watanzania wote kwa sapoti yao kwangu, naahidi sitowaangusha Watanzania, naenda kufanya kazi, naenda kuongeza namba ya Watanzania wanaocheza soka la kulipwa," alisema mchezaji huyo.

Mchezaji huyo alijiunga na timu hiyo ambayo imetinga hatua ya makundi Kombe la Shirikisho barani Afrika, baada ya kuvunja mkataba na timu ya Geita Gold hivi karibuni ambapo klabu kubwa za Simba, Yanga na Azam zilikuwa zikihusishwa kumchukua kipindi hiki cha dirisha dogo, kabla ya kuibukia kwenye klabu hiyo.

Mpole ambaye alimaliza ligi msimu uliopita akiwa na mabao 17 juu ya Mkongomani Fiston Mayele wa Yanga, hakuwa na msimu mzuri msimu huu hasa baada ya kushindwa kusajiliwa na timu yoyote baada ya msimu uliopita kumalizika, ambapo ilisemekana klabu mbalimbali zilimtaka, lakini klabu yake ilikuwa inakataa ofa kitu ambacho kilimkasirisha na kuonekana kama ana mgomo baridi.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MBAPPE KUUZWA KIANGAZI**
PSG haitamruhusu mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe (24), kuondoka Januari kwani inapania kumuuza msimu wa majira ya joto kwa bei inayofaa. ***(Ben Jacobs, Twitter)***

**JOÃO AWEKWA SOKONI**
KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, amechochea mazungumzo kwamba mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix, mwenye miaka 23, anauzwa kwa kusema "hakuna mtu wa muhimu" katika klabu hiyo. ***(Goal)***

**MARTINEZ NA ARSENAL**
KLABU ya Arsenal ilimtaka mlinzi wa Argentina, Lisandro Martinez, msimu wa majira ya joto, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, aliamua kungana na kocha wa zamani wa Ajax, Erik ten Hag, katika Klabu ya Manchester United. ***(VI via Manchester Evening News)***

**MESSI NA MKATABA PSG**
MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi, amekubali mkataba wake na Klabu ya Paris St-Germain kuongezwa kwa mwaka mmoja katika hatua ambayo itamfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, kusalia na mabingwa hao wa Ufaransa hadi majira ya joto 2024. ***(Le Parisiea)***

**SANTOS ANUKIA CHELSEA**
KLABU ya Chelsea inakaribia kufikia makubaliano ya kumnunua kiungo wa kati wa Vasco da Gama raia wa Brazil, Andrey Santos, mwenye umri wa miaka 18. ***(Fabrizio Romano)***

**UNITED YAMTAKA EMILIANO**
KLABU ya Manchester United ina nia ya kumsajili mlinda mlango wa Aston Villa, Emiliano Martinez, mwenye miaka 30, ambaye alichangia kuisaidia Argentina kushinda Kombe la Dunia. ***(Football Insider)***


**RONALDO NA WAARABU**
OFA ya Al-Nassr ya mkataba wa pauni milioni 160 kwa mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo, mwenye umri miaka 37, inaungwa mkono na Serikali ya Saudi Arabia. ***(Ben Jacobs via Express)***

**FRANKFURT YAANIKA UKWELI**
KLABU ya Eintracht Frankfurt ya Ujerumani imedai kuwa ilipewa nafasi ya kumsajili Cristiano Ronaldo na Manchester United kabla ya kuondoka Old Trafford. ***(DAZN, via Mail)***

**BUSQUETS ASHAWISHIWA**
KOCHA wa Barcelona, Xavi, amemshawishi nahodha wake, kiungo wa kati wa Hispania, Sergio Busquets, mwenye umri wa miaka 34, kusalia katika klabu hiyo hadi msimu wa majira ya joto, badala ya kushinikiza kuhama Januari. ***(Sport)***



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SURA YA MESSI KUWEKWA KWENYE NOTI ARGENTINA

**Nyuma ya noti hiyo itaandikwa 'La Scaloneta' ambalo ni jina la utani la kocha mkuu wao...**

**BUENOS AIRES, Argentina**

ARGENTINA inafikiria kuweka sura ya mshambuliaji Lionel Messi kwenye noti za nchi hiyo baada ya mshindi huyo mara 7 wa Ballon d'or kuiongoza Argentina kutwaa Kombe la Dunia 2022.

Kwa mujibu wa gazeti la El Financiero, maofisa wa bodi ya usimamizi wa fedha nchini humo wanatafuta njia za kuuenzi ushindi wa kihistoria wa Kombe la Dunia wa taifa hilo.

Kuweka picha yenye sura ya Messi akiwa na Kombe la Dunia kwenye noti za nchi hiyo inatajwa kuwa chaguo bora zaidi kwani tarakimu huanza na '10' ambayo ni namba ya jezi inayovaliwa na nyota huyo.

Nyuma ya noti hiyo imependekezwa kuwa 'La Scaloneta' ambalo ni jina la utani la Kocha wa Argentina, Lionel Scaloni.

Hii itakuwa na lengo la kuheshimu mafanikio ya kocha huyo aliyeiongoza timu ya taifa hilo kushinda Copa America 2021, Finalissima dhidi ya mabingwa wa Euros, Italia na ushindi wa Kombe la Dunia 2022 dhidi ya Ufaransa nchini Qatar.

Benki Kuu ya Argentina ilianzisha sarafu za kibiashara kuadhimisha ushindi wa kwanza wa Kombe la Dunia mnamo mwaka 1978.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,059,8

MECHI KALI
EL DAKLYEH
VERSUS
PYRAMIDS
1 | 7.77
X | 3.73
2 | 1.47

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BLATTER AMSHUTUMU INFANTINO



**NYON, Uswisi**

RAIS wa zamani wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), Sepp Blatter, amemshutumu mrithi wake, Gianni Infantino, kwa kukosa heshima, huku akipinga mipango ya kupanua Kombe la Dunia.

Toleo la Qatar 2022 la Shindano Kuu la Kandanda, ndilo la mwisho kuwa na muundo wake wa sasa wa timu 32, huku mataifa 48 yakitarajiwa kushiriki katika michuano ya 2026.

Infantino amekuwa akishinikiza kupanuka tangu alipochukua nafasi ya Blatter kama Mkuu wa FIFA na amechunguza kuhamisha Kombe la Dunia hadi mzunguko wa miaka miwili au mitatu.

Lakini mtangulizi wake anadokeza kuwa hafanyii kwa maslahi ya mchezo huo.

"Kinachofanyika kwa sasa ni biashara ya kupindukia ya mchezo," alisema Blatter akinukuliwa na gazeti la Ujerumani la Die Ziet.

"(Angalia) Kombe la Dunia lenye timu 48, au Kombe la Dunia la klabu ambalo lazima lionekane kama ushindani kwa UEFA, FIFA inaingilia jambo ambalo haliwahusu.

"Sina uhusiano na Infantino. Alikosa heshima kwa sababu amekataa mawasiliano yoyote nami tangu kuchaguliwa kwake. Anawasiliana nami tu kupitia mawakili."

# Barca: Ubingwa LaLiga muhimu

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Klabu ya Barcelona, Joan Laporta, amesema wakishinda taji la Ligi Kuu nchini Hispania maarufu kama LaLiga, itaonyesha wameanza kurejesha ubora wao.

Barcelona imekua ikipitia kipindi kigumu kwenye suala la kiuchumi na matokeo mabaya kiwanjani kwa miaka ya karibuni ambayo imekua ikiiweka klabu hiyo kwenye wakati mgumu sana.

Barcelona ilishinda taji la LaLiga mara ya mwisho msimu wa mwaka 2018/19, huku wakitolewa mara mbili



kwenye hatua ya makundi kwenye Ligi ya Mabingwai Ulaya taji ambalo wameshinda mwaka 2015.

Rais Laporta anasema lengo kubwa msimu huu ni kushinda taji la La Liga na kuongeza kuwa wakifanikiwa kushinda ubingwa huo itaonyesha taratibu wanarejea kwenye ubora wao ambao wameupoteza kwa muda mrefu.

Laporta anataka kuhakikisha anairudisha Klabu ya Bracelona kwenye zama zake baada ya kuichukua chini ya rais aliyepita Josep Maria Bartome.

Hii ni mara ya pili kwa Laporta kuiongoza klabu hiyo.

344,733/-

# WATUBAKI KUWASHA MOTO MPYA 2023 NDANI YA DSTV

**Na Mwandishi Wetu**

KUNDI maarufu la vijana wachekeshaji la Watubaki, limetimiza miaka miwili ya kuonyesha manjonjo yao katika chaneli ya Maisha Magic Poa ndani ya DStv.

Vijana hao machachari wamekuwa kivutio kikubwa kwa watazamaji wa televisheni ndani na nje ya nchi na umaarufu wao umekuwa ukiongezeka siku hadi siku huku wakiendelea kuongeza idadi ya wafuasi wao baada ya kuanza kuonekana kupitia DStv ambayo inaonekana katika nchi mbalimbali barani Afrika.

Watubaki limeundwa na vijana wenye vipaji vya uchekeshaji 12 ambapo pia wamekuwa na program maalum ya kukuza vipaji kwa vijana wenzao na kwa sasa wana jumla ya vijana 15 ambao wamefuzu kusimama jukwaani na kuchekesha kwa ustadi.

Kundi hili ambalo liliundwa rasmi Novemba 2020 wakati mlipuko wa UVIKO-19 ulipotokea, lilifanikiwa kusimama imara na kuhakikisha kuwa Watanzania wanaendelea kupata burudani hata katika nyakati za changamoto hususan kipindi hicho ambacho watu wengi walikuwa wakitegemea televisheni kwa habari na burudani kwa kiasi kikubwa.

Akizungumza katika hafla fupi ya kuadhimisha miaka miwili ya Watubaki ndani ya DStv, Kaimu Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Shumbana Walwa, alisema wakati wote MultiChoice imekuwa mstari wa mbele katika kuibua na kukuza vipaji hususan kwenye tasnia ya uzalishaji wa maudhui na kitendo cha kuwapa ulingo vijana hao ni ushahidi tosha kuwa wanatekeleza kwa vitendo azma hiyo.

"Nawapongeza sana vijana wetu hawa kwa kufanikiwa kuwapo DStv kwa miaka miwili sasa na bado wataendelea kuwapo. Hii inaonyesha kuwa mnafanya kazi nzuri na mnajiongeza na kuboresha maudhui yenu kuendena na wakati na mahitaji ya watazamaji. Kwa hakika mmefanya kazi kubwa sana na watazamaji wa Maisha Magic Poa wanatarajia makubwa zaidi mwaka 2023," alisisitiza Shumbana.

Desemba 23 (leo), ni siku rasmi ya kusherehekea mafanikio hayo makubwa ya kundi la Watubaki ndani ya Ukumbi wa Mlimani City ambapo onyesho hilo la kukata na shoka litarushwa siku maalum kupitia Maisha Magic Poa ndani ya DStv.



Mshambuliaji wa Yanga Princess, Blessing Nkor, akimiliki mpira dhidi ya beki wa Simba Queens, Daniella Kanyanya, kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DUBE, MBOMBO

INATOKA UK. 32

mamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 44 ikifuatiwa na Simba yenye pointi 38, moja mbele ya Azam FC iliyoko nafasi ya tatu baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 17.

Simba na Azam zilivutwa shati juzi na Kagera Sugar na Geita Gold FC, baada ya kulazimishwa sare ugenini, hivyo kutoa nafasi kwa Yanga kuongeza wigo wa pointi ambayo siku moja kabla ilishinda 3-0 nyumbani dhidi ya Coastal Union.

# SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS

INATOKA UK. 32

ganisha kwa kichwa mpira wa kona iliyopigwa na Aniela.

Mwanzoni mwa kipindi cha pili, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, alifanya mabadiliko ya wachezaji wawili kwa mpigo, akiwatoa Koku Kipanga na Pambani Kuzoya akiwaingiza Vivian na Asha Djaffar ambayo kwa kiasi kikubwa yalileta mabadiliko.

Alikuwa na Vivian aliyeisawazishia Simba Queens bao la kusawazisha dakika 58 kwa shuti kali la mbali baada ya kugundua kuwa kipa Safia amesogea mbele langoni.

Timu hizo ziliendelea kushambuliana kwa zamu, lakini wachezaji wa timu zote mbili wakikosa mabao mengi, na hadi mwamuzi Tatu Malongo alipopuliza kipenga cha kumaliza mechi hiyo ubao ulisomeka sare ya bao 1-1.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/12/22 | 18:00 | Everton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.31 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/12/22 | 18:00 | Bristol City vs West Bromwich Albion | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 03. 26/12/22 | 18:00 | Rotherham United vs Stoke City | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 04. 26/12/22 | 18:00 | Burton Albion vs Lincoln City | 2.37 | 3.30 | 2.90 |
| 05. 26/12/22 | 18:00 | Cambridge United vs Shrewsbury Town | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 06. 26/12/22 | 18:00 | Charlton Athletic vs Peterborough United | 2.70 | 3.30 | 2.55 |
| 07. 26/12/22 | 18:00 | Exeter City vs Portsmouth FC | 2.65 | 3.35 | 2.55 |
| 08. 26/12/22 | 19:00 | FC Annecy vs AS Saint-Etienne | 2.90 | 3.25 | 2.37 |
| 09. 26/12/22 | 20:00 | Goztepe Izmir vs BB Bodrumspor | 2.50 | 3.35 | 2.65 |
| 10. 26/12/22 | 20:15 | Cardiff City vs Queens Park Rangers | 2.48 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 26/12/22 | 22:45 | Royal Charleroi SC vs RSC Anderlecht | 2.80 | 3.45 | 2.38 |
| 12. 26/12/22 | 22:45 | Luton Town vs Norwich City | 2.75 | 3.30 | 2.50 |
| 13. 26/12/22 | 23:00 | Valenciennes FC vs Amiens SC | 2.46 | 3.20 | 2.85 |
| 14. 26/12/22 | 23:00 | Pau FC vs Paris FC | 2.95 | 3.20 | 2.38 |
| 15. 26/12/22 | 23:00 | Quevilly-Rouen Metropole vs Grenoble Foot | 2.46 | 3.05 | 2.95 |
| 16. 26/12/22 | 23:00 | SC Bastia vs SM Caen | 3.05 | 3.10 | 2.38 |
| 17. 26/12/22 | 23:00 | Nimes Olympique vs EA Guingamp | 2.90 | 3.25 | 2.40 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 23/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5543 | Philippines vs Brunei Darussalam | 1.01 | 14.55 | 48.50 |
| 14:00 | 5020 | Bhayangkara Surabaya Utd vs Arema | 2.74 | 2.93 | 2.54 |
| 14:30 | 4536 | Perth Glory vs Wellington Phoenix | 2.78 | 3.37 | 2.39 |
| 15:00 | 1550 | Neftchi Baku vs Keshla FK | 1.28 | 4.76 | 9.13 |
| 15:00 | 1816 | Chengdu Qianbao vs Wuhan Three Towns FC | 3.37 | 3.76 | 1.86 |
| 15:00 | 2203 | Shanghai SIPG vs Shandong Luneng | 4.29 | 3.65 | 1.69 |
| 15:00 | 5575 | Shanghai Shenhua vs Shijiazhuang | 2.24 | 3.15 | 3.25 |
| 15:50 | 3628 | City Football Club vs Fursan Hispania FC | 1.89 | 3.55 | 3.45 |
| 16:00 | 1378 | Marines FC Gisenyi vs Kiyovu Sports | 7.19 | 3.98 | 1.41 |
| 16:00 | 3058 | AS Ashdod vs Ahi Nazareth | 3.21 | 3.31 | 2.19 |
| 16:00 | 3182 | Maccabi Petach Tikva vs Nazareth Ilit | 1.53 | 4.08 | 5.78 |
| 16:00 | 3373 | Hapoel Kfar Saba vs Hapoel Rishon Lezion | 2.46 | 3.15 | 2.90 |
| 16:00 | 3478 | Ironi Tiberias vs Hapoel Acre | 2.10 | 3.25 | 3.50 |
| 16:00 | 4052 | Maccabi Jaffa vs Hapoel Ramat Gan | 1.93 | 3.35 | 3.95 |
| 16:15 | 3268 | Pusamania Borneo vs PSM Makassar | 1.94 | 3.40 | 3.85 |
| 16:30 | 1441 | Padova vs Pro Vercelli | 2.13 | 3.15 | 3.55 |
| 17:00 | 3798 | Bengaluru FC vs Hyderabad FC | 3.21 | 3.40 | 2.02 |
| 17:30 | 2763 | FK Sumgayit vs Sabah | 7.01 | 4.28 | 1.38 |
| 17:30 | 4150 | Pafos FC vs Akritas Chlorakas | 1.21 | 6.21 | 12.01 |
| 18:00 | 2404 | El Ittihad Alexandria vs Ceramica Cleopatra | 2.20 | 2.89 | 3.64 |
| 18:30 | 5121 | Asi D Abengourou vs Sporting Gagnoa | 4.38 | 2.87 | 1.91 |
| 19:00 | 3434 | Rayon Sports FC vs Gasogi United | 1.93 | 3.01 | 3.98 |
| 20:00 | 1185 | El Daklyeh vs Pyramids | 7.77 | 3.73 | 1.47 |
| 20:00 | 3319 | Antalyaspor vs Ankaragucu | 1.94 | 3.58 | 3.58 |
| 20:00 | 3988 | Anorthosis Famagusta vs Karmiotissa | 1.49 | 4.20 | 6.20 |
| 20:00 | 4203 | Umraniyespor vs Basaksehir | 3.83 | 3.48 | 1.90 |
| 20:00 | 4589 | AEL Limassol vs Olympiakos Nicosia | 1.67 | 3.66 | 5.01 |
| 20:30 | 2036 | RFC Seraing vs Eupen | 2.79 | 3.28 | 2.43 |
| 21:00 | 5940 | Stade Abidjan vs SOL FC | 3.40 | 2.95 | 2.28 |
| 22:00 | 3453 | Vilafranquense vs Mafra | 2.14 | 3.27 | 3.22 |
| 22:30 | 1902 | Taranto Sport vs Monopoli | 2.82 | 3.07 | 2.57 |
| 22:30 | 2927 | KAA Gent vs Standard Liege | 1.61 | 3.97 | 4.96 |
| 22:30 | 3435 | Latina vs Foggia | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 22:30 | 3959 | Mechelen vs Cercle Brugge | 2.60 | 3.45 | 2.50 |
| 22:30 | 5639 | Ross County vs Rangers | 8.18 | 5.18 | 1.32 |
| 22:45 | 1279 | Falkirk FC vs Queen of South | 2.16 | 3.51 | 2.96 |
| 22:45 | 2166 | Partick Thisle vs Inverness | 1.92 | 3.50 | 3.59 |
| 22:45 | 2558 | Ayr United vs Dundee FC | 2.45 | 3.40 | 2.61 |
| 22:45 | 3012 | Gap Connahs Quay vs The New Saints | 4.38 | 3.84 | 1.64 |
| 22:45 | 3584 | Raith Rovers vs Morton | 2.19 | 3.11 | 3.26 |
| 22:45 | 4196 | Haverfordwest vs Aberystwyth Town | 1.67 | 3.80 | 4.18 |
| 22:45 | 4281 | Bala Town vs Airbus UK Broughton | 1.05 | 9.78 | 23.48 |
| 22:45 | 4707 | Montrose vs Airdrieonians | 2.47 | 3.36 | 2.62 |
| 22:45 | 4951 | Flint Town United vs Caernarfon Town | 2.40 | 3.37 | 2.59 |
| 22:45 | 5289 | Motherwell vs Kilmarnock | 2.04 | 3.34 | 3.49 |
| 22:45 | 5694 | Pontypridd Town vs Penybont | 2.81 | 3.40 | 2.22 |
| 22:45 | 5744 | Arbroath vs Queens Park | 2.57 | 3.26 | 2.57 |
| 22:45 | 5795 | Clyde vs Alloa Athletic | 3.69 | 3.65 | 1.85 |
| 22:45 | 5914 | Cove Rangers vs Hamilton | 2.20 | 3.41 | 2.96 |
| 23:15 | 1889 | Rio Ave vs Maritimo | 2.03 | 3.29 | 3.59 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Ijumaa Desemba 23, 2022

Nipashe



UKURASA 29

**Sura ya Messi kuwekwa kwenye noti Argentina**

# DUBE, MBOMBO WAIPASUA KICHWA YANGA SC JUMAPILI

## ●●●Yawahi kambini kuwatafutia dawa, kocha asema inabidi…

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inaendeleza mbio zake za ubingwa kwa kung'ang'ania kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara, Yanga imewahi kambini mapema tayari kwa kuiwinda Azam FC, kuelekea mchezo wao Jumapili wiki hii.

Yanga wanaingia kambini leo kwa ajili ya maandalizi ya mchezo huo ambao watakuwa ugenini kukabiliana na wenyeji wao, Azam FC, katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wameanza maandalizi ya mchezo huo dhidi ya Azam FC baada ya kumalizana na Coastal Union, mechi ambayo iliwaonyesha mapungufu ya kwenda kuyafanyia kazi.

Alisema maandalizi hayo yameanza rasmi kwa kufanyika kazi safu yao ya ulinzi kulingana na umahiri wa safu ya ushambuliaji ya Azam FC inayoongozwa na Price Dube akisaidiana na Idrissa Mbombo.

"Hii mechi ni ngumu ya ushindani mkubwa kwa sababu tunahitaji kupata matokeo chanya yenye alama tatu, lakini wapinzani wetu wanahitaji hizo alama pia, tunatakiwa kujiandaa vizuri kwa kufanyia kazi madhaifu yetu ili kufikia malengo.

"Tunatambua Azam FC wana timu nzuri, wana wachezaji wazuri kila idara, kikubwa kabla ya kuwaangalia wapinzani wetu tunalazimika kujiimarisha madhaifu yetu na kuangalia ubora wao," alisema kocha huyo.

Alisema malengo yao makubwa ni kukusanya alama muhimu katika kila mechi kwa lengo la kutetea ubingwa waliokuwa nao mwishoni mwa msimu na wasipokuwa makini kupata pointi mechi yao ijayo itawaweka katika wakati mgumu.

Kaze alisema kikosi kinaingia kambini leo kwa ajili ya maandalizi ya mchezo huo na kuendelea kuwasisitiza wachezaji wao kuwa makini na kujitoa kila mechi kwa ajili ya kupata matokeo chanya.

Yanga ipokileleni mwa msi-

INAENDELEA UK. 31



Dube

## Simba Queens, Yanga Princess hakuna mbabe

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa kimataifa wa Nigeria, Chioma Wogu na Vivian Corazone kutoka Kenya, jana walizifungia mabao timu za soka za wanawake, Simba Queens na Yanga Princess, zikitoka sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ilikuwa ni mechi ya 'dabi' ya timu za wanawake, mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa upande wa wanawake ambayo ipo raundi ya tatu.

Mnigeria Chioma alianza kuipatia Yanga Princess bao, ambao walikuwa wageni kwenye mechi hiyo, kabla ya Mkenya Vivian aliyetokea benchini kusawazisha.

Matokeo hayo yanazifanya timu hizo kuwa na pointi nne kila moja na kupanda nafasi moja, Simba Queens ikitoka nafasi ya nne hadi ya tatu, na Yanga Princess ikipanda hadi nafasi ya nne kutoka ya tano.

Mechi ilianza kwa staili ya butuabutua, kila timu ikipiga mipira mbele bila mipango kitu ambacho kilisababisha kuchezwa kwa dakika 27 bila shambulizi lolote lile la maana.

Yanga Princess ndiyo ilianza kufanya shambulizi la hatari dakika ya 28, wakati mabeki wa Simba Queens walipokosea kuuokoa mpira ukarejea kwenye lango lao na kumkuta winga wa kushoto, Aniela Uwimana raia wa Burundi, akiwa peke yake na kipa Janeth Shija, lakini aliuzuia vibaya, kipa akawahi kudaka.

Dakika tano baadaye Yanga Princess ilirejea tena kwenye lango la Simba Queens, kwa mara nyingine tena Aniela alibaki peke yake na kipa Janeth, lakini mabeki wa Simba waliwahi na kufagia hatari hiyo.

Bessing Nkor nusura aipatie Yanga bao dakika ya 40 baada ya kutokea purukushani kwenye lango la Simba Queens, shuti lake likapaa juu ya lango.

Shambulio la hatari kwa Simba kwenye lango la wapinzani wao lilikuwa dakika ya 41, baada ya krosi ya Aisha Juma kumkuta Jentrix Shikangwa ambaye alipiga mpira kichwa ulilotemwa na kipa Safia Salifu, lakini ukakosa muunganishaji.

Dakika ya 45 Yanga Princess iliandika bao la kwanza lililowekwa wavuni na Chioma, aliporuka juu na kuun-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >